# Nipashe

Jumanne Machi 10, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580175

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Baada ya siku 735 hukumu ya kesi kina Mbowe leo

UKURASA 3




UKURASA 13

# Polisi: Mangula amelishwa sumu

UKURASA 2





## JELA MAISHA KWA KUBAKA MWANAWE WA KAMBO

UKURASA 3

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa taarifa ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Philip Mangula (picha ndogo), kulishwa sumu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mawaziri wa Afya SADC wajifungia kujadili corona

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu


**MICHEZO** EYMAEL AFUNGUKA ALIPOIBANA SIMBA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA



Rais John Magufuli akiongoza kikao cha Baraza la Mawaziri Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Polisi: Mangula amelishwa sumu

**Na Mary Geofrey**

KAMANDA wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, amedai Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Philip Mangula, amelishwa sumu.

Amesema jeshi hilo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama na taasisi mbalimbali katika uchunguzi waliofanya, walibaini ndani ya mwili wa Mangula kulikuwa na sumu baada ya kuanguka ghafla hivi karibuni na kulazwa kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Kamanda Mambosasa aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo, akisema walipokea taarifa kutoka kwa uongozi wa chama hicho Machi 2 mwaka huu, kuwa Mangula amewekewa sumu.

Februari 29 mwaka huu, Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, ilitoa taarifa kuhusu Rais John Magufuli kwenda MNH kumjulia hali Mangula, ikieleza kuwa alikuwa akipatiwa matibabu kwenye Chumba cha Wagonjwa Wanaohitaji Uangalizi Maalum (ICU) cha hospitali hiyo baada ya kudondoka ghafla akiwa ofisini kwake Lumbumba jijini Dar es Salaam, siku moja baada ya kufanyika kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM.

Kikao hicho kilikuwa kikijadili masuala mbalimbali likiwamo la adhabu ya wanachama watatu; waliokuwa makatibu wakuu wa chama hicho, Yusuph Makamba na Abdulrahman Kinana na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Benard Membe, waliokuwa na tuhuma za ukiukwaji wa maadili ndani ya CCM.

Mambosasa alisema kuwa katika taarifa waliyopokea kutoka uongozi wa chama hicho, walielezwa kuwa Mangula alipelekwa MNH na alilazwa ICU.

"Jeshi likishirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama na taasisi mbalimbali katika uchunguzi tuliofanya, tulibaini kwamba ndani ya mwili wa Mzee Mangula kulikuwa na sumu. Uchunguzi kuhusu namna sumu hiyo ilivyoingia mwilini mwake bado unaendelea kufanyika," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam litachukua hatua kali kwa mtu yeyote atakayebainika kupanga, kuratibu na kutekeleza uhalifu huo.

"Jeshi la Polisi litachukua hatua kali, awe ni mwana familia, kutoka ndani ya chama, nje au ndani ya chama, ndani au nje ya nchi au awe serikalini au chama chochote cha siasa, tutamchukulia hatua," alisisitiza.

Hii si mara ya kwanza kwa viongozi na wanachama wa CCM kuripotiwa kulishwa sumu. Hivi karibuni, Rais Magufuli alifichua jinsi alivyokumbana na baa hilo mkoani Dodoma wakati wa uongozi wa Rais wa awamu ya tano, Benjamin Mkapa.


DANISH REFUGEE COUNCIL

**TANGAZO LA ZABUNI**

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUNUNUA VITENGE

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAALIKA WAZABUNI **KULETA BEI ZAO.**

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE **10.03.2020 HADI TAREHE 24.03.2020 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI.** TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

***KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA* +255627428470**
au ***barua pepe*** **jackson.maseke@drc.ngo**

**ZABUNI ZITAFUNGULIWA HADHARANI TAREHE 26.03.2020 SAA 4:00 ASUBUHI** OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISHI.

**UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA**
**RFQ.TZA@drc.ngo**
**AU KULETA MOJA KWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.**

215661702



UNHCR
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**REQUEST FOR PROPOSAL: No. RFP/2020/SUP/001**

**FOR THE ESTABLISHMENT OF FRAME AGREEMENTS FOR PROVISION OF ROAD CARGO AND PASSENGERS TRANSPORT SERVICE IN TANZANIA.**

**1. Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Tanzania, invites qualified suppliers to make a firm offer for the establishment of Frame Agreement(s) for the provision of Road Cargo and Passengers transportation services (referred to hereinafter as services).

UNHCR may award Frame Agreement(s) with initial duration of 2 (two) years, potentially extendable for a further period of 1 (one) year. The successful bidder(s) will be requested to maintain their quoted price proposal for the duration of the Frame Agreement(s).

**2. Eligibility:**

Service providers or traders duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's needs are invited to participate in the bidding process.

The tender documents can be collected from the following UNHCR Offices:

UNHCR Representation Office Tanzania
Plot 1658 Masaki, Rufiji Street
P.O Box 2666 - **Dar es Salaam, Tanzania**

UNHCR Sub- Office Kibondo
Kabigwa (Near TANESCO)
P.O. Box 49
**Kibondo**

UNHCR Field Office Kasulu
Kimobwa (Mlimani Area)
P.O. Box 332 - Kasulu,
**Kigoma**

UNHCR Field Unit Mwanza
Mwanza Airport
P.O. Box 2273 – **Mwanza**

**CRUCIAL DATES FOR THIS REQUEST FOR PROPOSAL**

| | |
|---|---|
| Deadline for receiving requests for clarification | Tuesday 22nd March 2020 at 23.59 hours EAT |
| Suppliers' conference meeting | Wednesday 25th March 2020 at 11.00hours EAT |
| Deadline for submission of offers | Tuesday 14th April 2020 at 16.00 hours EAT |

***UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.***

215661402


# Mawaziri Afya SADC wajifungia kujadili corona

**Na Gwamaka Alipipi**

MLIPUKO wa ugonjwa wa virusi vya Corona duniani, umewakutanisha kwa dharura jijini Dar es Salam mawaziri wa sekta ya afya kutoka nchi 16 wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kujadiliana namna ya kukabiliana na baa hilo.

Ugonjwa huo ambao uligundulika mwaka jana China katika Jiji la Wuhan lililoko Jimbo la Hubei na kupewa jina la COVID-19, hadi kufikia jana, ulikuwa umesababisha vifo vya zaidi ya watu 3,800 duniani huku 100,008 wakiwa wameambukizwa.

Ugonjwa huo ambao umeshaathiri zaidi nchi za Italy, Iran, Korea Kusini, tayari umeripotiwa kuingia katika baadhi ya nchi za Afrika zikiwamo Misri, Nigeria, Afrika Kusini, Algeria, Cameroon na Togo na vifo kadhaa vimesharipotiwa.

Nchi nyingi duniani zimeanza kuchukua tahadhari katika mipaka yake ikiwamo viwanja vya ndege kwa kuweka vipimo vya kuwapima abiria wanaoingia katika nchi zao.

Mawaziri hao wa SADC walijifungia jana jijini Dar es Salaam kuanzia majira ya saa tatu asubuhi hadi saa 12 jioni wakiongozwa na mwenyeji wao, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa Tanzania, Ummy Mwalimu.

Ilielezwa kuwa katika kikao hicho, mawaziri hao walijadiliana namna ya kuisaidia kikanda kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa huo.

Athari kubwa zaidi za mlipuko wa virusi hivyo zimeonekana China ingawa Jumapili nchi hiyo iliripoti idadi ya chini zaidi ya maambukizo mapya katika siku moja tangu Januari.

Iran pia ni moja ya maeneo yenye maambukizo mabaya zaidi nje ya China ambayo sasa imethibitisha kuwa na maambukizo 6,566 na vifo 194.

HABARI KITAIFA

# Jela maisha kubaka mtoto wa kambo

**Daniel Limbe, CHATO**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Chato mkoani Geita, imemhukumu Makoye Mwinamila kutumikia kifungo cha maisha jela baada ya mkazi huyo wa Kijiji cha Mulumba, Kata ya Bwina wilayani hapa, kupatikana na hatia ya kumbaka mtoto wake wa kambo.

Hukumu hiyo ilitolewa jana baada ya Upande wa Mashtaka kukamilisha maelezo na ushahidi uliotolewa mbele ya mahakama hiyo.

Mwinamila alifikishwa mahakamani hapo akidaiwa kufanya ukatili huo dhidi ya mtoto huyo (jina tunalihifadhi) baada ya kumwacha mkewe sokoni akiuza mahindi.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Anosisye Erasto, akishirikiana na Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Mauzi Lyawatwa, walidai mahakamani kuwa mshtakiwa alitenda ukatili huo, akimtishia kumuua iwapo angepiga kelele wakati akimwingilia kingono.

Walidai mahakamani hapo kuwa kitendo cha kumwingilia mtu kimwili pasipo ridhaa yake ni kinyume na kifungu cha 130 (1)(2)(e) pamoja na cha 131(3) cha Sheria ya Makosa ya Jinai Sura ya 16 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa kabla ya mtoto huyo kutendwa ukatili huo, baba na mama waliondoka nyumbani kwao majira ya asubuhi na kwenda Kitongoji cha Budili kuuza mahindi.

Ilidaiwa kwamba, wakiwa Budili, hali ya hewa ilibadilika na kuonyesha mawingu mazito ya mvua hivyo mke wa mshtakiwa, Paulina John, akamshauri mumewe kurudi nyumbani ili kuondoa mahindi yaliyokuwa yameanikwa juani.

Ilidaiwa mahakamani hapo na upande wa mashtaka kuwa, mama aliwaona watoto wake wanne wadogo wakifika eneo lake la biashara huku binti yake (mwathirika wa tukio) akiwa kabaki nyumbani, na alipotaka kufahamu sababu za kwenda eneo lake la biashara, walimweleza kuwa baba yao ndiyo kawaagiza.

Ilidaiwa mahakamani kuwa, kutokana na hali hiyo, mama wa watoto hao alilazimika kurejea nyumbani haraka na kumkuta mumewe kitandani akifanya ukatili huo dhidi ya mwanaye na akalazimika kupiga yowe kuomba msaada kwa majirani, waliojitokeza na kumkamata mshtakiwa.

Baada ya maelezo ya pande zote, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Odira Amworo, alisema mahakama yake imejiridhisha pasipo kuacha shaka kuwa mshtakiwa anayo hatia, lakini akampa nafasi ya kujitetea ili apunguziwe adhabu.

Mshtakiwa aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwa madai kuwa hilo ni kosa lake la kwanza kutenda kwa kipindi chote cha maisha yake na kwamba anategemewa na familia pamoja na wazazi wake ambao ni wazee.

Licha ya utetezi huo, mahakama ilitoa hukumu ya kifungo cha maisha jela, Hakimu Amworo akisema adhabu hiyo inapaswa kuwa fundisho kwa watu wengine ambao wamekuwa wakifanya au kukusudia kufanya ngono pasipo ridhaa ya wenzao.

# Hatima kina Mbowe kortini leo

**Na Hellen Mwango**

LEO ni hukumu, ikiwa inatimu miaka miwili na siku tano, tangu kuanza kwa kesi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, na viongozi wanane waandamizi wa chama hicho.

Katika kesi hiyo inayosikilizwa na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, vigogo hao wanakabiliwa na mashtaka 13, wakituhumiwa kwa uchochezi, katika kesi iliyoanza kusilikizwa Machi 7, 2018 na Hakimu ambaye sasa ni Jaji, Wilbard Mashauri.

Mbali na Mbowe, wengine ni aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji na Katibu Mkuu wa sasa, John Mnyika, Naibu Katibu Mkuu visiwani, Salum Mwalimu na Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chadema (Bawacha) na mbunge, Halima Mdee.

Wabunge wengine ni Esther Matiko, Esther Bulaya, Mchungaji Peter Msigwa na John Heche. Katika kesi hiyo, baadhi ya washtakiwa waliwekwa mahabusu kwa miezi mitatu kutokana na kukiuka masharti ya dhamana.

Machi 14 mwaka jana, jalada hilo lilihamishiwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, baada ya Hakimu Mashauri kupandishwa cheo na kuwa Jaji.

Hakimu Simba alitoa mwongozo kwa mawakili wa pande zote mbili ili kuzuia ucheleweshaji wa kusikilizwa kesi hiyo.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na 16, mwaka 2018, wakiwa Kinondoni jijini Dar es Salaam, kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani kwa kutenda kosa la jinai na kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Inadaiwa washtakiwa wote katika tarehe hiyo wakiwa kwenye barabara hiyo, kwa pamoja wakiwa wamekusanyika wao sita na wenzao 12 ambao hawako mahakamani, wakiwa katika maandamano au mkusanyiko wenye vurugu na kutozingatia amri ya kusitisha maandamano iliyotolewa na askari, waligoma kutawanyika na kuendelea na mkusanyiko huo wa vurugu uliosababisha kifo cha Akwilina Akwiline na majeraha kwa askari wawili.

Katika shtaka ambalo linamkabili Heche peke yake, inadaiwa Februari 16 mwaka huo, katika Viwanja vya Buibui Kinondoni katika mkutano wa hadhara, alitoa maneno ya chuki dhidi ya serikali.

Inadaiwa alisema "kesho patachimbika, upumbavu ambao unafanywa kwenye nchi hii... wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano, watu wanapotea... watu wanauawa, wanaokotwa katika mitaro, lazima ukome", maneno ambayo yanadaiwa kusababisha chuki ya wananchi dhidi ya serikali.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi. ulifunga ushahidii ukiwa na mashahidi wanane huku Upande wa Utetezi uliongozwa na Wakili Peter Kibatala, ukiita mashahidi watano.

Hati ya mashtaka ya awali ilikuwa na mashtaka 12 yakiwamo ya kufanya mkusanyiko usio halali, lakini hati mpya iliyopo ina mashtaka 13 likiwamo la kufanya maandamano yasiyo halali wakiwa na lengo la kuvamia Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni.




## TANGAZO KWA UMMA

### MATUMIZI MABAYA NA YA UDANGANAYIFU YA JINA LA BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA (AfDB)

Tumepata taarifa za mawakala mbalimbali wanaojivika nafasi za uongo za kusaidia katika kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa nia ya kujipatia fedha. Udanganyifu huu mara nyingi hufanywa kwa kupitia barua-pepe, au njia nyingine za mawasiliano.

Benki ya Maendeleo ya Afrika inasikitishwa sana na udanganyifu huu, ambao ni ukiukwaji wa maadili ya taasisi, na itashirikiana na mamlaka zinazohusika kupambana na mtandao huo wa ulaghai.

Sisi, Benki ya Maendeleo ya Afrika, tunathibitisha kwamba:

- Tunatangaza waziwazi maombi yote ya manunuzi ya taasisi kwenye tovuti ya Benki, ambayo ni: **www.afdb.org/en/about-us/corporate-procurement**. Ikiwa ombi lolote la manunuzi halijatangazwa kwenye tovuti hiyo, ombi hilo halipo, ni ulaghai.
- Hatudai wala kupokea malipo kutoka kwa watoa huduma, wagavi, wataalamu-washauri, wanaotafuta ajira, n.k., ili kuwapa mikataba ya kutoa huduma, ugavi wa bidhaa au malipo ili kutoa ajira.
- Hatutumii anuani za barua-pepe kama vile Gmail, Yahoo Mail n.k.
- Tunatangaza nafasi zote za ajira kwenye tovuti yetu: **www.afdb.org/jobseekers**. Kama nafasi ya ajira haijatangazwa kwenye tovuti hiyo, nafasi hiyo haipo, ni ulaghai.

Kwa hiyo, tunawashauri watu wote, pamoja na wafanya biashara wanaopenda kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuzingatia yafuatayo:

- Zingatia matangazo yanayohusu manunuzi, ambayo yanapatikana kwenye tovuti ya Benki tu, na si kwingineko.
- Kamwe usilipe au kutuma fedha kwa mtu yeyote ili kupata kazi, mkataba wa huduma au kufanya biashara yoyote na Benki.
- Toa taarifa za majaribio yote ya udanganyifu kwa mamlaka zinazohusika za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na pia ifahamishe Benki kupitia anwani hii ya barua-pepe: **security@afdb.org.**

215653002

# 'Wazee wa tuma kwa namba hii' kortini

Na Hellen Mwango

WAKAZI watatu wa Sumbawanga maarufu kama 'Wazee wa tuma pesa kwa namba hii' wamewafikisha mahakamani wakikabiliwa na shtaka moja la kutuma ujumbe wa upotoshaji kwa Katibu wa Mawasiliano wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Dk. Maria Sasabo.

Washtakiwa hao ni, Japhet Mzuri (22), mkazi wa Makoko Stree Sumbawanga, Joseph Richard (24), mkazi wa Sumbawanga pamoja na Justin Sadoki (25), mkazi wa Kashai Mmoka, Sumbawanga.

Walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu, aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa Januari 18, mwaka huu, katika Wilaya ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa, washtakiwa hao walituma ujumbe ambao unasomeka 'chukua namba hii ndio utumie kutuma hiyo pesa 0757648067 jina litatokea Asha Mwamalekela'.

Simon alidai ujumbe huo ulitumwa kwa kwa Dk. Maria Sasabo, ambaye ni Katibu Mkuu wa Mawasiliano Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa lengo la kujipatia fedha kutoka kwake.

Baada ya kuona shtaka hilo washtakiwa wote walikana, upande wa mashtaka ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na waliomba kupangiwa tarehe ya kusoma hoja za awali.

Wakili Simon alidai hawapingi dhamana ya washtakiwa hao, lakini kutokana na sehemu wanayotoka wanaomba wapewe masharti ya dhamana ambayo yatawafanya kufika mahakamani kila tarehe ya kesi yao itakapotajwa.

Akitoa masharti ya dhamana, Hakimu Chaungu aliwataka kila mshtakiwa kuwa na wadhamini wawili ambao ni wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na watakaosaini bondi ya Sh. milioni 10, kila mmoja.

Hata hivyo, washtakiwa hao wamerudishwa rumande kwa kushindwa kutimiza masharti ya dhamana, kesi itakuja tena Machi 23, mwaka huu, kwa ajili ya washtakiwa kusomewa hoja za awali ili kesi ianze kusikilizwa.



Watuhumiwa watatu wa wizi wa kutumia mitandao, wakiwa chini ya ulinzi wa askari polisi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kusomewa shtaka moja la kutuma ujumbe wa upotoshaji kwa Katibu wa Mawasiliano wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Dk. Maria Sasabo. **PICHA: MIRAJI MSALA**


**The Guardian Limited**

**JOB VACANCY**

**The Guardian Limited ,publisher of leading Tanzania newspapers, The Guardian and Nipashe, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:**

**CIRCULATION FIELD OFFICER – DAR ES SALAAM**

**Job Purpose:**
To boost copy sales and develop relationships with agents and vendors in the sales channel in the assigned area to meet your set sales targets.

**Main Responsibilities:**

The successful candidates will be responsible for the following key results:
- Work with the agents and vendors in making sure that the business grows and The Guardian Limited publications are available and visible and sold at the set retail prices with optimal return levels.
- Develop and grow more channels of distribution.
- Monitor indicators relating to market arrivals, circulation sales and returns indicators and make appropriate reports to Circulation Supervisor.
- Identify and build rapport with existing and potential customers by communicating the benefits of Selling The Guardian and Nipashe.
- Monitor newspaper distribution and sale trends in particular areas, prepare weekly sales plans and update supervisor on a regular basis.
- Monitor daily performance of TGL brands in your particular areas of operation in comparison to our rival publications and make reports that guide growth strategies.
- Open up new markets in particular areas of operation that will in turn translate into higher sales.
- Attend customer complaints that in one's particular area of operation so as to maintain good customer relations and protect the company's interests.
- Liaise with supervisor in credit control and debt management within particular area of operation.
- Submit daily and weekly reports on progress on activities, including meeting set sales targets.
- Manage debt collection and credit control within one's respective area operation.
- Demonstrate ability to work under minimum supervision.

**Minimum Qualifications and Experience:**

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 2 year's relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge, and familiarity with a wide range of newspapers brands.

**MODE OF APPLICATION:**
Apply online via HRO email address: ;**vacancy@guardian.co.tz** by March 13, 2020

NB: Only shortlisted candidates will be contacted.

***The Guardian Limited is an equal opportunity employer.***

615654302


# Waziri aibua madudu miradi ya maji

Na Augusta Njoji, DODOMA

NAIBU Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, amesema miradi 153 ya maji ambayo haitoi maji na kuiita kuwa ni kichefuchefu na imekuwa ikifedhehesha wizara hiyo.

Sambamba na hiyo, ameagiza Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) kupitia upya gharama za maji vijijini kwa kuwa ni kubwa ikilinganishwa na mijini.

Aweso alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akifungua mkutano wa mrejesho wa uhakiki na tathmini ya utekelezaji wa mpango wa malipo kwa matokeo awamu ya nne (PBR) inayotekelezwa kwa ufadhili wa Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID). Pia aliiagiza Ruwasa kuweka mikakati ya kukarabati miradi ambayo inagharimu zaidi ya Sh. bilioni 66 ili wananchi wapate huduma ya maji kwa kuwa imekuwa ikiichefua wizara.

"Wizara yetu imerithi dhambi kama Yesu. Kwa mfano miradi ile 153 ni ya kichefuchefu ambayo inatufedhehesha sisi. Kuna kazi kubwa tumeifanya na inaonekana lakini hii sasa ndiyo inatuchafua. Lazima tuiwekee mpango mkakati kama Ruwasa ilivyojipanga," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema miradi hiyo imekuwa ikiharibu taswira ya wizara huku akisema uwezo wa kurekebisha upo.

"Tunaweza na tuna uwezo huo na Ruwasa ni jeshi kubwa mtaweza kuifanya kwa haraka," alisema.

Kuhusu gharama za maji, Aweso alisema uniti moja ya maji kwa jiji la Dar es Salaam ni Sh. 1,800 sawa na ndoo za maji 50 huku wananchi vijijini wakinunua maji uniti moja kwa Sh.5,000 jambo ambalo linawaumiza wananchi.

"Nikuombe sana Mkurugenzi wa Ruwasa jukumu letu ni kuhakikisha mwananchi wa mijini na vijijini wanapata huduma nafuu. Lazima tuangalie namna ya kumpa mwananchi unafuu, vijijini wananunua maji kwa gharama kubwa," alisema.

Akizungumzia jumuiya za watumiaji, Aweso alisema kumekuwa na tatizo la usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji licha ya serikali na wadau wa maendeleo kuwezesha upatikanaji wa maji.

"Lakini tatizo uendelevu wa miradi kuna miradi inakufa kwasababu jumuiya haina hata utaalamu tu wa kufunga koki haiwezekani, jumuiya zinazosimamia miradi ya maji ziwe jumuiya za kula kula tu, kesho anapewa mwenyekiti au katibu. Ukienda kwenye akaunti hakuna kitu," alisema.

Aliagiza Mkurugenzi wa Ruwasa kupitia jumuiya hizo na zile ambazo hazina uwezo za kula kula fedha zifutwe. Naye Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mhandisi Anthony Sanga, alisema kuna kero kubwa ya maji vijijini, hivyo bila kuwa na takwimu kwenye utendaji kazi watakwama.

Awali, Mkurugenzi wa Ruwasa, Mhandisi Clement Kivegalo, alisema katika awamu hiyo ya nne ya mpango huo ambayo inatekelezwa na Ruwasa, halmashauri 181 zilifuzu ambapo Sh. bilioni 63.46 zimetolewa.

"Hii ni sawa na ongezeko la takribani asilimia 110 ni zaidi ya mara mbili ya kiasi kilichotolewa katika awamu ya tatu, hata hivyo bado kuna maeneo ambayo tathmini inaonesha kuwa baadhi ya halmashauri hazikufanya vizuri katika vigezo vinavyotajwa," alisema.

Naye Mwakilishi wa Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID), Getrude Kihunrwa, alisema mradi huo umeleta matokeo chanya ikiwamo kuboreka kwa sekta za maji, idadi ya vituo kuongezeka na usahihi wa takwimu umepanda kutoka asilimia 20 mwaka 2014 hadi asilimia 40 mwaka huu.

TANGAZO


absa
Kadi inayobadili
muonekano wa kibenki
absa
4000 1234 5688 9010
AB SAMPLE
Prestige Debit
VISA
Jisajili leo kupata kadi yako ya kizazi kipya
Huo ndio Uafricanacity. Hiyo ndio Absa.
absa.co.tz
Vigezo na masharti kuzingatiwa.
Absa Bank Tanzania Limited (yenye usajili namba 38557) inaongozwa na kanuni za Benki Kuu ya Tanzania.
215661202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Utolewaji mikopo kwa wanawake upitiwe upya

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ameonyesha kutoridhishwa na utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake kwa Halmashauri ya Bariadi Mjini mkoani Simiyu, kwa kuwa inaonyesha kwenye makaratasi zaidi kuliko uhalisia.

Akihutubia mamia ya wananchi katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kitaifa iliyofanyika mkoani Simiyu juzi, alisema ni vyema vikahudumiwa vikundi vichache vitakavyotoa matokeo chanya kuliko kuwa na orodha ndefu.

Makamu wa Rais alisema kuwa alitembelea banda la Halmashauri ya Mji Bariadi, lakini hakuridhishwa mikopo inavyotoka, inatolewa, lakini haifikii vikundi.

Samia alieleza kuwa mikopo hiyo inatolewa kwa ajili ya kuwekwa kwenye taarifa kwamba vikundi kadhaa vimepata mikopo, ingawa lengo la mikopo hiyo ni kumwendeleza mwanamke na kuendeleza vikundi vya wanawake.

Kutokana na haki hiyo, alishauri kupunguzwa kwa utitiri wa vikundi, badala yake kushughulika na vikundi ambavyo vitatoa matokeo chanya kwa kuzalisha.

Pamoja na serikali kuweka utaratibu wa kuzitaka halmashauri zote nchini kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi ya wanawake, vijana na wenye ulemavu kutoka kwenye vyanzo vyao vya mapato, lakini makundi hayo katika halmashauri nyingi yamekuwa yakilalamikia kutoipata au kupata kiasi kidogo ambacho hakikidhi mahitaji ya kufanya shughuli za kiuchumi.

Kama mikopo hiyo inakosa uhalisia badala yake kutolewa ili kuweka kumbukumbu kwenye vitabu kuwa makundi hayo yanapewa mikopo hiyo, inakuwa imekosa maana.

Kundi la wanawake lililengwa kupawa mikopo hiyo lengo kubwa likiwa ni kuwatambua wanawake kuwa wana mchango mkubwa katika kuiendeleza familia, hivyo kama hawaipati tunaona kuwa kuna umuhimu kwa serikali kulifanyia tafakari ya kina kuona nini kifanyike kutimiza lengo hilo.

Serikali Kuu inaweza kujivua lawama kwa ni jukumu la halmashauri zetu, lakini tunachokiona ni kuwa halmashauri nyingi hazina wigo mpana wa vyanzo vya mapato, hivyo kushindwa kutoa mikopo kwa ajili ya makundi hayo.

Kwa kuwa Makamu wa Rais ameibaini changamoto hii mwenyewe, bila shaka kwa kutumia nafasi yake atalifikisha suala hili panapohusika ili kuitafutia ufumbuzi na kumaliza kikwazo cha uwezeshaji wa wanawake kiuchumi.

Hata hivyo, tunaamini kuwa serikali inaweza kutumia njia zingine za kuwawezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupitia njia zingine mbali na mikopo ya halmashauri, ambayo kimsingi imeonekana kuwa na changamoto ya kutokuwa na vyanzo vya kutosha vya mapato.

Tunatambua jinsi serikali yetu inavyowathamini wanawake hivyo kuwawekea mazingira mazuri ya kuwawezesha. Itakumbukwa kuwa uanzishaji wa iliyokuwa Benki ya Wanawake lengo lake lilikuwa ni kuliwezesha kundi hilo kiuchumi.

Tunaona kwamba kuna umuhimu sasa kwa serikali pia kutumia mifuko mingine kama Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) kusaidia uwezeshaji wanawake kiuchumi kwa kuwapa mikopo isiyo ya riba.

Vile vile, Serikali Kuu inaweza kutenga fedha zake kwa ajili ya mfuko wa kuyakopesha makundi hayo kupitia kwenye halmashauri, baada ya kuonekana kuwa halmashauri nyingi hazina uwezo wa kutekeleza jukumu hilo.

Ni matarajio yetu kuwa suala la kuwawezesha wanawake na makundi mengine litapatiwa ufumbuzi haraka kwa kuzingatia usemi kuwa 'ukimwezesha mwanamke unakuwa umeliwezesha Taifa'.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




### Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Tukijitolea inawezekana kupata walimu wa sayansi

**MOJA** ya changamoto inayozikabili sekondari za umma ni uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi na Hisabati, hali inayosababisha wanafunzi kutofundishwa masomo hayo kwenye baadhi ya shule.

Hata hivyo, serikali imeshaweka wazi kwamba ina kipaumbele wenye ajira za walimu wa masomo hayo kwa kufuata utaratibu wa kutuma vyeti vyao kabla ya kupangiwa kituo cha kazi.

Ni maelekezo ya Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Profesa Joyce Ndalichako, katika moja ya mikutano yake na Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (Tahossa).

Lakini, wakati serikali ikifanya jitihada hizo za kuajiri walimu wa kutosha, kuna haja wazazi wanaowatafuta walimu wa kujitolea wa masomo hayo, wanaosubiri ajira, ili wanafunzi wasiendelee kukosa masomo hayo.

Njia hiyo inaweza kuwasaidia wanafunzi kumudu masomo hayo kuliko kuendelea kusubiri hadi waajiriwe, wakati wapo mitaani bila kazi.

Hilo ni jambo ambalo wazazi na walezi wanaweza kuangalia na kuwa na uwezekano wa kuchangishana chochote kwa ajili ya posho za walimu hao.

Wale ambao wameona umuhimu, tayari wameshaanza kuutumia kwa kuchangishana fedha za posho na kupata walimu wa masomo hayo na sasa wanaendelea na kazi kufundisha watoto wao.

Mfano mmojawapo ni wazazi wa Sekondari za kata za Musoma Vijijini, mkoani Mara, ambao wamekubaliana kila mmoja kuchanga kati ya Sh. 200 hadi Sh. 1,000 kwa ajili ya walimu wa kufundisha watoto wao.

Hatua hii ni nzuri kutokana na ukweli kwamba kwa kawaida mtihani unapoandaliwa huwa ni wa masomo yote hata yale ambayo wanafunzi hawakuyasoma kutokana na uhaba wa walimu.

Kwa maana hiyo hatua iliyochukuliwa na wazazi hao ya kukaa na kuamua kwamba wapate walimu wa kujitolea kwa ajili ya kufundisha watoto wao masomo ya sayansi na Hisabati ni mfano mzuri wa kuigwa.

Walezi na wazazi hao wametimiza wajibu wao badala ya kuendelea kusubiri walimu waajiriwe wakati watoto wao wakikosa masomo hayo, huku wakiwa na uwezo wa kukabili changamoto hiyo.

Walimu hao wa kujitolea wanaweza kuwa na mchango mkubwa katika kufikia uchumi wa viwanda 2025, kwani watakuwa wamesaidia kuandaa wataalamu wa baadaye wakiwao wahandisi wa mitambo.

Hivyo wakati Tanzania ikiwa na walimu wachache wa masomo hayo, wazazi na walezi hawana budi kujiongeza na kuchukua hatua kama za wenzao wa Musoma Vijijini walioamua kuchukua hatua hizo.

Serikali imeshaeleza mipango yake hivyo kumaliza tatizo la upungufu wa walimu wa sayansi na Hisabati nchini, lakini wakati ikiwa kwenye mkakati huo, ni muhimu jamii kuwa njia mbadala kama hiyo ya kupata walimu wa kujitolea.

Jambo hili linatakiwa kupata baraka za viongozi wa maeneo yenye shule hizo hasa wale ambao ni wabunifu, kuanzia wa serikali za mitaa, madiwani na wabunge na kuhamasisha wananchi ili watambue umuhimu wake.

Mchango wao ni wa muhimu kwa kutambua kuwa nchi imedhamiria kuingia kwenye uchumi wa kati, ambao ni wa viwanda, hivyo umuhimu wa masomo hayo hauwezi kuepukwa, kwa sababu wataalamu zaidi wanahitajika.

Waliotambua umuhimu wote wameanza kwa kutafuta walimu wa kujitolea, ambao hadi sasa wanaendelea na kazi, kwani sasa ni wakati wa kuwa na wataalamu wengi wa fani za sayansi.

Hao ndiyo watakaoweza kutosheleza mahitaji ya sekta ya viwanda nchini, kwa hiyo hatua hiyo itamlazimisha mwanafunzi kusoma kwa bidii, ili kuhakikisha anafaulu masomo hayo ingawa tatizo lililopo ni uhaba wa walimu.

Wanafunzi kuendelelea kukosa masomo hayo kunaweza kuwafanya wayaone ni magumu na kukimbilia mengine, na kumbe kama wangefundishwa kikamilifu wangeweza kuyamudu.

Kwa maana hiyo umuhimu wa kuwa na walimu wa kujitolea upo palepale, kwamba wazazi na walezi wanatakiwa kujiongeza na kuweka mkakati wa kupata walimu wa kujitolea kwa ajili ya kuwafundisha na kuwaendeleza watoto wao.

## MJADALA/ TANGAZO




# Wadudu hawa ni kero kila mahali

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya msimu wa mahindi na mazao mengine kuanzia tatizo linalojitokeza kwa kasi ni wadudu waharibifu.

Tukianza na tatizo la kushambulia mahindi, visumbufu hivyo hushambulia na kutafuna majani ya mahindi tangu yakiwa mafupi na kusababisha kudumaa.

Wadudu hao jamii ya funza hawaishii hapo bali pia wanaharibu mtama na nafaka nyingine shambani na kwenye bustani.

Hali hiyo inaanza kuwakatisha tamaa wakulima kutokana na kasi ya kuzaliana kwa visimbufu hivyo ambavyo haviishi kwenye mahindi bali hushambulia mboga na matunda pia.

Aidha, hali ilivyo sasa kuna uhitaji wa haraka wa kuongeza upatikanaji wa dawa za kuua wadudu hao waharibifu wa mimea ambao licha ya kutibu mimea sehemu nyingine huzuka tena na kuongeza hofu kuwa huenda nao wamekuwa sugu kwa dawa.

Yote hayo huongeza gharama kwa wakulima na kusababisha usumbufu kwa vile visimbufu hivyo vimeenea sehemu nyingi na wakulima wanashindwa kuwadhibiti.

Wadudu hao ni waharibifu kiasi kwamba majani ya mahindi machanga hutobolewa na mengine shina zima huoza.

Wadudu wanaoshambuliwa mahindi wanapatikana karibu nchi nzima na iwapo hawatadhibitiwa wataendelea kusababisha hasara ya mabilioni ya dola na Shilingi si kwa mkulima pekee bali hata taifa ambalo akiba ya chakula itakuwa shakani.

Pamoja na kwamba kuna dawa za kudhibiti ukweli ni kwamba hazikingi vya kutosha kwani hata baada ya kunyunyuzia dawa, baadhi ya wadudu hurudi kushambulia mahindi.

Pamoja na kuumiza mahindi na mtama unaopandwa maeneo ya ukanda wa pwani, wadudu wengine jamii ya 'utitiri' mweupe na mweusi hushambulia mapapai, mapera na matopetope pamoja na mastafeli kwenye bustani za wakulima wengi.

Ni vigumu kupata mpapai ambao haushambuliwa na wadudu. Aidha, matunda kama mapera yanashambuliwa na huenda yasistawi tena kutokana na athari zinazotokana na wadudu hao.

Kwa miaka mingi wakazi wa Dar es Salaam watakubaliana name kuwa wanashindwa kuvuna mchicha kwenye bustani zao kutokana na wadudu hao jamii ya funza wadogo wanaokula mboga za majani.

Kwa upande mwingine inakuwa vigumu kujua namna ya kupambana na maradhi hayo kwa sababu hakuna maofisa ugani hasa sehemu za mijini wa kuwasaidia wakulima kufahamu namna ya kutibu mimea yao.

Kukosekana kwa maofisa ugani kunasababisha wakulima kutumia kemikali kienyeji ambazo huenda ni hatari kwa afya zao.

Wadudu weupe wanaumiza mihogo na kusababisha wakulima kushindwa kula kisamvu kwani nacho kimejaa wadudu weupe na weusi wanasababisha majani kujikuchа na kusinyaa.

Kuongezeka kwa wadudu wanaoshambulia mahindi, matunda, mboga na majani ya mihogo kunaongeza ugumu wa maisha kwa kuwa hata wakulima wanaojituma kuzalisha mboga kwenye bustani za nyumbani wanashindwa kufanya hivyo.

Kutokana na ukubwa wa tatizo ni wakati wa Wizara ya Kilimo, wajasiriamali na wadau wa viuatilifu kusaidia kupatikana dawa hasa za asili ili kudhibiti magonjwa yanayotokana na wadudu hao.

Wataalamu hao wasaidie kupata dawa au viuatilifu vya asili kama vile matumizi ya majani ya mwarobaini na sababu za unga au maji kuzalisha tiba za kuangamiza visumbufu hivyo.

Tunapendekeza hivyo ili kuepusha uwezekano wa kutumia sumu kali kutiba mchicha au mapapai ili kuepusha walaji na athari za kula kemikali kupindukia jambo ambalo ni hatari kwa maisha yao.

Kwa vile msimu wa kilimo umeanza ni vyema pia wataalamu wa kilimo kutembelea wakulima wa mijini na hata ikibidi kuandaa mikutano ikiwezekana kwenye ofisi za serikali za mitaa au hata kuwafikia nyumbani kuwaelimisha kuhusu namna ya kukabiliana na wadudu.

Hata hivyo, wakulima wanaosikiliza redio na kutizama televisheni wangependa pia kusikia taarifa za kitaalamu kuhusu namna ya kukabiliana na wadudu waharibifu hasa wale wanaoshambulia mahindi, mboga na matunda sehemu mbalimbali bila kujali ni vijijini na mijini.

Ni vyema wataalamu wakatuma taarifa za kitaalamu na za kutumia njia za asili ili kudhibiti wadudu visumbufu kwenye makundi mbalimbali ya mitandao ya kijamii ili watu wasome na kudhibiti uharibifu.


the Jane Goodall Institute

## JOB OPPORTUNITY

### Finance & Administrative Manager
***Kigoma, Tanzania***

**Organization Overview:**
Founded in 1977, the Jane Goodall Institute (JGI) USA is an international non-governmental organization that continues Dr. Goodall's pioneering work on chimpanzee ecology and behavior. Its mission is to promote wildlife conservation, in particular chimpanzee sustainability, through research, education, and community conservation. The breadth of JGI's mission reflects Dr. Goodall's personal philosophy that the survival of all species, whether chimpanzee or human, depends upon the collaboration of all people. In 2012, JGI formally adopted an ambitious 30-year goal to protect 85% of Africa's wild chimpanzee populations in their natural habitats. In reaching this goal, JGI will capitalize on its considerable strengths and experience gained from working throughout the chimpanzee range, which includes more than 50 years of chimpanzee behavioral research at the Gombe Stream Research Center; its 20 years of developing people- and community-centered conservation strategies; its impressive expertise in the use geospatial technology to innovatively map and monitor human and chimpanzee use of forest resources; and its global environmental and humanitarian youth program – Roots & Shoots.

Under its Department of Africa Programs (AP), JGI USA implements community-based conservation activities in the Democratic Republic of Congo, Republic of Congo, Tanzania, and Uganda. Our Africa Programs partners include but are not limited to the United States Agency for International Development (USAID), Disney Foundation, Arcus Family Foundation, Allen Family Foundation, US Fish and Wildlife Services (USFWS), the Turner Foundation, and a strong individual donor base.

The USAID-funded Landscape Conservation in Western Tanzania Project strengthens landscape scale conservation in the western geographical landscape of Tanzania through the development of a strategic landscape approach built upon USAID's previous and continued support to NRM and conservation in Western Tanzania. This is a five-year funded cooperative agreement under USAID.

JGI is searching for a Finance & Administrative (FAM) Manager to join a dynamic team of professionals responsible for the implementation of the program and the responsible stewardship of resources. Reporting directly to the Chief of Party (COP) based in Kigoma, the FAM will be responsible for overseeing the administrative and financial management, accountability requirements and human resources management for this project, ensuring accurate and timely financial and administrative support services are providing to the program team. S/he has overall supervisory responsibility for the finance team and the administration team, focusing on general ledger activity, daily posting process, payroll, accounts receivable and accounts payable, month-end closing process and financial report preparation.

Work involves the ability to manage a queue of priorities; responsibility for making independent decisions based upon knowledge of organization operations, policies and procedures; and assigning and reviewing the work of support staff. Providing technical assistance to staff in implementing and complying with financial and administrative procedures to ensure compliance with regulations and serve as the financial liaison to JGI, local NGOs, other implementing partners and implementing units.

JGI is currently seeking to recruit suitably qualified and competent Tanzanian to fill the position of Finance & Administrative Manager with the following job functions and qualifications below:

**Essential Functions:**
- Coordinate, including being able to perform, activities across the various accounting functions: payroll, accounts payable, accounts receivable and general accounting.
- Manage weekly accounts payable process under the direction of program leadership. Support Staff Accountant in payroll, monthly billing and daily accounts receivable processes.
- Prepare and/or coordinate monthly reconciliation of general ledger accounts. Work with HQ accounting to report timely and accurate financial data.
- Facilitate "closing" of financial records on a monthly basis and in a timely manner.
- Support the leadership for the external annual audit process.
- Work closely with the Tanzania and HQ program and financial support teams.
- Review expenses to ensure that they have been recorded consistently and in accordance with JGI policies and procedures, generally accepted accounting procedures and USAID requirements.
- Ensure the collection of accurate and complete documentation to support accounting entries in accordance with established JGI policies and procedures and USAID requirements.
- Work closely with accounting staff to review accounting process and procedures, analyze and reconcile accounts and recommend controls to prevent errors and promote efficiency.
- Coordinate with the Grants Manager to assess the capacity of grant applicants and review request for advances, liquidations and support documentation.
- Provide high quality and proactive technical support to the program team including the review and interpreting financial results and making corrections in the G/L as identified.
- Ensures proper cash handling procedures; responsible for proper control of petty cash.
- Performs related duties as required

**Minimum Qualifications:**
- o A minimum of a Bachelor's degree (preferably a Master's degree) in Business Administration or Finance.
- o At least five years of experience managing the financial and administrative aspects of donor-funded assistance programs of similar size, complexity and setting.
- o Demonstrated experience in managing and supervising a team.
- o Demonstrated experience in managing sub-grants including conducting risk assessments
- o Ability to communicate effectively in English, both verbally and in writing.
- o Broad understanding of national laws, policies and norms related to accounting and administration.
- o Demonstrated experience in budgeting, human resources, procurement and compliance issues.

**Application Procedure:**
All applications should be submitted together with the signed application letter, most recent curriculum vitae (resume), copy of relevant certificates & transcripts, testimonials, active mobile phone number & e-mail address, and should be sent to the following e-mail address: **jgi-tanzania@janegoodall.or.tz** with a subject "Application for Finance & Administrative Manager".

***Only the shortlisted candidates will be contacted for the interview.***

***Deadline: Five (5) days from the first date of advertisement.***

JGI Tanzania is an equal opportunity employer and considers all applicants on the basis of merit without regard to race, national or tribal origin, religious belief, sexual orientation, and marital status.

***QUALIFIED WOMEN ARE HIGHLY ENCOURAGED TO APPLY.***

215662302

# Walipwa bil. 5.8 /- kupisha umeme

**Restuta Damian, BIHARAMULO**

WAKAZI 992 kati ya 1,254 wa Kata Nyakanazi wilayani Biharamulo mkoani Kagera, wamelipwa fidia ya Sh. bilioni 5.8 za maeneo ya ardhi zao yaliyochukuliwa na serikali kwa ajili ya kujenga kituo cha kusambaza na kupoza umeme.

Umeme huo utatoka kwenye mradi wa Rusumo Regional Hydroelectric Falls Project (RRHFP) unaoendelea kujengwa katika maporomoko ya Mto Kagera yanayopita wilaya Ngara mkoani Kagera.

Hayo yalibainishwa Meneja mradi wa Nyakanazi-Geita, Elias Mokunga, wakati akieleza hatua za awali kwenye mradi wa kv 220 zenye urefu km144 utakaonufaisha mikoa ya Tanzania kwani, ambacho ndicho kituo kikuu cha kupozea umeme kutoka Rusumo wilayani Ngara ambako mradi mkubwa unajengwa kwa ajili ya nchi tatu.

Mokunga alisema fidia hiyo inaendelea kulipa wananchi 262 waliobaki, na kwamba wapo katika hatua nzuri za malipo na maeneo yanayopewa kipaumbele ni mashamba, ardhi na makazi.

Alisema gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 93, na kuwa Tanzania na Umoja wa Ulaya (EU zimetoa shilingi bilioni 5.8 zilizotumika kulipa fidia wananchi na kiasi kingine kinatolewa na washirika wa maendeleo ambao ni Ujerumani, EU na Ufaransa.

Alisema kiasi kunachotakiwa ni zaidi ya shilingi bilioni 100 ambazo zitagawanywa katika shughuli mbalimbali ikiwamo ugawaji wa umeme bure kwenye vijiji 21 na kiasi kinachotakiwa kwenye ugawaji huo ni Euro milioni 7.9 kutoka EU.

"Benki ya ujerumani ilitoa Euro milioni 20, Benki ya Maendeleo ya Ufaransa Euro milioni 14 na Euro milioni 7.9," alisema Mokinga.

Alisema baada ya mradi kukamilika wateja 5,674 wa awali, watachangia gharama za kusogeza ngazi, lengo ni kufikia wateja 10,000, na kwamba kuna baadhi ya vijiji vinaendelea kufanyiwa utafiti.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), Mwajuma Hamza (kushoto), akitoa maelezo kwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, jinsi chama hicho, kilivyoweza kuwanufaisha wanawake wengi nchini, wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake kitaifa, mkoani Simiyu juzi. **PICHA: HAPPY SEVERIVE**

# 'Zungumzeni na watoto wakiwa bado tumboni'

**Na Mwandishi Wetu**

JAMII imeshauriwa kuzungumza na watoto wao kuanzia wakiwa tumboni ili kukuza ubongo wao wakiwa bado wadogo.

Akizungumza katika mkutano wa siku mbili wa kujadili ukuaji na maendeleo ya watoto wakiwa katika hatua za awali, Mtafiti kutoka Taasisi ya Ubongo Learning, Aneth Ngongi, alisema mtoto anaanza kujifunza mambo mengi tangu akiwa tumboni.

"Mtoto angali tumboni ana uwezo wa kujifunza mambo mengi yaliyopo duniani kupitia kusikia na hisia hivyo ni vyema kwa wazazi kuanza kuongea na kucheza naye katika kipindi hicho," alisema Aneth.

Alisema ndiyo maana taasisi hiyo imekuja na mfumo wa kidijitali wa kujifunzia elimu kwa watoto ambao utawasaidia kujifunza kupitia katuni na kucheza.

Alisema ni vyema wazazi kuanza kuweka mazingira bora ya kujifunzia kwa watoto wawapo wadogo kwa kuchagua maudhui ya kuelimisha.

"Ubongo Learning tuna nafasi kubwa ya kuzifikia familia nyingi barani afrika kupitia simu na kutoa ujumbe wa kuelimisha na kubadilisha maisha yao hivyo ni kujumu la wazazi kupokea maudhui yetu," alisema Aneth.

Alisema taasisi hiyo imekuwa na vipindi vya luninga vyenye mafunzo mbalimbali kwa watoto kulingana na umri wao.

Alisema kipindi cha 'Akili and me' kinalenga kutoa elimu kwa watoto wenye umri kati ya miaka mitatu hadi saba kikijikita katika kufundisha namba, alfabeti, hisia na afya ambavyo vitamsaidia mtoto kukua akiwa na uelewa.

Alisema kipindi cha pili ni Ubongo Kids ambacho kinawalenga watoto wenye umri wa miaka saba hadi 13 ili waweze kujua mapema masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hesabu (STEM) na kujifunza kwa hisia za jamii (Social emotional learning).

Alisema Ubongo Learning imekuwa ikifanya kazi katika nchi 13 barani Afrika kwa kutumia lugha tofauti kulingana na nchi husika.

Aliongeza kuwa kwa kutumia mada mbalimbali za shuleni wamewakijengea uwezo wanafunzi katika maeneo ambayo mitaala haitosherezi.

Naye Mkuu wa kitengo cha Uzalishaji cha Ubongo Learning, Amani Mkamba, alisema wanafanya tafiti shuleni kwa kupitia mtaala na kuangalia palipo na upungufu ndipo wanaanza kuandaa vipindi hivyo.

Alisema kupitia taasisi zinazotoa takwimu zimewapa mrejesho kuwa wamefanikiwa kuwafikia watu milioni 16.9 wanaoangalia vipindi kupitia luninga na luninga ya mtandaoni (youtube).

Mkutano huo ulioongozwa na ujumbe usemao 'Kujenga Ubongo' umefanyika Machi 6 na 7 mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Mfumo huo wa kufundishia una uwezo wa kuinua na kubadilisha fikra na tabia kwa wasimamizi na wadau ili kufikia lengo mahsusi la kutoa elimu ya awali kwa kupitia vichocheo na michezo nyumbani na katika jamii.

Mada ya 'Kujenga Ubongo' imewavutia wadau mbalimbali katika kujadili maendeleo ya watoto walio katika hatua ya awali

# Ataka watumishi Osha wanolewe

**Na Gwamaka Alipipi**

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Antony Mavunde, ameitaka Menejimenti ya Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (Osha), kuendelea kujenga uwezo wa watumishi wake mara kwa mara ili waendane na mabadiliko ya teknolojia.

Amesema kuna haja wakala huo kuwekeza zaidi katika kuwaelimisha wananchi kuhusu masuala ya afya na usalama kazini kwa kuwa wengi wao bado hawana ufahamu wa kutosha wa masuala hayo muhimu.

Alitoa agizo hilo jana wakati akifungua kikao cha sita cha baraza la tatu la wafanyakazi wa Osha na mafunzo ya kujiandaa kustaafu, kujikinga na magonjwa yanayoambukiza kama vile Ukimwi na virusi vya corona.

"Kuna mabadiliko mengi yanayotokea hususani katika teknolojia, hivyo ili kuendana na kasi ya mabadiliko hayo, hatuna budi kuwaendeleza wataalamu wetu kiujuzi mara kwa mara. Hii itawawezesha kutekeleza majukumu yao kwa weledi na hatimaye kuleta tija katika uzalishaji.

"Mchango wa taasisi ya Osha katika kufanikisha sera ya nchi yetu ya uchumi wa viwanda ni mkubwa mno, kwani viwanda vinaambatana na vihatarishi mbalimbali vya kiusalama na afya, hivyo kuendelea kujenga uwezo wa wakaguzi wetu wa usalama na afya mahali pa kazi ni jambo la msingi sana," alisema.

Aliipongeza Osha kwa kazi nzuri inayofanyika katika ukaguzi wa usalama na afya kwenye maeneo ya kazi nchini, kutoa huduma bora zinazowaridhisha wateja na hivyo kuondoa malalamiko ambayo yalikuwa yakijitokeza miaka ya nyuma.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa Osha, Khadija Mwenda, alisema miongoni mwa agenda za kikao hicho ni kujadili rasimu ya mpango mkakati wa taasisi wa miaka mitano ijayo (2020/2021-2024/2025) ambao baadhi ya malengo yake ni kusajili maeneo mengi zaidi ya kazi na kuhakikisha yanakidhi viwango vya usalama na afya mahali pa kazi.

"Tukiwa tunamalizia kutekeleza mpango mkakati unaoishia mwaka huu wa fedha, tuliona ni muhimu kufanya tathmini ili kubaini matatizo au ombwe lililokuwapo katika mpango huo ambapo tathmini hiyo ndiyo imetuwezesha kuja na mpango mkakati mpya unaotatua matatizo yaliyobainika," alisema.

## Wachangishana ujenzi kituo polisi

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAKAZI wa Kata ya Ulowa Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamechangishana fedha na kujenga kituo cha polisi ili kukabiliana na wimbi la uvamizi nyakati za usiku kwenye makazi na maduka yao.

Uvamizi na uporaji huo umekuwa ukifanyika wakati wa mavuno.

Hayo yalibainishwa wakati Naibu Waziri wa Ujenzi ambaye ni Mbunge wa Ushetu, Elias Kwandikwa, akikabidhi mabati bando nne kwa ajili ya uwezekaji wa kituo hicho ambacho kimejengwa kwa nguvu za wananchi, vyama vya msingi (Amcos) na wadau wa maendeleo.

Aloyce Jacobo, mkazi wa Kata ya Ulowa, alisema, wamechukua hatua ya kuchangishana na kujenga kituo cha polisi baada ya kukithiri kwa uvamizi nyakati za usiku kwenye makazi na maduka ya biashara, na kwamba matukio hayo yote yanatokea wakati wa mavuno ya kilimo cha tumbaku na pamba.

"Uvamizi huu ulianza kata za jirani za Mbika, Ubagwe Kijiji cha Nongwe baadaye wakafika hapa kwetu Ulowa, na... uvamizi huo hufanyika nyakati za usiku hasa wakati wa mavuno ya mpunga, tumbaku na pamba," alisema.

Diwani wa Viti Maalum, Gabriela Kimaro, alisema kujengwa kwa kituo cha polisi kunatokana na kuandamwa na matukio mbalimbali ya wizi kwenye maduka, mifugo na uvamizi barabarani.

Aidha, Kimaro alisema wananchi waliingiwa na hofu na kuchukua hatua ya kuomba askari watano kutoka Kituo cha Polisi Nyamilangano.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Kwandikwa, alisema serikali imejipanga kuweka mazingira mazuri ya ulinzi halmashauri nzima ya Ushetu ili wananchi waweze kufanya shughuli za uzalishaji mali kwa amani na utulivu.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, aliwapongeza wananchi wa Kata ya Ulowa kwa kujenga kituo cha afya kwa ajili ya kupambana na uhalifu na kuwataka wakazi wa kata za jirani kuiga mfano wa kata hiyo.

# Wanaokiuka matumizi vyandarua kukamatwa

**Na Tiganya Vincent, TABORA**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, amewaagiza viongozi wa vijiji na mitaa kuwakamata watu wote watakaokutwa wakitumia vyandarua kwa matumizi mengine mbali na kujikinga na mbu.

Alisema matumizi ya vyandarua nje ya kujikinga na mbu yanapingana na juhudi za serikali za kupambana na malaria na kusababisha kupoteza nguvu kazi ya Taifa.

Mwanri alitoa agizo hilo wilayani Kaliua wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Mkoa wa Tabora ziro malaria inaanza na mimi.

Alisema kuwa baadhi ya watu wanatumia vyandarua kuvulia samaki katika madimbwi na wengine wanatumia kuzungushia vifaranga vya kuku visisumbuliwe na mwewe.

Mwanri aliongeza kuwa kuna watu wengine wanatumia vyandarua hivyo kwa ajili ya kuzungushia bustani za matunda na mboga ili kuzuia wadudu waharibifu.

Alisema matumizi hayo ambayo ni kinyume cha kujikinga na mbu ni marufuku mkoani na atakayekutwa atachukuliwa hatua.

Awali Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Honoratha Rutatatinisibwa, alisema mwelekeo wa serikali ni kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2030 ugonjwa wa malaria uwe umetokomezwa.

Alisema takwimu zinaonyesha kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa malaria kwa Mkoa wa Tabora bado ni tatizo ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ina asilimia 16.7, kufuatia Uyui asilimia 16.1 na Sikonge ambayo ina asilimia 13.9.

Dk. Rutatatinisibwa alisema Urambo ina asilimia 12.8, Manispaa ya Tabora asilimia 8.9, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega asimilia 8.7, Nzega Mji asilimia 6.8 na Igunga asilimia 5.6.

Alisema nguvu zaidi zinahitajika katika kupambana na tatizo la malaria mkoani Tabora.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Elias Kwandikwa (wa tatu kulia), akikabidhi mabati 48 kwa ajili ya kuezekea Kituo cha Polisi cha Kata ya Ulowa, kilichojengwa kwa nguvu za wananchi, vyama vya msingi (Amcos) na wadau wa maendeleo, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Kilimo cha mkonge chapigwa jeki matrekta ya bil. 1/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amevutiwa na juhudi kubwa iliyofanywa na Benki ya NMB katika kilimo cha katani mkoani Tanga, baada ya benki hiyo kutoa matrekta 11 yenye thamani ya Sh. bilioni 1.

Akizungumza baada ya kukabidhi matrekta hayo, Majaliwa alisema wakulima wa mkonge hawanabudi kutumia vema fursa ya uwapo wa NMB ambapo aliwahimiza kuyatumia vema kwa manufaa ya wote na kuongeza tija kwenye kilimo cha mkonge.

Waziri Mkuu alipokea matrekta hayo katika hafla iliyofanyika nje ya kiwanda cha kuchakata singa cha Mwelya wilayani Korogwe, mkoani Tanga ikiwa ni sehemu ya ziara ya kikazi mkoani humo.

"NMB ni benki yenye watu wabunifu, nimeshuhudia hata kwenye mazao mengine ya kimkakati kama pamba na korosho; wakiwakopesha wakulima na mimi mwenyewe hukabidhi matrekta hayo, hivyo wakulima mnatakiwa kuchangamkia benki hii yenye matawi nchi nzima," alisema Majaliwa.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela, alisema mkoa wake utahakikisha matrekta hayo yanatumika kama yalivyokusudiwa na kwamba kama atatokea mkulima au mfanyakazi yeyote kutaka kuyahujumu sheria zitachukua mkondo wake.

"Matrekta haya ni ukombozi mkubwa kwa wakulima wa Mkoa wa Tanga, kwa sababu huko nyuma walikuwa wakinyonywa na Katani Limited kiasi cha kutokopesheka kabisa, lakini hivi sasa serikali imefanyia maboresho ili waweze kufaidika na zao hili muhimu kwa uchumi wa taifa," alisema Shigela.

Ofisa Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi na Biashara Benki ya NMB, Filbert Mponzi, alisema benki hiyo inatambua kilimo ni moja ya kipaumbele cha Taifa kwa kuwa takwimu zinaonyesha Watanzania zaidi ya asilimia 80 wanaoishi vijijini na mijini wanategemea kilimo.

Kwa kulitambua hili, NMB imefungua akaunti za wakulima zaidi ya 800 katika vyama vitano vya ushirika vya msingi vinavyoendesha mashamba ya mkonge ya Ngombezi, Magunga, Mwelya, Hale na Magoma mkoani humo.

"NMB imetoa mikopo ya jumla ya Sh. bilioni 1.024 kwa vyama vinne vya ushirika vya msingi vya Ngombezi, Magunga, Mwelya na Magoma kwa ajili ya ununuzi wa matrekta 11 na matrekta 22, ili kuwezesha usafirishaji wa mkonge kutoka kwenye mashamba ya wakulima kwenda kwenye viwanda vya uchakataji wa mkonge," alisema Mponzi.

Mwenyekiti wa vyama vya msingi vya ushirika wa wakulima wadogo wa mkonge (Amcos) wilayani Korogwe, Greyson Nyari alisema: "Tunaishukuru Benki ya NMB kutukabidhi matrekta haya ikiwa ni mkopo nafuu, yatatusaidia kuendesha shughuli za kuhudumia mashamba, kutachonga barabara za kuingia mashambani na kusombea majani ya mkonge kwa ajili ya kupeleka kwenye korona tayari kuchakatwa na kuwa singa."

# Umeme changamoto kubwa Ukerewe

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

WILAYA ya Ukerewe mkoani Mwanza inakabiliwa na changamoto ya nishati ya umeme kutokana na kukatika mara kwa mara.

Imeelezwa kuwa wakati mwingine wakazi wa wilaya hiyo wanakosa nishati hiyo kwa siku mbili hadi tatu.

Hayo yalibainishwa na Mbunge wa Jimbo la Ukerewe, Joseph Mkundi, wakati wa Kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Mwanza kilichofanyika jijini hapa.

Alisema katika wilaya hiyo, umeme hukatika kwa wiki nzima, tatizo ambalo limedumu muda mrefu, hivyo Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) wilaya wameshindwa kupata ufumbuzi na hoja yao mara nyingi ni kuanguka kwa nguzo na kebo (cable) inayopita ndani ya ziwa zinazovusha umeme kutoka Kisorya hadi Ukerewe kuingiliwa.

"Ni tatizo ambalo limekuwa likituathiri sana kiuchumi na shughuli nyingine za kibinadamu, nitoe tu wito serikali kupitia Wizara ya Nishati tupate suluhu ya kudumu angalau wananchi wa Ukerewe waweze kufaidika na nishati hii ya umeme kwa ajili ya shughuli zao mbalimbali za kimaendeleo," alisema Mkundi.

Alisema mbali na kukatika kwa umeme, pia kwenye visiwa ambavyo vinatumia nishati ya umeme wa jua mfano kisiwa cha Ukara bado wanaendelea na mjadala kuona kwa namna gani bei ya umeme itashuka, kwa sababu hivi sasa kupitia kampuni ya Jumeme mwananchi analipa Sh. 2,500 kwa uniti moja.

Meneja wa Tanesco Mkoa wa Mwanza, Henryfried Byabato, alisema changamoto iliyopo Ukerewe ni kutokana na kebo iliyopita chini ya maji kutobolewa na wavuvi ambayo inatoa umeme Kisorya hadi Kisorya.

"Kukatika kwa umeme maeneo ya Ukerewe na Sengerema hasa Ukerewe tunachangamoto ya kebo inayopita ndani ya maji iliathiriwa na wavuvi kwa sababu haijapita chini sana, lakini mpango uliopo tutaweka nguzo za chuma ambazo zitaenda umbali wa mita 400," alisema na kuongeza:

"Tutavuta waya wa juu kwa hiyo nategemea changamoto hiyo itatatuliwa. Pia tumeenda mbele zaidi kuwa maeneo yenye maji hasa kwenye majaruba tuta weka nguzo za zege na ipo kwenye mpango wetu tayari na tutalitekeleza."

## Vikundi kinamama vyakopeshwa 68%

**Shaban Njia na Neema Sawaka, KAHAMA**

HALMASHAURI ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, imetoa mikopo yenye riba nafuu kwa vikundi vya kinamama kwa zaidi ya asilimia 68 ili kuwawezesha na kuwainua kiuchumi na kuwafanya kuachana na utegemezi.

Hayo yalimebainika juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, yaliyofanyika katika Kijiji cha Bugela Kata ya Ulowa wakati Ofisa Maendeleo ya Jamii (dawati la uwezeshaji wananchi kiuchumi) Minaeli John Ngomoi, alipokuwa akitoa taarifa ya utoaji wa mikopo.

Alisema Halmashauri ya Ushetu imefanikiwa kutoa mikopo kwa vikundi hivyo, vijana na watu wenye ulemavu kwa zaidi ya asilimia 68 na kwamba mwaka 2015 hadi 2019/20 halmashauri imeshatoa zaidi ya Sh. milioni 301.1

Aidha, alisema mwaka wa fedha 2015/16 halmashauri ilitoa mikopo kwenye vikundi saba vya kinamama vikiwa na wanachama 35 wenye thamani ya Sh. milioni nane, huku mwaka 2016/17 vikundi 21 na wanachama 105 vilipata shilingi milioni 51.

Pia alisema kuwa, mwaka wa fedha 2018/19 halmashauri ilitoa mikopo kwenye vikundi 16 vyenye wanachama 80 vilivyopata Sh. milioni 75.1, huku mwaka 2019/2020 vikundi vya kinamama 35 vyenye wanachama 175 vikipata Sh. milioni 176.

Naye Diwani wa Viti Maalumu Kata ya Ulowa, Gabriela Kimaro, alipongeza halmashauri kwa kutenga fedha kwenye mapato ya ndani kila baada ya robo ya makusanyo katika kuviwezesha vikundi vya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu.

Akizungumza baada ya kupokea taarifa hiyo, Naibu Waziri wa Ujenzi ambaye ni Mbunge wa Ushetu, Elias Kwandikwa, alimpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kwa kutoa kipaumbele kwenye kuviwezesha kiuchumi vikundi vya kinamama ambavyo vilikuwa vimesahaulika awali.

Kwandikwa alisema mikopo hiyo itawasaidia wanawake hao kuwainua kiuchumi na kuwawezesha kumiliki biashara na rasilimali nyingine kama ilivyo kwenye vikundi vya wanaume.



Gavana wa Klabu ya Rotary (DIST. 9211) aliyemaliza muda wake, Sharmila Bhatt (wa pili kulia), akiwa katika picha ya kumbukumbu na wanawake wenye mafanikio (kutoka kulia) Dk. Zohraida Karim (Mzungumzaji Mwamasishaji), Aneth Yesaya (Katibu wa Jukwaa la Viziwi), Jennifer Shigoli (Mjasiriamali) na Catherine Shindika (Mwelimishaji), wakati wa hafla ya Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyoandaliwa na Klabu ya Rotary ya Pugu, jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Rais wa Klabu hiyo, Satyam Gupta (kulia) na Katibu, Hemaly Jethwa (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi Dar wawezeshwa taulo za kike

**Na Sabato Kasika**

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Msigani, Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, wamepata msaada wa taulo za kike kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Taulo hizo ambazo ni katoni tano, zilitolewa juzi na taasisi isiyo ya kiserikali ya Mpakani Tunaweza kama mchango wake kwa ajili ya wanafunzi wa shule hiyo.

Aliyekabidhi taulo hizo ni Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Asia Khalifa, na kusema, Mpakani Tunaweza imeona njia nzuri ya kuadhimisha siku hiyo ni kutoa msaada wa taulo za kike.

Katika hafla hiyo iliyofanyika Shule ya Msingi Msigani na kuhudhuriwa na wanafunzi, walimu, wazazi na viongozi wa serikali, alisema, taasisi inataka kuhamasisha jamii kuchangia upatikanaji wa taulo hizo kwa wanafunzi.

"Tunataka wanafunzi wa kike waendelee kubaki madarasani hata wanapokuwa kwenye hedhi, ndiyo maana Mpakani Tunaweza tumekuja na kaulimbiu ya ziada kwenye Siku ya Wanawake Duniani," alisema Asia.

Aliitaja kaulimbiu hiyo kuwa ni; 'Wape taulo za hedhi wabaki darasani', na kwamba na jukumu la jamii kuhakikisha wanafunzi wanapata taulo hizo kadri inavyowezekana ili wasipoteze muda wa masomo.

Akipokea taulo hizo kwa niaba ya wanafunzi, Ofisa Elimu Kata ya Msigani, Veronica Mallya, alisema kata yake ina shule za msingi tano alizozitaja kwa majina ya Temboni, Msigani, Kisiwani, Bwawani na Malamba Mawili.

"Katika shule hizo, kuna wanafunzi wa kike 9,320, ambao asilimia 10 hadi 20 hukosa masomo wanapokuwa kwenye hedhi kwa kukosa taulo za kike, kwa siku tatu hadi tano," alisema Mallya.

Alisema shughuli iliyofanywa na asasi ya Mpakani ni ya kuigwa katika Wilaya ya Ubungo ili kuwawezesha wanafunzi wa kike kubaki darasani, na kwamba kwa wastani wanafunzi wa kike hukosa masomo kwa siku tatu hadi tano kwa mwezi wakiwa kwenye hedhi.

Naye Diwani wa Kata ya Msigani, Agustino Mushi, alisema atawasilisha pendekezo kwenye vikao vya madiwani wa Manispaa ya Ubungo ili kuishawishi manispaa yake kutenga fedha miongoni mwa asilimia nane inayotengwa kwa ajili ya wanawake na vijana kwa ajili ya kununua taulo za kike kwa ajili ya shule zote za manispaa ya Ubungo kuanzia msimu wa fedha wa mwaka 2020/2021.

Baadhi ya wazazi waliohudhuria hafla hiyo walitaka taulo hizo zigawiwe kwa wazazi ili wawape watoto wao badala ya utaratibu uliopendekezwa wa kuwapa walimu ndiyo wazigawe kwa wanafunzi.

# Diwani aitaka halmashauri kuongeza walimu

Na Jaliwason Jasson, HANAN'G

DIWANI wa Viti Maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanan'g, mkoani Manyara, Regula Mtey, ameishauri halmashauri hiyo kuongeza idadi ya walimu wa awali, ili wawasaidie katika uumbaji wa herufi na kuwapa msingi mzuri wanafunzi hao.

Ushauri huo aliutoa juzi, alipokuwa kwenye Baraza la Madiwani, wakati akichangia hoja ya kuboresha elimu, katika eneo la halmashauri yao.

Mtey alisema, halmashauri hiyo imewasainisha walimu mkataba kufaulisha wanafunzi wa awali, ili ajue kusoma na kuandika.

"Kuna shida ya walimu kwa kuwa yapo baadhi ya madarasa yana wanafunzi 200, hali hii inakuwa ngumu kwa mwalimu mmoja, kumudu wanafunzi wote hawa, kama kuna uwezekano, tuwaongezee idadi ya walimu, hata kwa kuajiri walimu wa muda, ili wanafunzi wafaulu," alisema Mtey.

Alisema kuliacha tatizo hilo liendelee ni kuwapa shida walimu, kwa sababu wao ndio wanafundisha uumbaji wa herufi.

"Kama tunavyojua mtoto akitoka darasa la chini, akiwa vibaya anayepata ugumu ni mwalimu wa darasa linalofuata atakayempokea, hivyo lazima tujenge msingi vizuri," alifafanua.

Naye Mbunge wa Viti Maalum, Rose Kamili, aliiomba halmashauri kuwapa motisha walimu wanaoishi mazingira magumu, ili wawe na moyo wa kujituma kwa ajili ya kusaidia kuongezeka ufaulu.

Akiahirisha baraza hilo, Mwenyekiti wa Halmashauri, George Bajuta, aliwataka madiwani wote katika vikao vyao vya maendeleo ya kata, kuifanya ajenda ya elimu ya kudumu na kuwashauri kubuni mbinu za kusaidia kuongeza ufaulu katika maeneo yao.

Mkazi wa Katesh, Thomas Simon, akizungumza na Nipashe alisema, serikali kama haitawekeza kwa watoto wa awali, itafanya kazi bure katika elimu.

# Wamshukuru RC kuwarudishia ardhi

Na Cynthia Mwilolezi, MANYARA

WAKAZI wa Kijiji cha Landanai, Kata ya Naberera wilayani Simanjiro, wamemshukuru Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti kwa kuwapatia ekari 1,000 za ardhi zilizoporwa na kigogo mmoja wa wilaya hiyo.

Wakazi hao walisema uamuzi huo wa Mkuu wa Mkoa kuwarudishia ardhi yao iliyoporwa ni ushindi kwao.

Mmoja kati ya wakazi hao, Julius Ezekiel alisema, ardhi yao ilichukuliwa na mafisadi wa ardhi na wao wakalalamikia jambo hilo kwa Mnyeti ambaye ameagiza warejeshewe.

Alisema kigogo mmoja wa wilaya hiyo aliwapora ekari hizo 1,000 za ardhi na wao wakakosa sehemu ya kuchungia mifugo na kilimo kutokana na tamaa ya mtu mmoja.

Diwani wa Kata ya Naberera, Haiyo Mamasita, alimshukuru Mkuu wa Mkoa kwa hatua hiyo kubwa ya kurudisha ardhi kwa wananchi wake.

"Huyo kigogo alitumia nafasi yake ya udiwani na kujimegea ardhi hiyo ekari 1,000 bila halali na sisi tulipodai alitumia nafasi yake kung'ang'ania eneo hilo," alisema Mamasita.

Alisema Rais John Magufuli hakukosea kumteua Mnyeti kuongoza mkoa wao kwa kuwa amekuwa akiwatetea wanyonge.

Mnyeti alisema, alifanya ziara ya kuzungumza na wananchi hao mwishoni mwa mwaka jana na wakamweleza tatizo hilo.

"Baada ya kupata malalamiko haya niliunda kamati ya kufuatilia suala hili tukabaini kuwa wananchi wana haki kwa sababu mmiliki hakupewa kihalali, ndipo nikaagiza wananchi warudishiwe eneo lao," alisema Mnyeti.

Alisema ameshatoa maelekezo ya matumizi ya ardhi hiyo ekari 1,000 hivyo irudishwe kwa wananchi hao ambao watapanga matumizi ya eneo hilo.



Msimamizi wa mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA), katika Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha, Mhandisi Isack Raphael (kushoto), akitoa maelezo kuhusu hatua iliyofikiwa kwenye ujenzi huo, kwa jopo la wataalamu viongozi na watendaji wa wilaya hiyo, waliotembelea mradi huo, juzi. Wa pili kulia ni kiongozi wa jopo hilo, ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Issack Joseph Kadogo. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# Mahabusi Gereza Kisongo wakumbukwa

Zanura Mollel, ARUSHA

KANISA la Wasabato Kijenge, lililopo wilayani Arusha, kupitia Chama cha AMO, juzi limekabidhi msaada wa vitu vyenye thamani ya Sh. milioni 1.2 kwa wafungwa na mahabusi wa Gereza Kuu la Kisongo mjini hapa, kwa ajili ya kujikimu na kusaidia mahitaji mbalimbali.

Akizungumza jana baada ya kutoa msaada huo, Mwenyekiti wa AMO, katika kanisa hilo, Mchungaji Mugwe Thomas Mkono, alisema chama hicho kina wauminі 85 ambao wamejitolea kutoa huduma hiyo, katika gereza hilo kwa ajili ya kusaidia wafungwa na mahabusi.

"Msaada huu leo umetolewa na wanaume wa chama hiki kwa kuchangishana, ambao wameanza kwa kupeleka msaada wa vitu kwa wafungwa na mahabusi waliopo katika gereza hili, pamoja na kutoa msaada huu, tutaendelea na huduma ya uinjilisti," alisema Mchungaji Thomas.

Mzee wa kanisa hilo, William Waziri alisema, mikakati ya kanisa kwa mwaka 2020, ni kuwafikia watu wanaoishi katika mazingira magumu ikiwamo wafungwa na watu wasiojiweza.

"Tunahitaji kuwafikia kwa lengo la kuwapatia mahitaji ya kimwili na kuwaonyesha upendo Wakristo ili kuwaondoa katika kutenda maovu, yaliyosababisha kuwa gerezani kwa kufuata taratibu za nchi," alisema waziri.

Watanzania wameaswa kujitoa na kuwasaidia wafungwa na mahabusi kwa upendo, kwa kuwa hata hao waliopo gerezani na mahabusu ni wanadamu kama watu wengine wanahitaji kupewa ushauri na msaada.

# Sababu kuchelewa mradi wa maji yatajwa

**Na Godfrey Mushi, MWANGA**

SERIKALI imetaja sababu kuu ya kuchelewa kukamilika kwa mradi mkubwa wa maji katika Wilaya za Mwanga, Same mkoani Kilimanjaro na Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga ni kukwama kwa vifaa Bandari ya Dar es Salaam.

Mkwamo huo ulithibitishwa juzi na Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, baada ya kutembelea kwa awamu ya pili na kukagua mradi huo Wilaya ya Mwanga.

Akiwa Wilaya ya Mwanga, alisema: "Kuna baadhi ya sababu zinazosababisha mradi huu kuchelewa kukamilika, mojawapo ni ucheleweshwaji wa vifaa katika Bandari ya Dar es Salaam.

"Kama waziri mwenye dhamana naamini kwamba siku siyo nyingi wananchi wa wilaya hizi tatu watapata maji ya kutosha kutoka kwenye mradi mkubwa wa maji unaojengwa kwa sasa. Mradi utahudumia wilaya mbili za Mkoa wa Kilimanjaro ambazo ni Mwanga na Same na wilaya moja ya Mkoa wa Tanga ambayo ni Korogwe."

Mradi huo una thamani ya Sh. bilioni 241 na unatarajiwa kunufaisha takribani wananchi 434,000 wa wilaya zote tatu.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Mbarawa amewaahidi wasimamizi wa mradi huo kuwa atafuatilia kwa haraka vifaa hivyo vilivyokwama bandarini ili viweze kutoka na kazi hiyo iendelee kwa kasi.

Alisema vijiji vyote vilivyopitiwa ama vilivyoko kandokando na mradi huo wa maji vitapatiwa maji na kwa sasa wataalamu wameshapewa jukumu na serikali kuandika andiko kwa ajili ya vijiji ambavyo awali vilikuwa havijajumuishwa kwenye mradi.

Ili kuhakikisha kuwa zoezi la kukamilisha mradi huo linakwenda kwa haraka, Waziri Mbarawa amemwagiza mkandarasi wa mradi huo kuhakikisha wanaajiri makandarasi wengine ili kuifanya kazi iende kwa haraka na kukamilika kwa wakati.

Kwa mujibu wa Prof. Mbarawa, mpaka sasa kasi ya mkandarasi siyo ya kuridhisha na kutokana na hali hiyo serikali kuanzia sasa haitafumba macho kama kasi ya mradi itakwenda ndivyo sivyo.

Mradi huo unatekelezwa na kampuni mbili za M.A Kharafi & Sons na Badr East Africa Enterprises.

# Ukimya, uoga, visasi unavyochangia ukatili kijinsia

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

STADI ya awali ya kuhusu ukatili wa kijinsia katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, inaonyesha tamaduni ya ukimya na uoga wa kulipwa visasi ni miongoni mwa visababishi na matokeo ya ukatili wa kijinsia unaoendelea kutikisa katika jamii ya ukanda huo.

Akizungumzia stadi hiyo, mratibu wa mradi wa kukuza usawa wa kijinsia kwa kutumia elimu ya haki za binadamu wa Shirika lisilo la kiserikali la Tusonge CDO, Consolatha Kinabo, alisema mbali na uoga wa kuwapo kwa visasi, kuna jambo jingine la uhaba wa mifumo ya ulinzi pamoja na umaskini.

Alikuwa akitoa mrejesho kuhusu stadi hiyo, wakati wa uzinduzi wa awamu ya pili ya mradi huo uliofanyika katika Manispaa ya Moshi na kujumuisha wadau zaidi ya 50 kutoka mashirika mbalimbali.

"Visababishi na matokeo ya ukatili wa kijinsia tumeona kwamba mtoto wa kike anapata ujauzito, maisha yake ya baaadaye huandaliwa kuwa mama wa nyumbani ila kwa kijana aliyehusika na ujauzito huo huendelea kupata fursa za kufanikiwa kimaisha.

"Sababu zinazochangia ni tamaduni ya ukimya na uoga wa visasi, uhaba wa mifumo ya ulinzi, umaskini, unyanyapaa wa kijamii, uelewa duni wa haki za binadamu na usawa wa kijinsia. Visababishi ni mila potofu na tamaduni zinazokandamiza kutokana na jinsia."

Mkurugenzi Mtendaji wa Tusonge, Agnatha Rutazaa, akiwasilisha matokeo hayo kwa wadau na Kansela Mkuu wa Ushirikiano na Maendeleo wa Serikali ya Canada, kupitia ubalozi wake nchini Tanzania, Gwen Walmsley, alisema aina za ukatili zilizoainishwa na wanajamii ni ukatili wa kingono kwa watoto, rushwa ya ngono na ukatili wa kisaikolojia unaohusisha matusi na vitisho.

Alitaja aina nyingine kuwa ni ukatili wa kiuchumi kama kutopewa elimu, fursa, urithi, ardhi na masuala ya ukatili wa kimwili ikiwamo vipigo na kujeruhiwa na silaha. Yamo pia masuala ya mila potofu kama ndoa za utotoni, ndoa za kulazimishwa na ukeketaji.

Hata hivyo, wakati anazindua awamu ya pili ya mradi huo unaotekelezwa kuanzia mwaka 2019/2024, Kansela Gwen alisema, changamoto ya ukatili wa kijinsia ipo nchini Tanzania na kwamba kwa sasa Tanzania inashika nafasi ya 130 kati ya 160 katika masuala ya haki na usawa wa kijinsia.

"Bado changamoto zipo katika masuala ya usawa wa kijinsia, kwa sababu Tanzania ina uwakilishi mzuri katika utawala, wakati jambo hili linaanza Tanzania ilikuwa na Spika wa Bunge mwanamke, Anne Makinda na sasa tuna Makamu wa Rais ambaye ni mwanamke (Samia Suluhu Hassan) na mengi ambayo tunayaona kwa wanawake wa kitanzania wamechukua nafasi za uongozi ambazo zinatia hamasa watoto wa kike Tanzania nzima," alieleza.

"Naomba niwapongeze Tusonge, Equitas na mashirika mengine kwamba ni matumaini yetu mambo ya msingi kama haki za binadamu na ukatili wa kijinsia yataenda kutatuliwa kwa kupatiwa ufumbuzi wa kudumu."

Kansela Gwen alisisitiza kuwa kwa jinsi Tanzania inavyojitahidi kuzalisha kwa kiwango cha kina cha kati, anaamini taifa haliwezi kuwaacha wanawake nyuma, hivyo ni lazima wahitaji mchango wa wanawake ili kufikia malengo hayo.



Wanawake wanaharakati wa Wilaya ya Siha, wanaoendesha vuguvugu la ukombozi wa mwanamke kimapinduzi (Tapo), wakiandamana kuelekea alipokuwa Ofisa Elimu Mkoa wa Kilimanjaro, Paulina Mkwama (hayupo pichani), kulaani ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyoadhimishwa wilayani humo, mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Akemea rushwa ya kufifisha usawa

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

WAKILI maarufu na mtetezi wa haki za binadamu katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Elizabeth Minde, amekemea kile alichokiita rushwa ya kufifisha safari ya kufikia haki sawa, akitaka wanaharakati wa Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, kuchimba na kuibua mambo hayo.

Alisema kwa kuwa sasa safari ya usawa bado ni mbichi, wanaharakati wanawake wilayani humo wana kila sababu ya kujitokeza zaidi kuibua mambo ambayo wanaona hayaendi sawa kama vile mashauri ya ukatili wa kijinsia yanayoamuliwa kienyeji na hivyo kuendelea kuwaumiza wanawake.

Minde alieleza masikitiko yake wakati akizungumza na wanawake kutoka makundi mbalimbali wakiwamo wanaharakati wa Wilaya ya Siha, kwenye Maadhimisho ya Siku ya Wanawake yaliyofanyika jana katika Kata ya Sanya Juu.

"Tunaomba tuthaminiwe kwa sababu tuna mchango mkubwa sana katika maendeleo ya nchi, safari ya usawa iko moto, safari ya kupata haki sawa bado ni mbichi. Kesi nyingi zinakufa katika madawati ya polisi.

"Tunapenda wanaharakati wa Siha mfuatilie ili yale mambo yanayoishia dawati, yanayoishia Polisi, hospitali, ripoti za uongo kuandikwa hiyo ndio kazi ya wanaharakati kuibua masuala hayo, kwa sababu yanayoendelea yanaumiza," alieleza Wakili Minde.

Akifafanua, wakili huyo alisema wengi wa wanawake bado hawaelewi sheria nyingi, ziwe za mirathi, ndoa na ardhi, licha ya jukumu kubwa la kusukuma uchumi wa nchi walilonalo bila ya kujali itikadi.

"Viti maalumu kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu ni halali yetu na hata viti vingine vya majimbo ni halali yetu, napenda niwausie tusiache hizo nafasi. Matatizo mengi ya kisheria tuliyonayo ni ya kupambana na rushwa ya ngono na pesa ndani ya jamii."

Ofisa Elimu Mkoa wa Kilimanjaro (REO), Paulina Mkwama, akizungumza na wanawake hao aliwataka kutosahau majukumu yao kama mama wa familia, huku akisisitiza kuwa bado wanayo kazi kubwa ya kuhakikisha wanakomesha mimba za utotoni, ukeketaji na ukatili wa kingono dhidi ya watoto.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Ndaki Mhuli, akitoa nasaha zake kwa wanawake hao, alisema serikali inawaunga mkono wanawake hao na itawapa ushirikiano wa kila hali kufikia ndoto zao na hata sera ya utoaji mikopo kwa makundi maalum halmashauri hiyo imekuwa ikilizingatia.

Nipashe

# TESA

Jumanne Machi 10, 2020

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 15

**Haipendezi mtoto kusoma kwa shinikizo la polisi**



Ukurasa 18

'Madudu' yanayosababisha TCU kuvifuta vyuo vikuu



Ukurasa 19

## 'Wasichana mko Eden epukeni sauti ya nyoka'



# Mfumo wa elimu na utetezi wa Dk. Bashiru ziarani IPP

Ukurasa 16

ELIMU YA KIPOLISI

# Ni lazima kupambana na dawa za kulevya



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia na Kudhibiti Dawa za Kulevya, Rogers Siang'a, akizungumzia udhibiti wa mihadarati. **PICHA: MTANDAO**

BIASHARA ya mihadarati ni kosa la jinai na tishio kwa usalama wa wananchi na taifa kwani imekuwa ikizalisha makosa mengine makubwa na yanayoathiri maisha ya raia kama vile usafirishaji haramu wa binadamu (human trafficking), kutakatisha pesa (Money laundering) na makosa mengine yanayovuka mipaka ya mataifa (trans-national organized crime).

Serikali ikishirikiana na wadau wengine ndani na nje ya nchi inafanya jitihada katika kuzuia na kupambana na tatizo hili kwa kutumia vyombo vyake vya dola vinavyohusika katika kudhibiti na kupambana na mihadarati.

Wahusika hawa ni Jeshi la Polisi chini ya Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai ikisaidiana na wadau wengine wanaohusika kwenye ukamataji na upelelezaji wa makosa haya kuhakikisha tatizo hili linadhibitiwa kikamilifu.

**POLISI INAVYOHUSIKA**

Mikakati ya Jeshi la Polisi katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya ni pamoja na kuanzisha madawati maalumu yanayoshughulika katika ukamataji, upelelezi na ukusanyaji wa taarifa za kiintelijensia kwa makosa ya dawa za kulevya, ikisaidiana na kitengo cha Polisi Jamii katika mikoa yote pamoja na kanda zake.

Uelimishaji wa jamii kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya, uuzaji na usafirishaji wa dawa za kulevya, kwa kutumia fursa hizo katika makongamano mbalimbali, warsha, sherehe mbalimbali za kitaifa ili kuweza kupunguza tatizo hilo kwa haraka kuliko kupambana na raia moja moja au vikundi vidogo vidogo.

Uimarishaji wa doria, misako na operesheni katika vijiwe na mitaa yote ambayo wahalifu hao wamekuwa wakikaa na kufanya biashara hiyo ya dawa za kulevya, hivyo kupunguza tatizo hilo kwa baadhi ya mitaa na vijiwe vingine kupelekea kusambaratishwa kabisa.

Kuimarisha doria za majini na ulinzi mipakani mfano viwanja vya ndege mipaka ya nchi kavu kwa kushirikiana na taasisi nyingine za kiserikali na zile za binafsi katika kupambana na wahalifu ambao wamekuwa wakitumia boti na majahazi ya kisasa katika kuingiza dawa za kulevya, pia usafiri wa ndege katika kuingiza na kutoka nje ya nchi.

Mafunzo ya kuwajenga wapelelezi na watafutaji wa taarifa (intelligence) yamekuwa yakitolewa ndani na nje ya nchi kwa udhamini wa wadau mbalimbali kutoka wahisani ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na kusaidia kupunguza tatizo la dawa za kulevya.

**MIKAKATI KIJAMII**

Kuimarika kwa mfumo wa utoaji taarifa toka kwa jamii husika kutokana na uhamasishaji na uelimishaji kuhusu athari za dawa za kulevya, unaotolewa na Jeshi la Polisi pamoja na wadau wake, vilevile kutokana na mzigo ambao familia, jamii husika na taifa imekuwa ikipata kutokana na kuhudumia waathirika wa dawa za kulevya, hivyo jamii yenyewe wamehamasika katika kushiriki moja kwa moja katika utoaji wa taarifa za uhalifu na wahalifu wa dawa za kulevya bila shuruti.

Taasisi binafsi, baadhi ya wananchi wazawa, taasisi za kidini na wadau wengine wameshiriki katika vita hii ya kupambana na dawa za kulevya kwa kujenga na kuanzisha vituo vya kulelea waathirika wa dawa za kulevya (Sober houses) katika maeneo mbalimbali ya nchi, na serikali imekuwa ikiwapa ushirikiano wa ushauri na kuwashirikisha katika hafla mbalimbali za kitaifa ili kuleta hamasa kwa jamii na taifa.

Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) yanashiriki katika udhibiti na upambanaji wa janga la dawa za kulevya kwa watoto na vijana kwa kuunda vikundi vya michezo mbalimbali inayohusisha makundi ya vijana wa mitaani, watoto walio katika makambi ya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira magumu, na wanafunzi waliopo kwenye vyuo mbalimbali.

**MIKAKATI KITAIFA**

Kutungwa kwa sheria mpya Na 5 ya mwaka 2015 ambayo imefanya baadhi ya marekebisho katika sheria ya zamani na kuziba mianya na upungufu ambao wahalifu wamekuwa wakiitumia katika kukwepa mkono wa sheria.

Kuundwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Mihadarati ambayo imepewa nguvu ya kukamata, kupeleleza, kukusanya taarifa za uhalifu na wahalifu wa dawa za kulevya, hivyo kusaidia Jeshi la Polisi na taasisi nyingine zisizo za kiserikali zinazojihusisha katika kupambana na uhalifu huu katika kupunguza kasi za ongezeko la tatizo.

***Ofisi ya Uhusiano Makao Makuu ya Polisi.***

JIELIMISHE

# Wanawake 6,000 hupata VVU kwa wiki

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Kutokomeza Ukimwi (UNAIDS), hivi karibuni mjini Geneva Uswisi na Johannesburg Afrika Kusini, lilizindua ripoti mpya ikionyesha kuwa wanawake wamekuwa wakiambukizwa zaidi VVU kwa kasi kubwa.

Hali hiyo inasababishwa na kukosekana kwa usawa na fursa sawa kati ya wanaume na wanawake hali inayosababisha kuendelea kuwafanya wanawake na wasichana kuwa katika hatari ya kuambukizwa zaidi VVU.

Hivyo ugonjwa huo kusalia kuwa sababu ya kwanza ya vifo miongoni mwa wanawake wenye umri wa kupata watoto ikiwa ni takribani miaka 40 tangu kuanza kwa ugonjwa huo.

Taarifa kuhusu ripoti hiyo iliyotolewa kuelekea Siku ya Kimataifa ya Wanawake, imemnukuu Mkurugenzi Mtendaji wa UNAIDS Winnie Byanyima, akisema, "VVU linahusika na ukosefu wa usawa na haki vinavyowakabili wanawake na wasichana na jinsi upungufu katika haki na huduma, vinavyozidisha tatizo hili. Hii haikubaliki, inaepukika na inatakiwa kufikia ukomo."

Miaka 25 iliyopita, serikali zilifanya jambo la kihistoria kupitisha Azimio la Beijing na Jukwaa la Kuchukua Hatua, mpango mkakati wa kimataifa ulio kamili wa kutimiza haki za binadamu za wanawake na wasichana na kufikia usawa wa kijinsia.

Ripoti ya UNAIDS inafafanua kuwa hatua zimepigwa katika maeneo ya msingi ikitolea mfano, wasichana wengi wako shule na pengo la jinsia katika shule za msingi linapungua duniani kote. Katika baadhi ya nchi kuna wanawake wengi wanaohusika katika uongozi wa kisiasa na nchi nyingine zimefanya kazi kuwalinda haki za wanawake katika sheria.

Matibabu ya VVU yameongezeka ambapo kufikia katikati mwa mwaka 2019 kulikuwa na zaidi ya watu milioni 24 waliokuwa wanaishi na VVU na wakiwa kwenye matibabu wakiwamo wanawake milioni 13 wenye umri wa miaka 15 na zaidi.

Ripoti hiyo pia inaonyesha hata hivyo kuwa ahadi nyingi zilizotolewa kuboresha maisha ya wanawake na wasichana kote duniani, hazijatekelezwa. Takribani miaka 40 ya mapambano dhidi ya ugonjwa huu, umesalia kuwa chanzo cha vifo vya wanawake wa kati ya umri wa miaka 15 na 49 na wanawake wa umri mdogo takribani 6,000 wa umri wa miaka 15 hadi 24, wanapata VVU kila wiki.

Ripoti inasema, "tuna maeneo muhimu ya kushughulikia ikiwamo kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake. Katika maeneo ambayo kuna maambukizi makubwa ya VVU, ukatili wa watu waliko katika uhusiano, umeongeza hatari ya wanawake kupata VVU kwa asilimia 50.

"Kuwa na VVU kunaweza pia kuchochea vurugu, ambapo wanawake wanaoishi na VVU wamekuwa maara kwa mara wakiripoti kufanyiwa ukatili kutoka kwa wenza wao, familia na wanajamii na pia katika huduma za afya."

Aidha, ripoti inaeeleza hatua kadhaa za kuchukuliwa ili kurekebisha hilo na kutaja kuwekeza katika sera na programu za VVU ambazo zimethibitisha kukuza usawa wa kijinsia, kuwekeza katika elimu, ikiwemo ya afya ya uzazi na uwezeshaji wanawake na wasichana kiuchumi, kurekebisha sheria ambazo zinakawamisha haki sawa kwa wanawake na wasichana wote ikiwamo hatua za kukomesha unyanyapaa na ubaguzi, unyanyasaji na uhalifu unaoelekezwa kwa wanawake na wasichana. **UN Reports**


Mkurugenzi Mkuu wa UNAIDS, Winnie Byanyima. **PICHA: MTANDAO.**

ELIMU

## NA MWALIMU REUBENI LUMBAGALA

# Haipendezi mtoto kusoma kwa shinikizo la polisi

TUPO kwenye karne ya 21 yenye kasi kubwa ya maendeleo kwenye kila nyanja, lakini wapo baadhi ya Watanzania wanaoishi maisha ya karne za nyuma kwenye zama hizi za sayansi na teknolojia.

Hawa ni wale wanaokataa kusomesha watoto wakingoja mkono wa dola uwashukie. Wanasubiri kusikia msako kwa wasioripoti shuleni, kwasioonekana madarasani tangu shule kufunguliwa. Wazazi na walezi hawa vipi?

Hili ni tatizo kubwa. Maisha ya karne za ukoloni hayajaweka mkazo wala msukumo mkubwa kwa wananchi kusaka maarifa kupitia shule kwani tulikuwa tupo chini ya utawala wa wakoloni na hata umuhimu wa elimu haukufahamika kwa walio wengi.

Ikumbukwe elimu ilisaidia sana kupata ukombozi wa kifikra hadi kufikia hatua ya kuuchukia ukoloni na kuanzisha harakati za kudai uhuru ili wananchi waweze kujitawala wenyewe na kufurahia maisha.

Baada ya nchi nyingi za Afrika kupata uhuru wake na Tanzania ikiwamo, kumekuwa na juhudi kubwa za kuinua sekta ya elimu kuanzia kisomo cha awali hadi elimu ya juu.



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Liberatus Sabas, akiwa na wanafunzi shuleni akiwafundisha masuala ya elimu. **PICHA: MTANDAO.**

Kwa ngazi za Juhudi kubwa zinazofanywa na serikali na sekta binafsi za kuinua sekta ya elimu baada ya uhuru, zinatokana na ukweli kuwa, juhudi za maendeleo katika nyanja zote zinaanzia na zinategemea sana mafanikio ya sekta ya elimu.

Hivyo, kabla ya kuinua sekta nyingine zozote, ni lazima kuanza na elimu, kwani elimu ndiyo chanzo cha maarifa kinacholetea mafanikio ya kila sekta ili kufikia maendeleo endelevu.

Kumekuwa na ongezeko kubwa la ujenzi wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu hapa nchini ili kuongeza wigo wa udahili wa wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu ili kuwa na wasomi wa kutosha ambao ni rasilimali muhimu kwa ajili ya kuongeza kasi ya maendeleo na ukuaji wa uchumi.

Ili kuhakikisha kila mtoto anapata haki yake muhimu ya elimu, mwaka 2016 serikali ilianza kutekelezeka kwa vitendo sera ya elimumsingi bila malipo ili wanafunzi kuanzia darasa la awali hadi kidato cha nne waweze kusoma shule bila kulipa ada na michango mingine ambayo ilikuwa kero kubwa kwa wazazi na walezi kusomesha watoto wao.

Tukiwa tupo karne ya 21 yenye raia wenye kiu kubwa ya kusaka maarifa, ujuzi na stadi mbalimbali (elimu), wapo baadhi ya Watanzania wachache ambao wanarudisha nyuma juhudi nzuri za sekta ya elimu kwa kuwakataza na kuwazuia watoto wao wasijiunge na elimu hasa elimu ya sekondari ya kidato cha kwanza baada ya kufaulu elimu ya msingi na hatimaye kuchaguliwa kujiunga na shule za serikali kuendelea na masomo yao.

> “Wazazi na walezi wajifunze kutokana na makosa. Wapo wengine ambao ni kizazi kisichosoma, wangependa na watoto wao waingie katika mkumbo huo?

Baadhi ya wazazi na walezi wa aina hii ni kikwazo kikubwa kwa mpango wa serikali wa kuhakikisha kila mtoto anapata haki yake ya msingi ya elimu ili aweze kujitegemea baada ya kuelimika shuleni.

Ni jambo la kushangaza kuona licha ya utekelezaji wa sera ya elimumsingi bila malipo, bado baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa kikwazo dhidi ya elimu za watoto wao kwa kutowapeleka shule kwa wakati kujiunga na masomo ya sekondari.

Kwa kuwa serikali ina mkono mrefu na imedhamiria pasi na shaka kuhakikisha kila mtoto anapata elimu, imeamua kutumia vyombo vyake vya ulinzi na usalama kuwasaka wazazi na watoto ambao bado hawajaripoti shule tangu muhula wa masomo ulipoanza Januari 6, 2020.

Viongozi wa serikali katika wilaya na mikoa kote nchini wamekuwa wakitoa takwimu katika maeneo yao juu ya idadi ya wanafunzi ambao hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari mwaka huu walikuwa bado hawajaripoti kwenye shule za sekondari walizopangiwa kujiunga nazo. Hata baadhi ya wanafunzi walioripoti kwenye shule mbalimbali, kunatokana na nguvu ya ziada iliyotumiwa na migambo na askari polisi kuwakamata wazazi ambao watoto wao hawakuripoti.

Wakuu wa wilaya, wakurugenzi, mofisa tarafa, watendaji kata na wa vijiji kote nchini wanafanya kazi kubwa kufuatilia watoto ambao hawajaripoti shule ili waweze kuripoti shule na kuanza masomo mara moja.

Nikiwashauri wazazi na walezi ni wakati wa kubadilika na kuendana na dunia ya sasa ambayo bila elimu ni kama watu wanaoishi gizani. Nyakati hizi ni za kila mtoto kupata haki yake ya elimu. Hatuwezi kuishi maisha ya miaka 1947 kwenye dunia ya mwaka 2020.

Ni fedheha kubwa kwa karne ya 21 tuliyopo mtoto kusoma shule kwa msukumo wa wanamgambo, polisi jamii na polisi na si kwa ridhaa ya wazazi na walezi wenyewe.

Maisha halisi ya wazazi na walezi wanaowakataza watoto wao wasisome ni fundisho tosha la kuhitaji ukombozi wa elimu kwenye kaya zao ili kupata wasomi wa kukomboa familia zao.

Ni wakati wa wazazi kubadilika na kuiunga mkono serikali kwa kuwapeleka watoto shuleni na pia kuwapatia mahitaji muhimu kama sare, viatu, madaftari na chakula ili wasome vizuri na wafanikiwe maishani. Elimu ndiyo ukombozi wa maisha ya watoto, wazazi na Taifa lao. Wazazi tubadilike.

Wazazi na walezi wajifunze kutokana na makosa. Wapo wengine ambao ni kizazi kisichosoma, wangependa na watoto wao waingie katika mkumbo huo?

Waliosema elimu ni ufunguo wa maisha waliufahamu ukweli kuwa kwa kuelimisha watoto, wazazi na walezi wana uhakika wa kupata maisha bora, kumudu maisha yao na kwa ujumla kuwa na dunia bora kuliko ile ya wazazi na wao.

Ikumbukwe hata maandiko yanawakumbusha wazazi na walezi na watoto wao kuitafuta elimu.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***
***Maoni: (+255) 764 666349.***

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Mfumo wa elimu na utetezi wa Dk. Bashiru ziarani IPP



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally (kulia), akifurahia jambo na Wahariri na Viongozi Waandamizi wa Kampuni ya The Guardian Ltd, inayochapisha magazeti ya The Guardian an Nipashe, alipotembelea ofisi za kampuni hiyo, eneo la Viwandani, Mikocheni, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOHN BADI**

KATIBU Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ali, siku za karibuni amekuwa akitembelea vyombo vya habari kufahamiana kwa karibu zaidi na tassisi hizo na pia kutumia uwapo wake na mazungumzo na sehemu ya viongozi na watawala wa tasnia hiyo kwa uenezi.

Katika muendelezo huo Dk. Bashiru amezuru vyombo vya IPP Media na kuzungumzia masuala kadhaa mojawapo likiwa ni hali ya elimu na kile wabunge wanachoishauri serikali kukifanya ili kuiboresha sekta hiyo.

Kwa Katibu Mkuu wa CCM ni fursa ya kutoa maelezo kuhusu inachokielewa CCM kuhusu masuala tofauti ambako hili la uchaguzi ni wazi linachukua nafasi kubwa kila aendako, lakini yako masuala ya ziada. Mojawapo ni hitaji lililoelezwa na wabunge kuwa iundwe tume ya kuangalia upya mfumo wa elimu nchini halafu serikali itekeleze mapendekezo yake, kuondoa upungufu mkubwa uliopo sasa.

Wakati suala hilo bado linajadiliwa bungeni, ingawa Naibu Waziri wa Elimu, William ole Nasha, alitoa maelezo kuwa serikali iko mbioni kupitia upya mfumo wa elimu na kuangalia wapi pa kufanya marekebisho, Katibu Mkuu wa CCM alikuwa na hisia tofauti.

> “ Eneo jingine ni lugha, kuwa licha ya kutumia Kiingereza elimu ya sekondari, uwezo wa kumudu mazungumzo katika lugha hiyo nje ya kupokea maelezo darasani ni mdogo.



Baadhi ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu kwenye moja ya chuo kikuu kilichoko jijini Dar es Salaam. **PICHA MTANDAO.**

Anakataa kabisa wazo kuwa mfumo wa elimu ni mbaya, kuwa wanaotokana na vyuo na vyuo vikuu vya Tanzania hawana stadi za kuajiriwa na wana elimu ya kinadharia isiyoweza kutumika kama mtaji katika ajira. Pia hawana uwezo au stadi stahiki za kujiajiri wenyewe, masuala ambayo ni mapana kujadili katika ziara ya saa chache.

Dk. Bashiru alikuwa na majibu kwa hoja hizo au madai hayo (kwa mitazamo ya wadau tofauti) akisema kuwa elimu inayotolewa hapa nchini ni nzuri, na wahitimu wake wana uwezo wa kushindana kokote pale duniani. Licha ya kuwa maeneo ya ulinganisho aliyotoa hayakuwa na uhakika kitakwimu bila kutafuta kwa mapana zaidi, kila ambaye amewahi kusoma nje anaweza kufanya mlinganisho kivyake. Kuna walimu hawahesabiki kutoka Tanzania wanaofundisha au waliofundisha nje nyakati zilizopita, na huwezi kusema kuwa uwezo huo ulijengwa tu na kusoma masomo ya ziada nje, hasa katika ngazi ya ‘uzamivu,’ ila msingi uliojengwa hapa.

Licha ya kuwa hapakuwa na maelezo ya wazi kwa maeneo mengine ya ukinzani au ukosoaji kuhusu elimu, inatosha tu kuangalia kama ulinganisho huo unatosha kusema kama elimu yetu inafaa au hapana. Unaweza kusema maelezo hayo ni kama yanadhihirisha nyufa katika mjadala kuhusu mfumo wa elimu. Hivi kuna uwezekano mfumo mbovu utoe wanafunzi au wahitimu shindanishi nchi za nje?

Inabidi kwanza mtu akatae kuwa wahitimu wa Tanzania wanaweza kushindana ‘nguvu sawa’ na wale wa nje, bila kuwepo uhakika wa awali kuwa wale wa nje ndiyo watakaoshinda, ili hoja ya awali iwe sahihi.

Hata hivyo, yako maeneo kadhaa ya kuangalia katika matukio ya siku hadi siku kujua ngazi ya elimu na aina gani ya mwanafunzi anayetoka hapo, halafu kigezo hicho pia kitumike kwa nchi za nje au za jirani, kama wahitimu wao wana udadisi mkubwa kuliko wa kwetu, au ufahamu wa maeneo mengi zaidi ya kitaaluma na kijamii kuliko sisi. Ni ulinganisho wa hisia na uwezo wa kuingiliana kitaaluma na kijamiii kwa mfano mikutanoni.

Njia nyingine ambayo si rahisi kuigundua au kuifuatilia kwa haraka ni kuangalia katika mazingira ya kila siku ya nchi za jirani, na hapa tumezoea kujilinganisha zaidi na Kenya na siyo Uganda. Enzi za kipindi cha uhuru Uganda ndiyo waliokuwa na chuo kikuu pekee Afrika Mashariki, Makerere halafu vingine vikafuata, kwani kila nchi iliweka kipaumbele cha kuwa na chuo kikuu chake baada ya uhuru.

Kwa muda wa miaka mitano au sita kukawa na Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki na vyuo vikuu vikawa shirika, kwani mapema zaidi vilikuwa hasa ni sehemu ya Chuo Kikuu cha London, kikisimamia mitaala. Mabadiliko ya mitaala yakaanza katikati ya miaka ya 1960 hasa Dar es Salaam, na kufikia 1970 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kikawa chuo kikuu huru, na taasisi ya Afrika Mashariki ikasambaratika.

Kwa wanaosoma magazeti ya Kenya kwa mfano, siyo rahisi kukuta mjadala wa viwango vya elimu nchini, kwani kilichojengwa miaka ya awali hadi kufikia uhuru hakijabadilika sana. Kuna mikondo tofauti hasa katika elimu ya juu na fani za jamii zaidi, ambako kila nchi ina ushindani wa kiitikadi unaotegemea jinsi jamii hiyo ilivyofikia uhuru, hisia zake na ni kwa njia gani zinaunganishwa kuwezesha ajenda endelevu za maendeleo, au utengani kiasi fulani kisiasa na kijamii.

### KIINGEREZA

Wakati mwingine inawezekana kusema kuwa yote haya yanakuwa na athari katika elimu, mivutano ya nini cha kuamini au kukataa.Kwa upande mwingine tatizo la mfumo wa elimu ni kielelezo cha utamaduni kuwa wanafunzi hawana upana wa uelewa wa masuala ya kigeni (ya tamaduni za nje) kwani historia ya dunia haifundishwi katika mashule, bali ya Afrika.

Eneo jingine ni lugha, kuwa licha ya kutumia Kiingereza elimu ya sekondari, uwezo wa kumudu mazungumzo katika lugha hiyo nje ya kupokea maelezo darasani ni mdogo. Na kwa jumla wahitimu wa Tanzania wanaweza wasichangamkie fursa za kukutana na kuongea kwa Kiingereza labda kama wanatafuta kazi, na sehemu za kazi, maofisa si wachache wanaongea lugha hiyo kiofisi wanajitahidi tu, hasa wasio na shahada.



Kuboresha elimu kuzingatie kuweka kabati za kutunza vitabu na madaftari shuleni ni muhimu ili kuwapunguzia wanafunzi mzigo wa kutembea na vitabu na daftari muda wote. **PICHA MTYANDAO.**

> “ Unaweza kusema maelezo hayo ni kama yanadhihirisha nyufa katika mjadala kuhusu mfumo wa elimu.

Aidha, ni vigumu kwa wahitimu kuzungumza lugha hiyo hata kuandika maombi ya kazi. Ni wachache wanaoweza kujieleza kwenye mahojiano yote haya yanaweza kuwaweka pabaya hasa kwenye ajira zinazotolewa na mashirika ya kimataifa pamoja na asasi za kigeni.

### BUNGE

Inavyoelekea kuna chembe ya tatizo ambayo inasukumwa katika mfumo wa elimu wakati suala liko kwingine, yaani hili tatizo la ajira, kwani hakuna uhusiano kati ya kuwa na uwezo wa kufanya kazi na kupata kazi ya kufanya. Walichosema wabunge katika taarifa ya kutaka iundwe tume kilikuwa kimesheheni viashiria kuwa ajira kwa jumla zinakosekana kwani vijana hawaajiriki, hoja ambayo haiwezi kuwa sahihi kabisa.

Inavyoelekea ni kuwa wabunge wana hisia kali kuhusu mfumo wa elimu kwa sababu ambazo kwa upande mmoja ziko wazi na kwa upande mwingine si rahisi kudhihirisha ubovu wa elimu nchini. Hivyo si rahisi kusema kuwa waajiri wanapata shida kupata watu wanaofaa maeneo tofauti, lakini kuna matatizo ya ziada kwa mfano teknolojia kuondoa sehemu kubwa ya kazi za asili .

Kwa mfano katika vyombo vya habari aliyotembelea Dk. Bashiru, ni eneo ambalo haliwezi kutatuliwa kwa elimu bali mikondo mipana zaidi ya biashara, wawekezaji na watangazaji bila kusahau athari za utandawazi katika vyombo vya habari kwa kuwa wengi wanatumia simu zao na mitandaoni kulipia gharama kiasi kusoma machapisho mbalimbali.Aidha, hupata kila kitu cha ndani na nje ya nchi kupitia mitandao ya kijamii na hiyo ni changamoto mojawapo inayotishia hatma ya tasnia ya habari.

RIPOTI

## Surua tishio Sudan Kusini



Mtaaalamu wa afya akihudumia watoto nchini Sudan Kusini. **PICHA: MTANDAO.**

TANGU kujitenga na Sudan na kuwa taifa huru, Sudan Kusini kwa mara ya kwanza, imezindua kampeni ya nchi nzima kuwalinda watoto milioni 2.5 dhidi ya surua, ambayo bado ni tishio nchini humo.

Kampeni hiyo inafanywa kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Afya ya Sudan Kusini, Muungano wa Chanjo Duniani -Gavi, na mashirika ya Afya Duniani (WHO) na Shirika la Watoto Duniani (UNICEF) pamoja na wadau wengine.

Zaidi ya chanjo, pia watoto wanapewa virutubishio vya vitamini A na vidonge vya kudhibiti minyoo.

Ripoti ya WHO na UNICEF inaeleza kuwa kampeni hiyo ni muhimu kwa afya ya watoto nchini Sudan Kusini, wakati huu ambao nchi bado inapambana na mlipuko mbaya wa surua ambapo tayari watoto 4,700 walithibitishwa na vifo 26 vimetokea tangu Januari mwaka jana 2019 hadi kufikia mwezi uliopita.

“Tunahitaji kuongeza chanjo ili kuwalinda watoto dhidi ya milipuko wa surua” ameeleza Dkt Makur Matur Kariom wa Wizara ya Afya ya Sudan Kusini akiongeza kusema, “Kwa bahati mbaya, katika Sudan Kusini chanjo ya mara kwa mara dhidi ya surua inabakia katika kiwango cha chini cha asilimia 59 pekee. Kwa maana hiyo watoto wengi katika nchi yetu hawalindwi dhidi ya ugonjwa.”

Kampeni hiyo itaendeshwa kati ya awamu mbili ya kwanza imeanza sasa na itakwenda kwa takribani asilimia 70 ya kaunti zote katika eneo lililokuwa Equatoria ya Kati, Equatorial ya Mashariki, Jonglei, Lakes, Bahr el Ghazal Kaskazini, Bahr el Ghazal Magharibi, Warrap na Upper Nile.

Awamu ya pili itaendelea katika maeneo yaliyobaki za Equatoria ya Kati, Jonglei, Unity, Upper Nile na itahitimishwa wiki ijayo Machi 2020.

Taarifa hiyo ya WHO na UNICEF inasema chanjo hiyo si tu inawalenga watoto ambao hawajachanjwa, bali pia wale ambao walishapata chanjo moja ya awali wanachanjwa tena.

“Kila mtoto ana haki sawa na hakuna mtoto aliyeko mbali sana.” Anaeleza Dk Mohamed Ag Ayoya, Mwakilishi wa UNICEF nchini Sudan Kusini. **UN NEWS**

JE, WAJUA?

# 'Madudu' yanayosababisha TCU kuvifuta vyuo vikuu



Wahitimu wa vyuo vikuu wakiwa katika mahafali yao. **PICHAZOTE: MTANDAO**

MABORESHO yaliyofanywa na serikali kwenye Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu (HEAC) lililoanzishwa mwaka 1995, yalipelekea kuundwa Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) iliyoanza mwaka 2005.

Lengo la kuanzishwa HEAC ilikuwa kudhibiti ubora wa vyuo vikuu nchini vilivyokuwa vinaanzishwa na kuendeshwa na taasisi binafsi. Uanzishwaji wa vyuo binafsi ulitokana na mabadiliko yaliyofanywa na serikali katika uendeshaji wa elimu ya juu mwishoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Ili kuweka uhusiano mzuri kati ya serikali na sekta binafsi na uoanishaji wa elimu itolewayo na vyuo vikuu nchini, pamoja na kuzingatia kuwa suala la ubora ni mtambuka linahusu taasisi zote zinazotoa elimu ziwe taasisi za serikali au taasisi binafsi, baraza lilifanyiwa maboresho na mwaka 2005 iliundwa TCU ili kuongeza majukumu ya kudhibiti ubora katika vyuo vikuu vinavyomilikiwa na kuendeshwa na serikali.

Katibu Mtendaji wa TCU, Profesa Charles Kihampa, anasema TCU ilipewa majukumu makubwa matatu ambayo pamoja na kusimamia sheria, kanuni na taratibu za uanzishaji na uendeshaji wa vyuo vikuu nchini.

Jukumu lingine ni kusaidia na kutoa miongozo kwa vyuo vikuu kuhusu uthibiti wa ubora wa vyuo vikuu, njia mbalimbali za uendeshaji wa vyuo, kuandaa na kuratibu mafunzo mbalimbali kwa wahadhiri, waendeshaji na viongozi wa vyuo vikuu nchini.

> Licha ya TCU kutoa ushauri, mafunzo na namna mbalimbali za uboreshaji, na muda wa kufanya maboresho, baadhi ya vyuo havikufanikiwa kufanya maboresho kama inavyotakiwa.

Anasema jukumu la tatu ni kutoa ushauri kwa umma, vyuo vikuu na serikali kupitia waziri mwenye dhamana ya elimu nchini kuhusiana na mabadiliko mbalimbali ya sayansi, teknolojia, sera na mwelekeo wa elimu ya vyuo vikuu nchini na duniani kwa ujumla.

### MAFANIKIO

Profesa Kihampa anasema katika uongozi wa serikali ya awamu ya tano, TCU imetekeleza majukumu yake ya kisheria kwa ufanisi mkubwa, ikiwa ni pamoja na kusimamia ubora wa elimu inayotolewa na vyuo vikuu.

Anasema TCU imeendelea kuimarisha mifumo yake ya udhibiti ubora ili kuhakikisha inatimiza jukumu lake la kuhakikisha vyuo vikuu vinaendana na mwelekeo wa nchi, Tanzania ikilenga kuwa taifa la watu wenye maarifa, ujuzi mkubwa, weledi na uwezo wa kutatua matatizo ya kijamii na kiuchumi kwa manufaa ya wananchi wake ifikapo mwaka 2025 na kuwa nchi ya uchumi wa kati unaochochewa na uwapo wa viwanda.

Profesa Kihampa anasema kwa mara ya kwanza tangu TCU ianzishwe, ilifanya ukaguzi maalum wa kitaaluma kati ya Oktoba 2016 na Januari 2017 kwa taasisi zote 64 za vyuo vikuu, vyuo vikuu vishiriki na vituo vya vyuo vikuu.

Anasema lengo la ukaguzi huo lilikuwa kuhakikisha elimu ya juu itolewayo inakidhi viwango vya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Profesa Kihampa anasema matokeo ya ukaguzi yalibainisha kasoro mbalimbali katika uendeshaji wa vyuo vikuu nchini, vyuo 45 vilikutwa na kasoro ndogondogo, hivyo kupewa ushauri kurekebisha katika kipindi kifupi ili viendelee na utoaji wa elimu ya juu.

Anasema vyuo 19 vilikutwa na kasoro kubwa, vikapewa ushauri na muda wa marekebisho, lakini havikufanikiwa kurekebisha katika kipindi kifupi na hivyo kuzuiwa kudahili wanafunzi wapya kuanzia mwaka wa masomo 2017/2018 na viliendelea kupewa ushauri na muda zaidi kufanya maboresho.

### VILIVYOFUTWA

Profesa Kihampa anaendelea kufafanua kuwa hadi sasa, vyuo vikuu tisa kati ya 19 vilisitishwa udahili, vimefanya marekebisho makubwa na vimeruhusiwa kudahili na kuendelea kutoa mafunzo kwa baadhi ya programu za masomo.

Anavitaja vyuo hivyo kuwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Umoja wa Afrika Tanzania (UAUT), Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji (Teku), Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Mihayo - Tabora (Amucta), Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala nchini (KIUT) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Marian (MARUCo).

Vingine ni Chuo Kikuu Kishiriki cha Uhandisi na Teknolojia cha Mt. Yosefu (SJUCET), Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikristo cha Tiba Kilimanjaro (KCMUCo), Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Stefano - Moshi (SMMUCo) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Mt. Fransisko (SFUCHAS).

"Kimsingi, mifumo ya ukaguzi na ufuatiliaji wa mara kwa mara imefanya vyuo kufanya maboresho makubwa katika miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maabara za kisasa, mifumo ya mawasiliano ya kielektroniki, madarasa na kuongeza idadi ya viongozi na wahadhiri wenye sifa stahiki kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo," anasema.

Anaongeza kuwa licha ya TCU kutoa ushauri, mafunzo na namna mbalimbali za uboreshaji, na muda wa kufanya maboresho, baadhi ya vyuo havikufanikiwa kufanya maboresho kama inavyotakiwa.

Kwa kuzingatia muda uliotolewa na hali ya vyuo husika na dosari kubwa zilizobainika ikiwa ni pamoja na uhaba wa rasilimali watu na fedha, Profesa Kihampa anasema baadhi ya vyuo havina uwezo wa kujiendesha hata vikipewa muda zaidi.

Anasema kwa kulibaini hilo, TCU ililazimika kufuta usajili wa vyuo saba na kuelekeza wanafunzi wahamishiwe kwenye vyuo vingine vinavyokidhi viwango vya ubora.

Anavitaja vyuo vilivyofutwa usajili kuwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Eckenforde Tanga (ETU), Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Tiba na Teknolojia (IMTU), Chuo Kikuu cha Mlima Meru (MMU) na Chuo Kikuu cha Tumaini - Kituo cha Mbeya (TUMA - Mbeya Centre).

**ITAENDELEA**

UCHAMBUZI

## NA DK. FELICIAN B KILAHAMA



Baadhi ya mabinti wakiwa darasani ili wafanikiwe, wanahitaji kusaidiwa na kulindwa ili kumaliza masomo bila kuanguka majaribuni. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# 'Wasichana mko Eden epukeni sauti ya nyoka'

MAANDIKO matakatifu yanatutaka tuwalee watoto wetu katika njia ipasayo nao hawataiacha hata wakiwa watu wazima.

Kadhalika, wazazi na walezi na watoto wetu tunatakiwa kuitafuta elimu kwa nguvu zote maana kutofanya hivyo tutaangamia kwa kukosa maarifa ambayo moja ya vyanzo vyake ni elimu.

Kimsingi elimu rasmi inapatikana shuleni ambako kuna walimu na wanafunzi na miundombinu muhimu kuwezesha wanafunzi kuelimika ipasavyo.

Sasa suala la wasichana kuwa wajawazito wakiwa shuleni linatoka wapi? Mbaraka Mwinshehe, miaka ya 1970, katika moja ya tungo zake aliimba: "enyi vijana sikilizeni mnapokuwa shuleni zingatieni masomo yenu na acheni mchezo wa mapenzi mnawapa uchungu wazazi wenu". Maneno haya ni hai mpaka leo hasa nyakati hizi ambazo tabia ya vijana kuchangamkia mapenzi inaotesha mizizi kuliko ilivyokuwa miaka iliyopita. Wakati wa shule za 'middle school' (darasa la tano mpaka la nane) tulisoma mchanganyiko: wavulana na wasichana tena tukiwa vijana wakubwa.

Mfano, shule niliyosomea, tuliomaliza darasa la nane mwaka 1965 karibu wote tulikuwa na miaka 18 au zaidi.

Pamoja na hali hiyo visa vya mapenzi shuleni vilikuwa adimu mno. Tofauti na sasa ambako vijana wengi wanamaliza elimu ya msingi wakiwa na miaka 14 au chini ya hapo, lakini masuala ya ngono na mahusiano ya kimapenzi ni jambo la la kawaida.

Enzi za zamani ilikuwa ni aibu kubwa kwa mwanafunzi kupata ujauzito shuleni. Jamii wakati ule pia ilikuwa na maadili yaliyokuwa yakizingatiwa na wote na kila mzazi alimkanya mtoto yeyote kama anavyofanya kwa watoto wake.

Nia ilikuwa kuhakikisha tabia njema inazingatiwa kwa faida ya jamii nzima na kwa mtoto mwenyewe.

Sasa ni dunia ya zama tofauti na ule wa ujana wetu: umegubikwa na maendeleo ya teknolojia, ni wakati wa kidijitali ukiambata na masuala kama utandawazi; uhuru wa kujieleza; usawa wa kijinsia; demokrasia na yote haya yakisheheni ndani yake kinachoitwa "haki za binadamu". Najiuliza kuweka picha za ngono na mapenzi kwenye mitandao ya kijamii inakuwaje haki ya kibinadamu kama siyo kukengeuka?

Miaka ya nyuma kutii bila shuruti na kuzingatia maadili yanayokubalika kijamii ikiwa ni pamoja na vijana kuwaheshimu wazazi na watu wazima ilikuwa nguzo kwa jamii.

Nyakati hizi hali imebadilika sana vijana wamekuwa wagumu kutii au kuwaheshimu watu wenye umri mkubwa. Lugha za kukejeli kama "hapa Dar-es-Salaam hakuna wazee bali wako huko Msata na Chalinze" yameshamiri .

Hii ishara ya kukosa heshima na kwa mtazamo huo hata ushauri toka kwa wazazi au wazee unadharauliwa matokeo yake ni kama hayo ya wasichana kuwa na mimba

> "Fikiria iwapo darasa zima la wasichana lisheheni wenye mimba je, tunachokitafuta ni kuzalisha watoto shuleni au elimu? Yawezekana kwa bahati mbaya mwanafunzi akawa mjamzito kwa kubakwa.

wakati wanatakiwa kujikita masomoni.

Nakumbuka Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, nyakati hizo, alisisitiza kuheshimiana na kujali utu wa mtu na alihimiza wanafunzi kuweka nguvu masomoni akijua kuwa taifa linahitaji wananchi wenye elimu na nidhamu nzuri.

Sera ya "Ujamaa na Kujitegemea" iliambatana na jamii kuheshimiana na kuthaminiana pamoja na utu wema na siyo wasichana kupata ujauzito wakiwa shuleni.

Hata hivyo sheria, kanuni na taratibu vilikuwapo kuhakikisha jamii inawekwa katika hali isiyopelekea kila mtu kufanya anavyotaka. Hapo mwanzo Mungu alipowaumba Adam na Hawa aliwapa uhuru kamili ulioambatana na haki za binadamu lakini pia aliwawekea mipaka (kwa kuweka kanuni ya kwanza) alipowaagiza kuwa vitu vyote vilivyoumbwa vilikuwa halali yao kutumia isipokuwa matunda ya "mti uliwekwa katikati ya Bustani ya Edeni".

Iwapo kanuni hiyo itavunjwa akawatahadharisha kuwa "hakika mtakufa". Haikuchukua muda mrefu binadamu akaivunja hiyo kanuni alipodanganywa na nyoka na akaitii sauti yake kuliko ya muumba wake akachuma matunda akayala hivyo kukosekana utii kukaanzia hapo.

Lakini haikuishia hapo bado binadamu akawekewa Sheria (Torati). Jinsi jamii ilivyoongezeka kukawekwa utawala na sheria, kanuni na taratibu kuzingatiwa.

Leo kuna bunge ambalo kazi yake kubwa ni kutunga sheria ambazo huambatana na adhabu kulingana na uhalisia wa kosa. Shule zetu pia ziwe za umma au binafsi zina sheria, kanuni na taratibu zake. Moja ya kanuni ni wanafunzi kuzingatia masomo na siyo kinyume cha hapo.

Watoto wetu wanakwenda shuleni kuitafuta elimu ili hatimaye wawe na maarifa na ujuzi katika nyanja mbalimbali.

Sheria ya kijana wa kike kuwa na mimba akiwa shuleni na kutakiwa afukuzwe haitofautiani na amri ya Mungu kwa Adam na Hawa kuwa "mkila matunda ya mti wa kati hakika mtakufa". Walipoitii sauti ya nyoka kifo kikatuandama hadi leo. Hivyo wasichana mkilaghaiwa na kutii sauti za wanaume mkatapa mimba mkiwa shuleni mtafukuzwa mkae mkijua hivyo.

Nakubaliana na hoja kuwa wasichana wanayo haki ya kupata elimu bila kikwazo chochote na inatia moyo tunaposikia wasichana wanafanya vizuri kwenye masomo.

Nawapongeza sana kwa jitihada hizo wanapokazana kupambana na wavulana kielimu lakini baadhi yao wasigeuze shule kuwa mahali pa kuchanganya elimu na mapenzi.

Kwa upande mwingine inasikisha tunaposikia baadhi ya wasichana hawazingatii Sheria bali wanajiingiza kwenye "mapenzi" kwa kuamini kuwa wapo wa kuwatetea kwa kusingizia haki za binadamu.

Ni kweli mwanafunzi akiwa shuleni wanayo haki ya kusoma wakati huo ajue hana haki ya kuzaa maana huo siyo wakati muafaka wa kuzaa. Maliza masomo uwe na haki ya kuzaa au kufanya anavyotaka. Tusidanganyane bali tuambizane ukweli na ukweli utatuweka huru na mafanikio yatakuwa mazuri kinyume cha hapo "majuto ni mjukuu". Sasa inapokuwa hivyo ukafukuzwa kosa ni la nani: mwenye shule au mwanafunzi mwenyewe?

Fikiria iwapo darasa zima la wasichana lisheheni wenye mimba je, tunachokitafuta ni kuzalisha watoto shuleni au elimu? Yawezekana kwa bahati mbaya mwanafunzi akawa mjamzito kwa kubakwa.

Kesi kama hiyo ikithibitishwa anaweza kuendelea na masomo baada ya kujifungua lakini isiwe kwa kujitakia. Nakubaliana na Sheria kuwa anayethibitishwa amejitakia mwenyewe ajue atavuna alichokipanda.

Akijifungua madarasa ya "QT" yapo mengi ataendelea na elimu kadri atakavyoona inafaa. Tujenge taifa lenye maadili mema na watu wenyekupenda kutii kwa kulenga kuimarisha utu wetu: kuheshimiwa na kuheshimiana. Wanaobaka watoto wadogo na wanafunzi sheria zitoe adhabu kali bila kuwaonea huruma.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

## Baadhi ya watu wamekuwa wakifanya biashara mbalimbali kwenye maeneo ya shule na kusababisha wanafunzi wakose utulivu wanapokuwa madarasani. Wadau wanasemaje?



### MESHACK KAPANGE (KATIBU MKUU WA CHAKAMWATA TANZANIA)

KWANZA kabisa Chakamwata ni Chama cha Kutetea maslahi ya Walimu Tanzania. Sasa nikirejea kwenye hoja ni kwamba, ukijipa muda wa kutafakari, utagundua kuwa wenye biashara kwenye mazingira ya shule, wamesaidia kusogeza huduma karibu na wanafunzi.

Zamani sisi tulishinda na njaa shuleni kwa kuwa wazazi wetu hawakuwa na pesa na hata waliokuwa wanapewa pesa iliwapasa kwenda umbali wa kutembea zaidi ya dakika 10 kufuata huduma na zilikuwa chache. Wakati huo mwanafunzi ukipoteza au kuibiwa kalamu ilikula kwake. Sasa hivi kalamu au daftari likiisha wino unapata karibu ili mradi uwe na pesa.

Wateja wa maduka hayo siyo wanafunzi pekee, bali pia walimu na wakazi wengine wa maeneo hayo. Maduka hayo huwa na bidhaa na huduma mchanganyiko na kila wateja wakiwamo wanafunzi wanafuata huduma na bidhaa wanazozihitaji.

Zamani wanafunzi wengi tulishindwa kupata vizuri nukuu za masomo (leson notice) endapo kwa sababu fulani fulani mwanafunzi hakuhudhuria kipindi au hakuhudhuria shule kutokana na kuwa mgonjwa, kwenda nyumbani kufuata mahitaji.

Lakini siku hizi inamchukua mwanafunzi muda mfupi tu kuazima daftari za wenzake, kutoa fotokopi na kuendelea na mada mpya za masomo bila kupoteza muda wa kujisomea kwa kuandika notisi au kuwapotezea wenzake muda wao wa kujisomea kwa kukaa na daftari zao kwa muda mrefu.

Tena ikumbukwe wauza bidhaa na huduma hawa wanakuwa nje ya mipaka ya shule ila karibu na shule na wanafunzi.



### MUSSA KASELA (MWANAFUNZI CHUO KIKUU HURIA, MWANZA)

HILI limekuwa ni tatizo sugu sana katika jamii yetu ya Kitanzania kwa kuwa ni tatizo la muda mrefu kihistoria.

Kimsingi shule au taasisi ya elimu mazingira yake ya kijiografia yanatakiwa kuwa yametengwa katika maeneo tulivu yasiyo na mwingiliano wa shughuli zinazoweza kuharibu utulivu na usikivu. Chanzo kikubwa cha tatizo hili ni kukithiri kwa makazi holela.

Miji na vijiji tulivyonavyo ni makazi, ambayo hayakupimwa na matokeo yake makazi hayo yanavutia uwepo wa shughuli mbalimbali kulingana na wakazi wanavyojisikia. Ndiyo maana utakuta taasisi kama shule na vyuo mazingira yake yamechanganywa na shughuli mbalimbali.

Mwaka 1969 ilipitishwa sera ya uanzishaji na urasimishaji wa vijiji na vijiji vya ujamaa. Utekelezaji wa uanzishaji wa vijiji ulifanyika mwaka 1973/1974. Utekelezaji huo ulikumbana na vikwazo mbalimbali.

Kutokana na changamoto zilizojitokeza serikali iliunda tume ambayo moja ya mapendekezo ilikuwa ni uanzishaji wa taasisi ya kuwaandaa wasimamizi au watendaji wa serikali katika ngazi za vijiji na mitaa hadi kata.

Ndipo ilipoanzishwa Taasisi ya Mipango au Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kwa Sheria ya Bunge ya mwaka 1980.

Moja ya jukumu la hiki ni kuwaandaa wataalam wa mipango wakiwamo wa Mipango-miji wakishirikiana na wataalam wa ardhi kutoka Chuo cha Ardhi.

Lakini watu wamekuwa wakijenga maduka na kufungua biashara mbalimbali karibu na shule na kuharibu usikivu.



### DICKSON CHIROSA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

BIASHARA kwenye maeneo ya shule zinaweza kuwa na changamoto zake na hasa zile ambazo hazina umuhimu kwa wanafunzi, lakini zile ambazo wanafunzi wanazihitaji, mimi sioni tatizo zikiwa karibu na maeneo ya shule, kwasababu zinawasaidia wanafunzi. Kwa mfano maduka au vibanda vya kuuza vifaa vya shule yakiwamo madaftari na kalamu, sioni tatizo vikiwa kwenye maeneo hayo.

Vilevile biashara kama chakula na maji ya kunywa nayo bado nzuri tu kwa ajili ya wanafunzi, kuliko kuwaacha wavuke barabara kwenda mbali kufuata huduma hiyo na wakati mwingine wanaweza kupata ajali za magari, hasa wale wa shule za mijini.

Hivyo kwa mtazamo wangu, ninaona biashara kama hiyo karibu na maeneo ya shule ni nzuri na inasaidia kupata chochote na ikumbukwe kuwa wazazi nyumbani wanawapa watoto wao pesa kidogo kwa ajili ya kipoza njaa wawapo shuleni, kwa kutambua kuwa kuna vyakula vinauzwa karibu na shule.

Labda cha msingi ni kuhakikisha kunakuwa na utulivu ili wawapo kwenye masomo kusiwe na kelele za kuwavuruga. Lakini pia hatua alizochukua kuzuia viwanda kujengwa karibu na maeneo ya shule ni sahihi kabisa hata kama kingekuwa ni kiwanda cha kuzalisha vifaa vya shule, kinatakiwa kuwa mbali na mazingira ya shule kwa ajili ya utulivu na wakati mwingine kuna suala la uchafuzi wa mazingira.



### AUGUSTINE BYALILE (MWALIMU MKUU S/M JITIHADA, DAR)

KABLA sijaanza kujadili swali lako, mimi ninaunga mkono uamuzi wa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa wa kupiga marufuku kujenga viwanda karibu na maeneo ya shule, kwani baadhi ya watu wamejisahau na kufanya wanavyotaka bila kujali kwamba maeneo ya shule yanahitaji utulivu ili kuwawezesha wanafunzi kusoma bila usumbufu.

Ninasema hivyo kwa sababu siyo viwanda tu bali maduka, baa, nyumba za kulala wageni na shughuli nyingine za kibiashara karibu na maeneo ya shule, huvuruga usikivu wa masomo kwa wanafunzi, kwani wahusika wanatafuta wateja bila kujali kwamba kuna wanafunzi wanasoma.

Mategemeo yangu ni kwamba serikali itasimamia jambo hili bila kujali kuwa biashara hiyo ni ya nani, kwani wahusika ni wafanyabiashara na wengine ni wanasiasa na inawezekana kuondoa biashara zao kwenye maeneo ya shule kukawa na ugumu.

Lakini kama serikali imedhamiria, haiwezi kushindwa na kitu bila kujali maslahi ya mtu binafsi kwa ajili ya kuwaondolea wanafunzi na walimu usumbufu ambao wamekuwa wakiupata.

Siyo vibaya maeneo ya shule yakazungukwa na vibanda au maduka ya vitu vya shule, lakini baa, nyumba za kulala wageni, ni hatari kwa wanafunzi.

Huduma hizo zipigwe marufuku kwa ajili ya maendeleo ya elimu ya wanafunzi kuliko kujali biashara zaidi huku upande mwingine ukiumia.



### REHEMA MMANGA (MWANASHERIA, MKAZI WA JIJINI DAR)

KWA sasa imekuwa ni kama jambo la kawaida kukuta shule imezungukwa na shughuli mbalimbali za kibiashara.

Yawezelana kukawa na biashara nzuri tu inayofanyika kwenye maeneo hayo ya kuzunguka shule, lakini pia kuna haja ya kuwa makini nayo, ili isije kuwa inasababisha ukatili kwa watoto. Hivyo kwa maoni yangu juu ya watu wanaofungua biashara maeneo ya shule, wajipime/wachunguzwe kwanza aina ya biashara inayotarajiwa kuwekwa au wanyoifanya.

Serikali ya mtaa inaweza kukagua ili ikiwa biashara hizo hazifai maeneo ya shule, basi ni vyema washauriwe au kuzuiwa kuendesha kuifanya. Kwa ujumla wafanyabiashara wanatakiwa kuzingatia ustawi wa mtoto na utulivu pindi akiwa shuleni. Haipendezi na inasikitisha sana kuona maeneo ya shule kuna mabanda ya sinema, masoko, na shughuli nyingine nyingi.

Ningetamani maeneo ya shule yote yatengwe na yawe yamezungukwa na bustani za miti na mboga. Kwa shule zilizopo mjini hii ni changamoto kubwa. Ifikie wakati biashara hizi ziondolewe ili kupinga vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Mtoto ana haki ya kutunzwa, kulindwa na kupata elimu kama jinsi Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 inavyoelekeza.

Kulindwa ni pamoja na kuhakikisha maeneo yanayozunguka shule ni salama na tulivu kabisa.



# Wanawake asilimia 20 wafikiwa huduma za msaada wa kisheria

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

ASILIMIA 20 ya wanawake mkoani Mbeya, wamefikiwa na huduma za msaada wa kisheria ambao umesaidia kupata haki zao, ikiwamo kumiliki ardhi.

Hayo yalisemwa na Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Gabriel John, wakati akizungumza na Nipashe juu ya jitihada walizozifanya kuwasaidia wanawake kwenye masuala ya sheria.

John alisema licha ya kuwafikia wanawake kwa asilimia 20 kuwapatia msaada wa kisheria, lakini walibaini masuala yanayowafanya haki kuwa ni masuala ya ardhi na kutelekezewa watoto.

Alisema wanawake wengi wanakosa haki ya kumiliki ardhi kutokana na jamii kuendekeza mila na utamaduni uliopitwa na wakati ambao unaamini kuwa mwanamke hawezi kumiliki ardhi ya familia.

Alisema elimu ya sheria imesaidia kuibua kinamama wengi waliotelekezwa watoto wao na kubeba jukumu la malezi bila msaada wowote.

"Wanawake wengi walikuwa nyuma kwenye masuala ya kumiliki ardhi, lakini tumewasaidia kupata haki hiyo jamii nyingi zinamtenga na kumuona hastili kumiliki suala ambalo ni kinyume na sheria lakini wengine waliachiwa jukumu la kulea pekee yao watoto," alisema John.

Aidha, John alisema miongoni mwa vikwazo walivyokutana navyo katika kuwasaidia wanawake kisheria ni baadhi yao kuficha kutoa taarifa.

Alisema baadhi ya wanawake wanaofanyiwa vitendo vya kikatili, ikiwamo vipigo na kunyang'anywa ardhi hawaviripoti kwenye vyombo vya sheria wakiogopa kutengwa na ukoo.

"Katika kuhakikisha haki za wanawake zinalindwa na kuheshimiwa tumejiwekea sisi THRDC kuwafikia wanawake wengi waishio vijijini ili kuwapatia elimu ya masuala ya sheria," alisema John.

Katika taarifa yake mratibu wa kitaifa wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, kwa vyombo vya habari, alisema mwanamke ni mdau muhimu sana katika utetezi wa haki za binadamu.

Aidha, Olengurumwa alieleza kuwa hali ya sasa ya watetezi wanawake kwa sasa nchini imegubikwa na vikwazo mbalimbali, ikiwamo kutoaminiani miongoni mwao, kukosa umoja na mifumo kandamizi,

uwoga kutokana na changamoto za sasa za kiusalama na wengine kuingia katika nafasi walizonazo kama ajira pekee na kukosa hari na moyo wa utetezi.

Alisema kuna utofauti mkubwa kati ya utetezi wa kizazi cha kwanza na kizazi cha leo kwa madai kuwa watetezi wanawake wa awamu ya kwanza waliingia katika utetezi kama harakati na wengi wa watetezi wa leo wameingia katika utetezi kama ajira.

Licha ya vikwazo mbalimbali katika harakati za utetezi kwa wanawake na jamii kwa ujumla, alisema THRDC inaamini bado wanaweza kuhamasisha kundi hili muhimu kuongeza bidii, umoja, mshikamano na ujasiri katika utetezi wa haki hapa nchini.

# Chalamila ahamasisha wanawake kugombea

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewahamasisha wanawake kujitokeza na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba mwaka huu.

Chalamila alitoa hamasa hiyo juzi wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo kimkoa yalifanyika jijini Mbeya.

Alisema wanawake wanapoadhimisha siku yao, lazima waweke na mikakati ya namna ambavyo watashiriki kwenye nafasi za uongozi kuanzia udiwani ili kuchochea maendeleo na mabadiliko.

"Nawaomba wanawake tumieni vizuri nafasi zenu na ikibidi mhamasishane mkagombee uongozi hiyo itawasaidia kuaminika zaidi, lakini kupaza sauti zenu kwa pamoja ili kufikisha ujumbe," alisema.

Alisema serikali inatambua mchango wa mwanamke katika Taifa na ndio maana imewapa nafasi ya kuongoza sekta nyeti na wanafanya vizuri kuliko ilivyotarajiwa.

"Sikukuu ya Wanawake Duniani imebeba ajenda mbalimbali za maendeleo, lakini kubwa kwa sasa nchini ni uchaguzi mkuu ujao nawaomba kinamama mkagombee hizo nafasi acheni kubaki nyuma kama koti tunahitaji kupata 50/50 sasa sio porojo," alisema Chalamila.

Naibu Spika wa Bunge, Tulia Ackson, aliwaomba kinamama kuwa na umoja na kushirikiana, na kuwataka wajitokeze kuongea nafasi za uongozi.

Alisema wanawake ni jeshi kubwa na wana nguvu ya ushawishi, hivyo ni nafasi ya wao kuwaaminisha wanaume kuwa wanaweza katika masuala mbalimbali ukiwamo uongozi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Mkoa wa Mbeya, Stella Kategile, alisema katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani walikubaliana kuchanga shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya kinamama katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa.

Alisema lengo ni kuhakikisha huduma ya mama na mtoto katika hospitali hiyo inaboreshwa kwa kujengwa miundombinu rafiki ya kutolea huduma.



Mmoja wa wanufaika wa mpango wa Taifa wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), Nyambilila Nambukwa (71), ambaye ni mkazi wa Mtaa wa Pambogo, jijini Mbeya, akiwatoa nje kuku wake wa mayai kwa ajili ya kuwalisha nyumbani kwake, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Sababu vitendo ukatili kijinsia kupungua

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

MABARAZA na vikundi vya makuzi na malezi kwa watoto yametajwa kusaidia kupunguza kwa asilimia kubwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na udumavu kwa watoto katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Kauli hiyo imetolewa na Mwenyekiti wa kikundi cha Malezi ya watoto Nsalala, Otalo Kagoye, wakati anawasilisha taarifa ya utekelezaji wa baraza hilo la watoto katika Mji Mdogo wa Mbarizi Wilaya ya Mbeya.

Alisema mabaraza hayo tangu yaanzishwe yamesaidia kwa kiwango kikubwa kuwawezesha watoto katika shule za msingi kujua haki zao na kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii na kutoa taarifa katika ngazi za uongozi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Mbeya, Stella Kategile, alisema kuwa kama mkoa wanazingatia maelekezo ya serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kutekeleza mpango wa kudhibiti vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa mama na mtoto na kutoa elimu ya lishe kwa jamii nzima.

"Unajua mpango huu tangu uanze juu ya unatekelezaji wa makuzi kupitia mabaraza na vikundi vya makuzi na malezi kwa watoto vinavyoundwa ngazi ya jamii umekuwa ni msaada katika kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia," alisema Stella.

Stella alisema Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ni miongoni mwa halmashauri zinazotekeleza mpango huo mkoani Mbeya na kufanikiwa kudhibiti ukatili kwa watoto na wanawake ndani ya jamii pamoja na kupunguza hali ya udumavu kwa watoto.

Mwanafunzi wa Shule ye Msingi Nsalala, Lusia Amos, alisema kuwa baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo na na wa shule zingine wameanza kuwa na uelewa juu ya uwapo wa mabaraza hayo ya watoto ambayo yamewasaidia kujua haki zao.

Kwa upande wake Ofisa Maendeleo ya Jamii Ofisi ya Rais (Tamisemi), Hilda Mgomapaye, alisema maofisa maendeleo ya jamii ngazi ya mkoa, wilaya na kata ndiyo wamepewa jukumu la kuusimamia mpango huo kikamilifu kwa lengo la kuiwezesha jamii nzima kukabiliana na vitendo vya kikatili.

Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa nchini ambayo ipo kwenye kiwango kikubwa cha vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa mama na mtoto, na ni wazi kuwa uwepo wa mabaraza hayo na vikundi vya malezi vitasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza na kuongeza uelewa dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.





# Ukeketaji bado tatizo kwa jamii

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

UKEKETAJI umetajwa kuwa ni miongoni mwa vitu vinavyokwamisha jitihada za kupinga ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake kutokana na baadhi ya makabila kuendeleza vitendo hivyo.

Hayo yalibainishwa na wadau wa masuala ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto katika kikao cha mapendekezo ya wadau juu ya utekelezaji Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (Mtakuwwa), jijini hapa.

Akichangia katika kikao hicho, mdau kutoka Shirika lisilo la serikali la ATFGM kutoka mkoani Mara, Velerian Mgani, alisema suala la ukeketaji kwa wanawake na watoto linaendelea na kwamba mwaka jana kwenye mkoa huo kulikuwa na kesi 12 za ukeketaji zilizoripotiwa.

"Pia watoto 117 wilayani Tarime wamekimbia nyumbani kwao na kuishi kambini kwa kuhofia kufanyiwa ukatili huo kwa kukeketwa kilazima na wazazi wao," alisema.

Alisema mila na desturi wilayani Tarime ni kukeketa wanawake na watoto wa kike na hakuna sherehe kubwa kwa jamii ya Kikurya kama ya kukeketa au jando kwa wanaume. Alibainisha kwamba ikitokea mtu anapinga suala hilo, anauawa.

"Nina uchungu mkubwa mwaka jana aliuawa mwalimu wa shule ya Tarime huku wananchi wengine wakichomwa mishale na mikuki kwa sababu ya kuzuia na kupinga vikali wanawake na watoto wasikeketwe, lakini kwa wanaume kama atafanyiwa jando katika hospitali basi wenzake wakijua atafanyiwa tena katika jando la kimila," alisema Mgani.

Pia alisema Novemba hadi Desemba, mwaka jana, katika shirika lao walipokea watoto 557 kwa ajili ya kuwahifadhi baada ya kukimbia makazi yao kwa kuhofia kukeketwa.

Naye Mratibu wa mradi kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Zainabu Mmari, alisema hivi sasa wanashirikiana na zaidi ya asasi 30 katika kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Alisema malengo yao kama mtandao ni kuhakikisha hadi kufikia mwaka 2022 wawe wametokomeza ukatili kwa wanawake na watoto na kuboresha maisha yao.

# Mirembe yaonywa kuhusu rushwa

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Zainab Chaula, amewaonya watumishi wa Hospitali ya Mirembe kujiepusha na rushwa ili kutoa huduma sawa kwa wagonjwa.

Dk. Chaula alisema hayo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara hospitalini hapo ili kujadiliana namna ya kutatua changamoto walizo nazo katika maeneo yao ya kazi.

Alisema watumishi wa hospitali hiyo wakijiepusha na vitendo hivyo, watatenda haki na kutoa huduma sawa kwa wagonjwa wote katika maeneo yao.

Pia aliwataka watumishi hao kuhakikisha wanadumisha ushirikiano baina yao ili kuleta mabadiliko chanya katika utendaji kazi wao.

"Tunatakiwa kukaa pamoja na tutembee pamoja wakati wote ili kuleta mabadiliko katika hospitali na taasisi yetu. Tuache kulalamika maana sisi sote tulio hapa ndio serikali yenyewe," alisema Dk. Chaula.

Aliagiza uongozi wa hospitali hiyo kuwa wabunifu na kuhakikisha wanasimamia miradi yao vizuri hali itakayosaidia kuongeza makusanyo ya mapato na kuboresha huduma za afya.

"Hospitali inatakiwa iwe ya mfano, hivyo mnatakiwa kuongeza jitihada na ubunifu katika utendaji wenu, ikiwamo usimamizi mzuri wa miradi, tunataka kuona mabadiliko ili kuweza kusonga mbele," alisema.

Katibu Mkuu aliwataka pia watumishi katika hospitali hiyo kwenda katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kujifunza baadhi ya mbinu na ubunifu wanaoutumia katika kuendesha baadhi ya idara zao ili kuleta mabadiliko ya haraka ikiwamo ukusanyaji mapato.



Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaisha Moyo, akizungumza na walimu wa shule za awali wakati akifunga mafunzo ya walezi wa vituo vya kulelea watoto wadogo yaliyofanyika, jijini Dodoma wikiendi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mtendaji kizimbani tuhuma za mlungula

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

OFISA Mtendaji wa Mtaa wa Ausia Wilaya ya Kondoa, Saada Saidi (40), amefikishwa mahakamani kwa kupokea rushwa ya Sh.30,000 ili asichukue hatua kwa mtu asiyekuwa na choo.

Akizungumza na waandishi habari jana jijini hapa, Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema ofisa huyo amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kondoa baada ya kukamatwa akipokea rushwa kutoka kwa mtoa taarifa ambaye alitakiwa kuchukuliwa hatua kwa kutokuwa na choo.

Kibwengo alisema Takukuru pia imemfikisha mahakamani Ofisa Mifugo Mwandamizi wa Halmashauri wa Wilaya ya Kongwa, Nassoro Njarita (50), kwa tuhuma za kuomba rushwa ya Sh. 40,000 kutoka kwa mfanyabiashara wa bucha ili amruhusu kuuza nyama ambayo haijapimwa.

"Pia Mwenyekiti wa Kijiji cha Kinangali, Naftali Wami (56), amefikishwa kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 150,000 kutoka kwa mwananchi mmoja ili amruhusu kulima katika eneo lisiloruhusiwa," alisema.

Kadhalika, alisema taasisi hiyo imemfikisha mahakamani, Mkazi wa Mkonze, Benedict Mazengo (58) kwa mashtaka matatu ya matumizi mabaya ya mamlaka kinyume na kifungu cha Sheria Namba 31 na ubadhirifu kinyume cha kifungu cha namba 28 vyote vya Sheria Na 11 ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007.


"Pia anakabiliwa na kosa lingine la kusababisha hasara kata ya Ntyuka jijini Dodoma ya Sh. milioni 32.6 kinyume na Sheria ya Uhujumu Uchumi sura ya 200 marejeo ya 2002," alisema.

Mkuu huyo alisema katika uchunguzi wao kati ya Septemba, 2015 na Januari 2016 mtuhumiwa ambaye alikuwa mtendaji wa Kata ya Ntyuka alikusanya kiasi hicho cha fedha ikiwa ni ushuru wa madini ujenzi kutoka kwa wafanyabiashara kinyume cha sheria na taratibu bila kupeleka mapato benki.

Kibwego alidai kuwa washtakiwa hao wametenda makosa hayo kinyume na kifungu cha 15 (1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329 ya marejeo ya mwaka 2018.

Katika hatua nyingine, Takukuru imerejesha Sh. milioni 97.4 za vyama vya ushirika kutoka kwa wanachama 53 ambao walikuwa wakidaiwa kwa muda mrefu kwa Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo cha Mipango na Majengo mkoani Dodoma.

Alisema kazi ya kurejesha fedha hizo inaendelea na kuwataka viongozi na wanachama wote wanaodaiwa kulipa mapema kabla hawajachukuliwa hatua za kisheria.



# Wasimamizi ndoa, talaka wapewa somo

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Vuai Mwinyi Mohamed, amewataka wasimamizi wa ndoa na talaka wa mkoa huo kufanya kazi kwa kufuata kanuni na sheria.

Amesema kwa kutumia Sheria Na. 3 ya Mwaka 2018 ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, watajiepusha na matatizo yanayoweza kujitokeza wakati wa usajili wa ndoa katika maeneo yao.

Vuai aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa wasimamizi wa ndoa na talaka juu ya taratibu za usimamizi wa madaftari ya usajili wa ndoa na talaka katika Chuo cha Mafunzo ya Amali, Mkokotoni, Zanzibar.

Alisema usajili wa ndoa na talaka unaweza kutumika kupata takwimu sahihi pale serikali inapotaka kujua idadi ya wajane na wenye ndoa kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo.

"Usajili wa ndoa na talaka ni muhimu sana, hivyo niwasisitize wananchi kusajili ndoa na talaka katika sehemu husika ili kutambulika," alisema.

Pia aliwataka wasimamizi hao kuepuka kujaza madaftari ya ndao au talaka kinyume cha utaratibu na kuepuka kubadili taarifa katika cheti kama vile majina ya wanandoa na tarehe. Alisema kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha sheria hiyo.

Naye Naibu Mkurugenzi Mtendaji anayeshughulikia vizazi, vifo, ndoa na talaka, Shaaban Ramadhan Abdallah, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo watendaji hao ili kuweza kufanyakazi zao kwa ufanisi.

Alisema wananchi wanaposajili taarifa zao za vizazi, vifo na talaka kutawasaidia kuepukana na migogoro mbalimbali katika jamii ambayo inaweza kujitokeza ikiwamo mirathi.

"Endapo kuna ndoa itasajiliwa bahati mbaya, mmoja kati ya wanandoa hao akafariki dunia, watoto hawatadhulumiwa katika masuala ya mirathi na kupata haki zao," alisema.



Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, akizungumza katika mdahalo wa Siku ya Wanawake Duniani, uliofanyika mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Viongozi CCM waonywa kuwagawa wananchi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Magharibi, Mohammed Rajab Soud, amewataka viongozi wa majimbo kuendelea kutekeleza Ilani ya uchaguzi ya chama hicho na kuacha kuwagawa wananchi.

Amesema baadhi ya viongozi hawatekelezi majukumu yao na badala yake wanapita mitaani kupiga kampeni na kuwachafua wenzao.

Akizungumza katika mkutano wa kueleza utekelezaji wa ilani ya CCM kwa viongozi wa Jimbo la Pangawe juzi katika kiwanja cha Mpira Nyarugusu, alisema viongozi hao kupita mitaani kwa kupiga kampeni muda huu ni kinyume cha maadili ya uongozi na kuonya kuwa atakayebainika, jina lake halitarudishwa wakati atakapoomba ridhaa kwa mara nyingine.

Mohammed aliwataka wananchi watakaowabaini viongozi kwenda kinyume kupeleka taarifa sehemu husika ili wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Aidha, aliwataka viongozi hao kuendelea kuwatumikia wananchi na kuacha kupiga kampeni ili kujikinga na athari zinazoweza kujitokeza.

Sambamba na hilo, aliwakumbusha wananchi kuchagua viongozi wenye uchungu na nchi ambao watawaletea maendelo katika maeneo yao na kuacha ubabaishaji.

Kwa upande wao, viongozi wa Jimbo la Pangawe walisema tayari wameshatekeleza ilani kwa asilimia kubwa katika sekta mbalimbali zikiwamo maji, umeme, afya, barabara za ndani, vikundi vya vijana na wanawake.

# Bil. 3/- kujenga chuo cha ufundi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

ZAIDI ya Sh. bilioni tatu zinatarajiwa kutumika katika ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Amali (chuo cha ufundi) kilichoko Mwanakwerekwe Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Bakari Ali Silima, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika mahafali ya sita ya chuo hicho.

Alisema serikali imeazimia kuliongeza jengo hilo ili kupokea wanafunzi wengi na kuwafundisha fani mbalimbali kwa lengo la kuwaokoa vijana ambao wameshindwa kuendelea na masomo ya juu.

Dk. Silima alisema wanafunzi wengi wanahitaji kuwasaidia katika kubadilisha maisha yao hasa kwa kuwatafutia mbinu ambazo zitawafanya kuwa na uwezo wa kujiajiri baadaye.

Mkurugenzi huyo aliwataka wahitimu hao kujiajiri kupitia fani na ujuzi walioupata ili kuweza kujiajiri na kuajiri wengine kwa lengo la kujipatia kipato.

Alisema fani walizozisomea ni nguzo ya maisha yao kwa vijana hivyo ni vyema kuendeleza ujuzi wao ili kufikia lengo la kujiajiri na kuondoa umaskini.

Hata hivyo, alisema kuwa kufanikiwa kwa wahitimu hao ni kupitia jitihada za serikali kwa kuwaendeleza vijana na kuwanusuru katika janga la kujiingiza katika vitendo viovu ikiwamo utumiaji wa dawa za kulevya.

Naye Mkuu wa Chuo, Injinia Yussuf Suleiman, aliwataka vijana waliohitimu katika mafunzo hayo kujielewa kuwa wapo katika soko la ushindani wa ajira.

Akisoma risala kwa niaba ya wanafunzi wenzake Maryam Omar Yussuf, alisema masomo waliosomea ya fani mbalimbali yamewawezesha kuweza kujiajiri wenyewe na kupunguza utegemezi hasa katika familia.

Alisema watahakikisha wanawasaidia wengine kuona nao wanapata ujuzi na kuweza kujiajiri kupitia kazi za mikono na kuondoa dhana ya kusubiri ajira kutoka serikalini.

Jumla ya wanafunzi 89 wamehitimu masomo yao ya ufundi wakiwamo wanawake 35 na wanaume 53 na kutunukiwa vyeti vya fani mbalimbali ikiwamo fani ya ufundi seremala, uchongaji, ushoni, umeme, Tehama na ICT.

# Mimba shuleni zaitesa Morogoro

**Na Christina Haule, MOROGORO**

WIMBI la mimba kwa wanafunzi wa shule za sekondari na msingi mkoani Morogoro, limekua changamoto ambapo kwa mwaka 2018 /19 zaidi ya watoto 640 walishindwa kuendelea na masomo kwa sababu ya kupata ujauzito.

Hayo yamebainishwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Mohamedi Utaly, wakati akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kimkoa katika Kata ya Mzumbe wilayani Mvomero.

Alisema licha ya kuwapo kwa sheria mbalimbali za kuwalinda watoto wa kike ikiwamo kifungo cha miaka 30 jela kwa mtu atakayebainika kumpa ujauzito mwanafunzi, lakini changamoto ya ubakaji inaendelezwa bila woga.

Nao wazazi na wanafunzi walisema wanaamini upatikanaji wa mabweni ya kulala wanafunzi shuleni wanaotoka maeneo ya mbali utasaidia kwa namna moja au nyingine katika kupunguza changamoto ya ongezeko la mimba kwa wanafunzi mkoani hapa.

Rehema Omary, mkazi wa Mvomero, alisema, wanafunzi wanaishi mbali na shule ambapo wavulana wanaoendesha bodaboda wamekuwa wakiwadanganya kwa lifti, hivyo kuwasababishia mimba.

Prisca Geale ni mwalimu wa Shule ya Msingi Vikange na Juma Abdalah, mkazi wa Mzumbe anawahimiza wazazi nao kutambua kuwa wananafasi ya kuwaelimisha watoto wao madhara ya mimba za utotoni kwani kwa sasa wanafunzi hawana maadili bora, ambayo nayo pia inachangia katika suala hilo.

Siku ya Wanawake Duniani huadhimishishwa kila ifikapo Machi 8, ambapo mwaka huu kaulimbiu yake ilikuwa 'kizazi cha usawa kwa maendeleo ya Tanzania ya sasa na baadaye'.

# Shughuli za kilimo zaathiri barabara Pwani

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

WAKALA wa Barabara Tanzania (Tanroads) Mkoa wa Pwani umesema ongezeko la shughuli za kilimo kandokando ya mito hususan ndani ya Mto Rufiji, zinachangia kuzuia maji kupita na kukusanya mchanga katikati ya daraja, hivyo kusababisha hatari ya kukatika kwa barabara wakati wa mvua.

Hayo yalielezwa katika kikao cha bodi ya barabara kilichofanyika jana Mjini Kibaha na kuwahusisha wakuu wa Wilaya za Mkoa huo, wakurugenzi na wahandisi kutoka Tanroads na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura).

Akitoa taarifa ya mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2020/2021 wa Tanroads, Christina Nyamziga, Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango aliainisha changamoto hiyo kuwa imekuwa kikwazo kwa barabara kudumu kwa muda mrefu bila matengenezo.

Nyamziga alisema mbali ya kilimo pia ipo changamoto ya wizi wa samani za barabara, ongezeko la mifugo kwa baadhi ya maeneo ya mkoa huo pamoja na upatikanaji wa changarawe inayofaa kwa ujenzi.

"Changamoto nyingine ni kutopatikana kirahisi mtaalamu wa matengenezo wa mzani wa Vigwaza unaopima magari yakiwa yanatembea, wakati mwingine ukitokea uharibifu magari yote huingia kupima kwenye mizani, hali ambayo husababisha foleni na usumbufu kwa watumiaji wa barabara," alisema.

Nyamziga aliwasilisha taarifa ya mapendekezo ya Sh. milioni 973.820 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kutengeneza km 16.40, na Sh. milioni 1,755.930 kugharamia miradi ya serikali kuu kwa kutengeneza kilomita 25 za barabara za mkoa.

Alibainisha kuwa kiasi cha Sh. bilioni 4.9 kimelenga kugharamia miradi ya Serikali Kuu kwa kujenga kilomita 5.7 za barabara kuu.

Nyamziga alisema, katika bajeti ya mwaka 2019/2020, jumla ya shilingi bilioni 22.5 zilipangwa kutumika katika matengenezo mbalimbali ya barabara.

Alisema, hadi kufikia Desemba shilingi bilioni 8.7 zilipokelewa kwa ajili ya matengenezo ya barabara mbalimbali, ambapo shilingi bilioni 3.4 zimetumika kufanya matengenezo ya barabara kuu na za mkoa.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, alitoa rai kwa Tanroads na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) kuhakikisha wanasimamia barabara ziendane na thamani ya fedha zinazotolewa.



Mwendesha guta lililobeba mzigo mzito akisaidiwa na wasamaria wema kulisukuma wakati akitaka kuvuka barabara katika eneo la Sinza Mugabe, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali yaeleza umuhimu anuani za makazi

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

SERIKALI imesema kuwa mfumo wa anuani za makazi na postikodi ni moja ya nyenzo muhimu kwa maendeleo ya nchi kwa kuwa utaisaidia serikali kukusanya mapato kwa urahisi na kuimarisha hali ya ulinzi na usalama wa nchi.

Kauli hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, wakati akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuhusiana na umhimu wa anuani za makazi na postikodi.

Alisema serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya kushughulikia zoezi hilo kwa nchi nzima na kuwa litaanza katika ngazi ya taifa, mikoa, wilaya na kata na kuwa halmashauri zinapaswa kutoa ushirikiano ili kufanikisha zoezi hilo la anuani za makazi kwa ufanisi zaidi.

Alisema Mamlaka ya Mawasilino (TCRA) ilishamaliza kutengeneza postikodi nchi nzima na kuwa kilichobaki ni kutambua makazi ya wananchi nchi nzima ili kuwezesha kupewa anuani za makazi.

Naibu waziri huyo alisema mfumo wa anuani za makazi ni njia ya msingi ambayo inasaidia kubainisha na kutambua kitu mahususi kilichopo, kutambua eneo na kulipa anuani, majina ya barabara na nambali za nyumba.

Mhandisi Nditiye alisema mfumo huo ni mhimu sana kwa maendeleo ya nchi kwa kuwa unasaidia kukusanya mapato, kuimalisha ulinzi na usalama wa nchi na utazisaidia taasisi za kifedha kuwakopesha wananchi kwa urahisi zaidi.

Pia alisema hali ya mawasiliano ya simu kwa nchi nzima ipo katika kiwango kizuri na kuwa hali ya upatikanaji wa mfumo wa 3G ni nzuri na kuwa usambazaji wa mfumo wa mkonga wa taifa unaendelea vizuri.

Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, alisema Jiji limejipanga vyema katika zoezi hilo, na kuwa katika utekelezaji wake linatarajiwa litakuwa ni jiji la kwanza katika kuainisha anuani za makazi kutokana na umuhimu wa kukusanya mapato ya serikali.

Alisema miongoni mwa jitihada zilizofanywa ni kupitisha mwongozo wa mfumo wa anuani za makazi uteuzi wa timu ya wataalamu watakaosimamia zoezi hilo na kutenga bajeti juu ya utekelezaji wa zoezi hilo na kuandaa ramani za barabara katika jiji hilo.

HABARI KIMATAIFA

# Vifo vya corona Italia vyaongezeka

**ROME,** Italia

IDADI ya watu waliopoteza maisha kutokana na virusi vya corona nchini Italia kwa muda wa siku moja imeongezeka kutoka 133 na kufikia 366, maofisa wameeleza.

Maambukizi yameongezeka kwa asilimia 25 na kufikia 7,375 kutoka 5,883 kwa mujibu wa Shirika la Kitaifa la Utabiri na Udhibiti wa Matukio ya Dharura.

Ongezeko la maambukizi limekuja wakati mamilioni ya watu wakichukua hatua zilizotangazwa siku ya Jumapili ili kudhibiti maambukizi.

Watu takribani milioni 26 mjini Lombardy na katika majimbo 14 chini ya sheria mpya ya karantini wanahitaji ruhusa maalum kusafiri. Waziri Mkuu, Giuseppe Conte, ametangaza kufugwa kwa shule, maeneo ya kufanya mazoezi, makumbusho, nyumba za starehe na yale yenye mikusanyiko ya watu wengi.

**Baada ya Waziri Mkuu, Abdalla Hamdok kuunda serikali yake Septemba, mwaka jana aliahidi kuboresha hali ya wanawake licha ya ugumu wa kiuchumi.**

Mazuio hayo yatadumu kuanzia sasa hadi Aprili 3, mwaka huu.

Ongezeko hili linamaanisha kuwa Italia kwa sasa ina idadi kubwa iliyothibitishwa nje ya China, ambapo mlipuko ulianzia mwezi Desemba. Idadi hii imezidi Korea Kusini, ambayo ina idadi ya maambukizi 7,313.

Italia ni nchi mojawapo duniani yenye idadi kubwa ya watu wenye umri mkubwa na virusi hivyo ni hatari kwa wazee. Miongoni mwa watu waliopata maambukizi hivi karibuni ni Mkuu wa Jeshi, Salvatore Farina ambaye alisema alijitenga mwenyewe kuepuka kuambukiza wengine.

Taratibu mpya za karantini zinaathiri robo ya raia wa Italia na katikati mwa mji tajiri ulio kaskazini mwa nchi hiyo ambao ni chachu ya uchumi wa nchi hiyo.

Mfumo wa afya ni changamoto mjini Lombardy ambao upo Kaskazini mwa nchi hiyo yenye watu milioni 10.

"Tunataka kuhakikisha afya njema kwa raia wetu. Tunaelewa hatua hizi zinahitaji kujitoa, wakati mwingine kidogo wakati mwingine kujitoa kwa kiasi kikubwa,'" Waziri Mkuu Conte alisema wakati akitangaza hatua hizo mpya.

Chini ya hatua mpya, watu hawapaswi kuingia au kutoka Lombardy.

Hatua hizo zinachukuliwa Modena, Parma, Piacenza, Reggio Emilia, Rimini, Pesaro and Urbino, Alessandria, Asti, Novara, Verbano Cusio Ossola, Vercelli, Padua, Treviso and Venice.

Idara ya Mambo ya Uingereza imeshauri kutosafiri bila sababu ya lazima kuelekea maeneo hayo.

Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Tedros Ghebreyesus, aliisifu Italia kwa "kujitoa kwao kwa dhati" kwa kuweka mazuio.

Hadi juzi, karibu watu 50,000 waliopo Kaskazini mwa Italia waliathirika na karantini.

Juma lililopita serikali ilitangaza kufungwa kwa shule zote na vyuo nchi nzima kwa siku 10.

Idadi ya maambukizi ulimwenguni ni zaidi ya 107,000 na vifo vipatavyo 3,600.

Athari kubwa imeonekana China ingawa Jumapili iliripoti idadi ya chini zaidi ya maambukizi mapya katika siku moja tangu Januari.

Kwa upande wa Iran ni moja ya maeneo yenye maambukizi mabaya zaidi nje ya China ambapo sasa imethibitisha kuwa na maambukizi 6,566 na vifo 194.

Ripoti moja iliyotolewa Jumapili, ikinukuu mjumbe wa serikali, ilionyesha kulikuwa na vifo 200 katika mkoa wa Kaskazini wa Gilan pekee ingawa takwimu hizo baadaye ziliondolewa.

Juzi, Maofisa wa Ufaransa, walieleza virusi hivyo vimeenea miongoni mwa wabunge ambapo wawili walikutwa na maambukizi. **BBC**



Wahamiaji haramu wakijaribu kuvuka Bahari ya Aegean ambayo nchi ya Uturuki imeweka katazo kutovukwa na wahamiaji hao. **PICHA: MTANDAO**

## Waziri Mkuu wa Sudan anusurika kuuawa

**KHARTOUM,** Sudan

WAZIRI Mkuu wa Sudan, Abdullah Hamdok, amenusurika kuuawa baada ya msafara wake kulengwa kwenye Mji Mkuu Khartoum.

Televisheni ya taifa ya Sudan, ilitangaza kuwa Hamdok amepelekwa katika eneo salama.

Mkurugenzi katika ofisi ya Hamdok, Ali Bakhit, amethibitisha kuwa kiongozi huyo yuko salama.

Hakuna mtu au kundi lolote ambalo limedai kuhusika na jaribio hilo la mauaji.

Hamdok aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Sudan mwezi Agosti mwaka 2019, baada ya maandamano ya kudai demokrasia kulilazimisha jeshi kumwondoa madarakani kiongozi wa muda mrefu wa nchi hiyo, Omar al-Bashir na kukabidhi uongozi wa serikali kwa raia.

Karibu mwaka mmoja baada ya Bashir kuondolewa madarakani, Sudan inakabiliwa na mzozo wa kiuchumi. Kwa mujibu wa Shirika la Fedha Duniani, mfumuko wa bei umefika asilimia 60 na kiwango cha ukosefu wa ajira kwa mwaka 2019 kilikuwa asilimia 22.1. **DW**

## Ethiopia yatakiwa kurejesha huduma ya intaneti Oromia

**ADIS ABABA,** Ethiopia

SHIRIKA la Human Rights Watch limesema serikali ya Ethiopia inapaswa kurejesha huduma ya mtandao wa intaneti na mawasiliano ya simu katika eneo la Oromia.

Hatua hiyo imetatiza mawasiliano na shughuli za uokoaji maisha.

Tangu Januari 3, serikali ya Ethiopia imekatiza huduma hizo katika maeneo ya Kellem Wellega Magharibi mwa Oromia, Wellega Magharibi na Horo Gudru Wellega.

Katika eneo la Wellega Mashariki, wakazi waliripoti kuwa huduma za intaneti na mitandao ya kijamii zilikatizwa huku zile za kutuma ujumbe na kupiga simu zikipatikana katika miji mikubwa pekee.

Hatua ya kukatizwa kwa huduma hizo imetekelezwa katika maeneo yalioko chini ya udhibiti wa jeshi la serikali hiyo na inakuja wakati kukiwa na ripoti za operesheni za jeshi hilo dhidi ya kundi lililojihami ambalo wakati mmoja lilipigwa marufuku la Oromo Liberation Front (OLF).

Vyombo vya habari vimeripoti kwa uhakika kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu ikiwa ni pamoja na visa vya mauaji na vikosi vya serikali kuwashikilia watu wengi.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Shirika la Human Right Watch katika eneo la upembe mwa Afrika, Laetitia Bader, hatua ya serikali ya kukatiza mawasiliano kwa ujumla katika eneo la Oromia inasababisha madhara kwa raia wa eneo hilo na inapaswa kufutiliwa mbali mara moja. Laetitia alisema kuwa vikwazo hivyo vinaathiri vibaya huduma muhimu, habari kuhusu matukio muhimu na uchunguzi wa hali za binadamu na huenda ikachangia hali ya kibinadamu kuwa mbaya zaidi.

Shirika hilo limesema kuwa chini ya uongozi wa Waziri Mkuu, Abiy Ahmed, kukatizwa kwa mawasiliano bila sababu kumekuwa jambo la kawaida wakati wa ghasia za kijamii na kisiasa.

Shirika hilo limesema kuwa sheria ya kimataifa ya haki za binadamu, inalinda haki ya watu ya kutafuta, kupata na kutoa habari na maoni kupitia mifumo yote ya habari ikiwa ni pamoja na intaneti kwa njia huru.

Mashirika manne ya msaada yanayofanya shughuli zao katika maeneo yalioathirika, yameliambia Shirika la Human Rights Watch kuwa shughuli zao zimetatizwa kwa kiwango kikubwa kwa sababu hayawezi kupokea habari muhimu kuhusu hali ya usalama na kibinadamu.

Kwa mujibu wa ofisa mmoja wa msaada, huduma za afya pia zimeathirika huku madaktari na wahudumu wa magari ya kubeba wagonjwa wakishindwa kuwasiliana na wagonjwa.

Mnamo mwezi Agosti, Abiy aliwaambia waandishi wa habari kwamba atakatiza kabisa huduma za intaneti iwapo vurugu zilizosababisha mauaji zilizochochewa kupitia mitandao ya kijamii zingeendelea na kusema kuwa huduma za intaneti sio maji au hewa hivyo basi sio muhimu. **DW**

# Ndalichako ataka sheria itumike wanaokatisha ndoto wanafunzi

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amesema utekelezaji wa sheria ya adhabu kwa wanaokatisha ndoto za wanafunzi wa kike kupata elimu kwa kuwapa mimba haujafanikiwa.

Akiwa wilayani Kasulu mkoani Kigoma, Waziri Ndalichako alisema sheria ya adhabu kali ya miaka 30 jela dhidi ya watu wanao watamani wanafunzi kuwaoa au kuwapa mimba haitekelezeki ipasavyo kutokana na wazazi kuwakataza watoto wao kutoa ushirikiano kwa vyombo vya usalama.

"Serikali imeshaweka sheria kali, kazi yenu wananchi ni kushirikiana na serikali ili watu hao washughulikiwe sawasawa," alisema.

Ndalichako alisema lazima kila mwananchi hausike kukomesha vitendo hivyo ili kuwezesha kufikia usawa wa kijinsia kati ya mwanamke na mwanaume.

Dolla Mchomvu, mkazi wa Kigoma, alisema miongoni mwa sababu zinazofanya wazazi washindwe kutoa ushirikiano ni mila na desturi kwa kuwa wanaamini watoto wao wataolewa na waliowapa mimba.

Pia wazazi kuona watakapofungwa watabaki na mzigo wa kulea watoto hao na gharama za malezi. Naye mwalimu Selina Makabe, Mwenyekiti Jumuiya ya Wanawake Mkoa wa Kigoma, alisema miongoni mwa sababu zinazochangia watoto wa kike kukatishwa ndoto zao ni kukosa mabweni na kulazimika kupanga mitaani.

"Kumekuwa na shida sana kwa wasichana hawa kutokana na kipato kidogo cha familia zao hivyo wanajikuta wameangukia kwa watu wabaya," alisema.



Mkuu wa Rasilimali Watu wa Benki ya Stanbic, Eutropia Vegula, akikata utepe kuzindua chumba kwa ajili ya kunyonyesha kiitwacho "Stanbabies" ikiwa ni sehemu ya benki hiyo kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, katika ofisi ya makao makuu ya benki hiyo, Dar es Salaam. Chumba hicho kitatumika na wafanyakazi wanaonyonyesha wa benki hiyo wanapokuwa kazini. Anayeshuhudia ni Mkuu wa Biashara na Uwekezaji wa Benki hiyo, Manzi Rwegasira. **NA MPIGAPICHA WETU.**

## Mtuhumiwa ujambazi akamatwa na silaha

**Na Mary Geofrey**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linamshikilia mtuhumiwa wa ujambazi baada ya kukamatwa na silaha moja ya kivita aina ya AK47 yenye namba 1952 TPB 3954 na risasi tatu ndani ya kasha.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema mtuhumiwa huyo anafahamika kwa jina la Boniface Nicodemus (37) maarufu kwa jina la Mapunda, mkazi wa Vikindu mkoani Pwani.

Mambosasa alisema Nicodemus alikamatwa Machi 7, mwaka huu, saa 5:00 asubuhi, maeneo ya Majohe, Pugu jijini Dar es Salaam.

"Alikamatwa na kwenda kuwaonyesha askari alikoficha silaha hiyo huko maeneo ya Vianzi, Mkoa wa Kipolisi Rufiji ambayo amekuwa akiitumia kufanya uhalifu maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam na Pwani," alisema Mambosasa.

Alisema jeshi hilo linaendelea kuwasaka watuhumiwa wengine walioshirikiana naye katika uhalifu huo na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

**Alikamatwa na kwenda kuwaonyesha askari alikoficha silaha hiyo huko maeneo ya Vianzi, Mkoa wa Kipolisi Rufiji ambayo amekuwa akiitumia kufanya uhalifu maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam na Pwani.**

## Jela miaka 5 wizi mil. 45.3/-

**Na Beatrice Shayo**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kibaha mkoani Pwani, imemhukumu aliyekuwa meneja wa kituo cha kuuza mafuta cha Ukodi, Malima Charles (40), kifungo cha miaka mitano baada ya kumkuta na hatia ya kuvunja ofisi na kuiba Sh. milioni 45.3

Akisoma hukumu hiyo jana, Mkazi wa Mahakama hiyo, Joyce Mushi, alisema ameridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande zote na kwamba anatoa adhabu hiyo iwe fundisho kwa watumishi wengine wanaopewa dhamana ya kusimamia vituo vya mafuta. Mtuhumiwa huyo alikutwa na hatia kwa makosa ya mawili la kuvunja ofisi na kuiba.

Mwendesha mashtaka, Wakili wa Serikali Auleilia Mushi, alieleza mahakama kuwa mtuhumiwa akiwa meneja wa kituo cha kuuza mafuta cha Ukodi, alikula njama za kuvunja ofisi na kuiba Sh. 45,266,133 za mwajiri wake na kutoweka kusikojulikana, akijua fika kufanya hivyo ni kosa kisheria.

## Mshtakiwa mauaji ya mke atoa mpya tena mahakamani

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imepiga kalenda kesi ya mauaji ya Naomi Marijani inayomkabili Hamisi Luwongo, baada ya Jamhuri kudai kuwa upelelezi wake bado haujakamilika.

Hata hivyo, mshtakiwa alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rashidi Chaungu kwamba anaomba kibali cha kuonana na Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Godfrey Isaya, kwa ajili ya kuzungumza naye shida zake.

Hakimu Chaungu alimhoji mshtakiwa ana shida gani, lakini alisisitiza kuruhusiwa kumwona mfawidhi ambaye baada ya kesi yake kutajwa aliruhusiwa kwenda kumwona.

Kesi hiyo ilipangwa jana kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Salum Ally lakini kwa sababu ni mgonjwa, iliahirishwa na Hakimu Chaungu.

Hakimu Chaungu alisema kesi hiyo itatajwa tena Machi 23, mwaka huu, na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Awali, Wakili wa Serikali Janeth Magoha alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, hivyo kuiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Katika kesi ya msingi, mfanyabiashara huyo anakabiliwa na kesi ya kumuua mke wake, Mei 15, mwaka jana, katika eneo la Gezaulole, Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTEA KWA CHETI



**Brenda J. Chaggu** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0248-0016** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Marian Girls..Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/MAG/RB/209157/2020**

115660802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA MUUNGANO WA TANZANIA**

## HATI YA KIAPO

Mimi **HAMISI MOHAMEDI AMOUR** wa S.L.P 178-TANGA, Muslim mtu mzima nikiwa na akili zangu timamu nimefika Mahakamani na kutamka yafuatayo.

1. **Kwamba** mimi **HAMISI MOHAMEDI AMOUR** ni mkazi wa jiji la Tanga.
2. **Kwamba,** nimepoteza hati ya nyumba namba 05 KITALU 156 NGAMIANI, nimeitafuta bila mafanikio na nimekwenda polisi na kutoa taarifa na kupata RB NO TAN/RB/213396/2020 ERV NO. 9910811997551.
3. **Kwamba** kwa kiapo hiki naziomba ofisi za Mipango Miji katika jiji la Tanga wanipatie hati nyengine.

**UTHIBITISHO:** Nathibitisha kwamba maelezo niliyoyaeleza hapo juu ni ya kweli kweli tupu kadri nijuavyo kwa sheria za viapo na kwa uthibitisho zaidi nimefika Mbele ya Hakimu/Wakili na kutia sahihi yangu

HAMISI MOHAMEDI AMOUR

Leo ........
Mbele yangu ........
Cheo ........
Anuani ........
Sahihi ........

HAKIMU

HAMISI MOHAMEDI AMOUR

115661102

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.13 OF 2020**

**In the matter of the Estate of the late PAUL PAUL HAULE of VEYULA Area within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY BENARD PAUL MTUMBIKA**

## GENERAL CITATION

***(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 163)***

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 5th day of APRIL, 2020.

Date at Dodoma this 17th day of February 2020

RESIDENT MAGISTRATE

215661002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA LILILOKO IRINGA**

**MAOMBI NA 144 YA MWAKA 2019**

**ANDREA MWANDIMBILE .......MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**DOMONICUS KIHONGOSI......WAJIBU MAOMBI ALFREDULIPO**

## WITO WA KUITWA SHAURINI

**KWA,**
**ALFRED MTENGA**
**POPOTE ULIPO**

Fahamu kwamba ANDREA MWANDIMBILE amefungua shauri katika baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya dhidi yako Shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 23/03/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya mheshimiwa A.J.Majengo Mwenyekiti wa baraza

Hivyo unaamriwa kuhudhuria binafsi au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa,ambapo nyaraka zote zihusuzo shauri hilo utazikuta kwenye masijala ya baraza Ofisi za Baraza zilizopo mtaa wa Mahiwa, Kata ya Makorongoni Barabara ya kwenda Pwaga mkabala na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa

Imetolewa na mkono wangu na mhuri /lakiri wa Baraza leo hii tarehe 09/03/2020

A.J.MAJENGO
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA IRINGA.

215662202


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# GUARDIOLA HANA TATIZO NA MAKOSA YA EDERSON

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amemtetea Ederson kama golikipa wa aina yake baada ya nyota huyo wa Brazil kufanya makosa yaliyosababisha Manchester City kuchezea kichapo cha 2-0 kutoka kwa Manchester United.

Baada ya City kutawala mpira katika dakika za awali, Anthony Martial alitumia makosa ya Ederson kuiweka mbele United.

Ederson pia makosa yake tena nusura yamzawadie Martial bao la pili, lakini akawahi kuokoa na Scott McTominay akapiga bao la pili dakika za majeruhi.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Guardiola alisema Ederson ni golikipa wa aina yake licha ya kufanya makosa kwenye mchezo huo.

"Aliokoa mara moja au mara mbili... ni golikipa wa aina yake," alisema Guardiola akiiambia Sky Sports baada ya kipigo hicho cha tatu kutoka kwa wapinzani wao hao wa jiji moja msimu huu.

"Sijaja hapa kuwahukumu wachezaji wangu kama wamefanya makosa. Ni sehemu ya mchezo.

"Atarudi kwenye hali yake ya kawaida, kwani yeye ni golikipa wa aina yake katika nafasi hiyo."

# Lampard: Bado sijaridhika na kiwango

**LONDON,** England

FRANK Lampard bado hajaridhika na kiwango cha timu yake ya Chelsea licha ya kuifumua Everton 4-0 pale kwenye dimba la Stamford Bridge, Jumapili.

Carlo Ancelotti aliiongoza Chelsea kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England na Kombe la FA wakati akiwa kocha pale London kwa kipindi cha miaka miwili, wakati huo Lampard alikuwa mmoja wa wachezaji wake, lakini alijikuta akichezea kichapo kutoka kwa mwanafunzi wake Jumapili.

Mason Mount na Pedro walifunga kipindi cha kwanza, kabla ya Willian na Olivier Giroud kila moja kufunga bao moja, ndani ya dakika tatu za kipindi cha pili.

Wakiwa wametoka kushinda 2-0 kwenye mchezo wa Kombe la FA raundi ya tano dhidi ya Liverpool, Chelsea imeshinda mechi mbili tu kati ya nane zilizopita kwenye mashindano yote.

Licha ya kiwango hicho kilichoonyeshwa na Blues hao, Lampard bado hajaridhishwa na timu yake kama itaendelea kuwa na matokeo hayo hadi mwisho wa msimu.

"Nahofia kusema hivyo. Kiwango cha mechi mbili zilizopita kinaonekana kuwa hivyo, lakini nina uzoefu wakutosha kwamba, tunakwenda ugenini kucheza na Aston Villa, timu ambayo inapigana kupata matokeo," alisema Lampard.

"Ndio, tulikuwa na mwanzo mzuri msimu huu. Lakini hivi karibuni hatukuwa na mwendelezo mzuri."





# *Sarri amsifia Ramsey kuimarika*

**TURIN,** Italia

MAURIZIO Sarri amesifia kiwango cha Aaron Ramsey wakati Juventus ikiibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Inter Milan, akisema mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales ameimarika na kuwa fiti zaidi.

Ramsey alifunga kwa mara ya pili kwenye mchezo wa Serie A, mara ya kwanza akifunga dhidi ya SPAL.

Katika mchezo huo pia alitengeneza bao la pili la Paulo Dybala na Sarri amesema kumchezesha Ramsey katika nafasi ya viungo watatu kumekuwa na matokeo mazuri zaidi kuliko kumchezesha nyuma ya washambuliaji.

"Yeye (Ramsey) anaonyesha kwamba anahitaji kupata nafasi zaidi ya kucheza katikati ya uwanja," alisema kocha huyo wa Juve. "Anafanya vizuri kwenye nafasi yake, na kwa sasa yupo fiti zaidi kimwili tofauti na mwanzo na anaonekana kuimarika na kuwa fiti zaidi.

"Inter Milan ilijaribu kutupa presha kubwa kipindi cha kwanza na pengine walitumia nguvu nyingi kwa kufanya vile. Katikati ya mchezo mambo yakabadilika na tukapata bao."

# Liverpool wamtaka Werner, wamtoe kwa mkopo

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imeripotiwa kwamba wana mpango wa kumsajili Timo Werner na kumrudisha kwa mkopo katika klabu yake RB Leipzig mwishoni mwa msimu huu.

Werner mwenye umri wa miaka 24, amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na vinara hao wa Ligi Kuu England baada ya fowadi huyo kuwa na kiwango cha kuvutia kwa miamba hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Lakini kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani atasajiliwa pale Liverpool kwa ajili ya msimu wa 2020-21, hatakuwa kwenye mipango yao ya awali.

Liverpool wanaweza kumrudisha kwa mkopo Werner kule RB Leipzig kwa ajili ya msimu ujao kama watafanikiwa kuipata saini yake, kwa mujibu wa gazeti la Bild.

Werner amefunga mabao 27 katika mechi 35 alizocheza msimu huu, amekuwa akiwaniwa na klabu kadhaa za Ulaya.

Mjerumani huyo ambaye ameichezea timu yake ya taifa jumla ya mechi 29 alisema mwezi uliopita kwamba, anajisikia fahari kutakiwa na Liverpool.





# SOLSKJAER: NAJIVUNIA KUINOA UNITED HII

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer ameelezea kama "anajivunia" kuwa kocha wa Manchester United baada ya kuishuhudia timu yake ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye mchezo wa 'dabi' dhidi ya Manchester City.

Mashetani Wekundu hao walizima kabisa ndoto za City kuwa kwenye mbio za kutetea ubingwa wake msimu huu pale kwenye dimba la Old Trafford kwa mabao kutoka kwa Anthony Martial na Scott McTominay na kuendelea kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

United walikuwa wakiongoza kwa kipindi cha kwanza baada ya bao la Martial, huku la pili likifungwa na McTominay zikiwa zimesalia sekunde chache mpira kumalizika.

Akizungumza na Sky Sports baada ya mchezo huo wa Jumapili, Solskjaer hakusita kuwasifia wachezaji wake, ingawa alisema wanahitaji kuimarika zaidi.

"Kujituma, ari pamoja na hamasa ya wachezaji ilichangia ushindi. Siku nzuri tuliyokuwa nayo leo (juzi) ni kwa sababu ya wote, wachezaji na mashabiki," alisema.

"Bila shaka walitufanya tuwe imara - mashabiki wetu walionesha hamasa kubwa na kuwapa molari wachezaji wetu. Tumefanya kazi yetu."

# *Casemiro: Kipigo kitaigharimu Madrid LaLiga*

**MADRID,** Hispania

CASEMIRO amebainisha kupoteza kwa Real Madrid dhidi ya Real Betis kunaweza kuwagharimu kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Madrid walinyukwa mabao 2-1 Jumapili, na kuwaacha wakiwa nafasi ya pili dhidi ya wapinzani wao wa soka la Hispania, Barcelona kwenye msimamo, huku zikiwa zimesalia mechi 11 msimu kumalizika.

Casemiro amesema matokeo hayo yanaweza kuwaweka kwenye wakati mgumu Madrid kwenye mbio za ubingwa dhidi ya Barca ambao wanaongoza ligi kwa tofauti ya pointi mbili.

"Walikuwa wakali na walicheza vizuri, hakuna cha kujitetea, soka ni mchezo rahisi," alisema kiungo huyo kupitia tovuti ya klabu yao.

"Kwenye LaLiga kila mchezo ni mgumu. Kushinda LaLiga tunatakiwa kucheza vizuri kila mchezo na hatukucheza vizuri. "Tunatakiwa kujituma kwa bidii, hatukucheza kwa kiwango kizuri na hatukucheza kama tulivyocheza dhidi ya Barcelona.

"Sisi ni binadamu pia, lakini inaweza kutugharimu kwenye ligi. Sasa tunatakiwa kutumia nguvu zetu vizuri kwenye mchezo ujao dhidi ya Eibar."

Wakati bao la penalti la Karim Benzema likisawazisha lile la Sidnei la kipindi cha kwanza, Cristian Tello alifunga dakika ya 82 la ushindi kwa Betis.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MALEN AKARIBIA KUREJEA ARSENAL

●●● Kocha Arteta afikiria straika huyo ataku-wa mrithi wa Aubameyang ambaye anajiandaa...

**LONDON,** England

KATIKA kuhakikisha msimu ujao inakuwa na kikosi imara, Arsenal 'inajiandaa kufanya mchakato' wa kumrejesha kwenye kikosi chake straika wa PSV Eindhoven, Donyell Malen kwa lengo la kuziba pengo litakaloachwa na Pierre-Emerick Aubameyang.

**Nyota huyo wa kimataifa wa Holland, ambaye ana umri wa miaka 21, alilelewa kwenye kituo cha Arsenal kwa miaka miwili, kuanzia mwaka 2015 hadi 2017, na aliichezea The Gunners mechi kadhaa katika msimu iliyopita.**

Lakini Arsenal ilimuuza Malen kwa klabu hiyo ya Uholanzi (PSV) kwa dau la pauni 500,000 na tangu alipojiunga na klabu hiyo ameonyesha kiwango kizuri katika ligi ya nchi hiyo maarufu Eredivisie.

Malen amefunga mabao 17 na ameshiriki katika kutengeneza nafasi nyingine tisa za magoli katika mashindano mbalimbali aliyoichezea PSV msimu huu.

Kwa mujibu wa gazeti la michezo la Le 10 Sport la Ufaransa, limeandika baada la Malen 'kuivuruga' Arsenal, klabu hiyo italazimika kutoa pauni milioni 48 ili kukamilisha mchakato wa kumrejesha kwenye Uwanja wa Emirates nyota huyo.

Arsenal itatakiwa kupata mshambuliaji mpya wa kati kama kinara wake wa kupachika mabao Aubameyang ataondoka katika kipindi cha majira ya joto, baada ya Barcelona na Inter Milan kuvutiwa naye kufuatia ubora aliouonyesha kwa kufunga mabao 20 msimu huu.

Kocha Mikel Arteta alisema anataka kuona Aubameyang anabakia klabuni hapo, lakini kwa sababu mkataba wa mshambuliaji huyo unatarajiwa kumalizika majira ya joto mwakani, huu ndio wakati mzuri wa kumuuza na klabu kupata faida.

Katika mahojiano yaliyofanyika mwaka jana, Malen alisema uamuzi wa kuondoka Arsenal ulikuwa ni kupata nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha kwanza na si kwa sababu hakuwa fiti. Aliliambia gazeti la Uholanzi liitwalo De Telegraaf: "Sababu inayozungumzwa ambayo ilinifanya niondoke Arsenal si sahihi. Bado nina mkataba na Arsenal wa mwaka mmoja na hata kama wanataka kuongeza. Sichezi mpira kwa ajili ya pesa pekee. Sijawahi kufanya hivyo. La sivyo ningefikia uamuzi wa kuondoka England.

"Kuna taarifa kuwa sikua fiti wakati nilipojiunga na Arsenal. Lakini sikuwahi kuwa mnene pia, huo ndio kweli na nyingine ni habari za kupuuzwa.

**Wakati huo huo**, Manchester United inaamini itaibuka mshindi katika kumshawishi mshambuliaji wake Tahith Chong (20), kusaini mkataba mrefu na klabu hiyo.

Inaelezwa kuwa Chong anaweza kuondoka Old Trafford, baada ya Inter Milan, Juventus na Barcelona kutajwa kuwania saini ya mshambuliaji huyo.

Chong alijiunga na United akitokea kwenye akademi ya Feyenoord mwaka 2016.

Kama Chong atakubali kusaini mkataba mpya, inamaana kwamba United itaendelea kuzungukwa na wachezaji vijana baada ya Brandon Williams na Mason Greenwood kufanya vema msimu huu na kusaini mikataba mipya.

## ZISIKUPITE

### ARRIZABALAGA AWINDWA

REAL Madrid imejiandaa kumsajili golikipa wa Chelsea Mhispania Kepa Arrizabalaga (25), katika majira ya joto, huku the Blues ikionekana kuvutiwa na golikipa wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Marc-Andre ter Stegen na mlinda mlango aliyeko kwa mkopo Manchester United, Dean Henderson (22). ***(Star)***

### DE BRUYNE KUBAKIA CITY

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anajipanga kumbakisha kiungo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Kevin de Bruyne (28), kwa kumpa mkataba mpya ambao utamfanya alipwe mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki. ***(Express)***

### HENDERSON AFUNGUKA

GOLIKIPA wa Dean Henderson (22), amewaambia wachezaji wenzake wa Sheffield United kuwa atarejea klabuni hapo kwa mkopo katika msimu ujao kama ataendelea kukosa namba katika kikosi cha Manchester United. ***(Mail)***

### CAN AINGIA MTEGONI

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Emre Can (26), amesema amepata ofa ya kujiunga na Manchester United, lakini kama mchezaji wa zamani wa Liverpool, "hawezi kufikiria kwa mara ya pili". Kwa sasa Can yuko kwa mkopo Borussia Dortmund akitokea Juventus. ***(Kicker - in German)***

### GALLAGHER ANUKIA UHOLANZI

KIUNGO wa Chelsea ambaye ni raia wa England, Conor Gallagher (20), na yuko kwa mkopo Swansea, anawindwa na Vitesse Arnhem ya Uholanzi. ***(Sun)***

### CHONG AGOMBEWA ULAYA

MANCHESTER United inaamini itafanikiwa kumshawishi winga wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Tahith Chong (20), kubakia klabuni hapo licha ya Barcelona, Inter na Juventus kuonyesha nia ya kuhitaji huduma yake. ***(Sun)***

### BARISIC KUTUA SPURS

TOTTENHAM inajiandaa kusajili beki wa kushoto katika majira ya joto na tayari imeanza mchakato wa kuwania saini ya nyota wa Timu ya Taifa ya Croatia, Borna Barisic (27), ambaye anaichezea Rangers. ***(90 Min)***

### UNITED KUSAJILI WATATU

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer amesema Manchester United bado inahitaji kusajili "nyota wawili au watatu" wapya ili kurejea kwenye mbio za ubingwa huku ikiwa imefanikiwa kuifunga Manchester City mara mbili kwa mara ya kwanza ndani ya miaka 10. ***(ESPN)***

### GIROUD ALIKWAMISHWA

STRAIKA wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud (33), amebainisha alizuiwa kujiunga na watani zao Tottenham katika dirisha dogo la Januari. Giroud ameweka wazi pia akitarajia kujiunga na Inter katika kipindi hiko. ***(90 Min)***

### AUBAMEYANG: NINAFURAHA

STRAIKA wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang (30), ambaye ameendelea kuhusishwa na mpango wa kuondoka klabuni hapo amesema ana "furaha" kubakia hapo Emirates. ***(Mirror)***

## Mtibwa Sugar, Polisi hapatoshi

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila amesema kikosi chake 'kimeamka' na kimerejea kwenye makali yake ya kutoa 'dozi' katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo ziko kwenye hatua ya lala salama.

Mtibwa Sugar leo itakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi kuwakabili wenyeji wao Polisi Tanzania, ikiwa na kumbukumbu ya kushinda mechi zake mbili zilizopita.

"Ninashukuru timu yangu imebadilika na wachezaji wanaendelea kujituma, sasa hivi timu yangu imeanza kuwa sawa, mapungufu yote tumeyafanyia kazi na ninaendelea kuyafanyia kazi," alisema. Katwila ambaye yuko Moshi tangu juzi.

Alizungumzia mchezo wake wa leo dhidi ya timu ya Polisi Tanzania kuwa maandalizi yake yamekamilika na kudai hali ya kila mchezaji ipo vizuri.

"Ninajua mchezo dhidi ya Polisi utakuwa mgumu, kwa kuwa kila timu inataka pointi tatu na lengo letu tumepanga kurudi na ushindi kwetu," Katwila alisema.

Mechi nyingine za Ligi Kuu zitakazochezwa leo ni kati ya Azam dhidi ya Ruvu Shooting, Mbeya City wakaikaribisha Mbao, Coastal Union watawakabili Lipuli wakati Biashara United itawafuata Namungo FC.

## Mlandege, Selem View majaribuni

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

ILI kujiweka katika nafasi nzuri ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, uongozi wa Mlandege FC umesema timu yao itapambana kuhakikisha itaibuka na pointi tatu muhimu kwenye mchezo wa leo dhidi ya Selem View utakaochezwa katika Uwanja wa Gombani, Pemba.

Mwenyekiti wa timu hiyo, Mbaraka Himidi alisema kikosi chenye wachezaji 20 kilitua salama Pemba na leo kimedhamiria kupata ushindi katika mchezo huo na kuendeleza wimbi la ushindi.

Himidi alisema wanafahamu mechi zote zina ushindani, lakini wao wako tayari kupambana na kupata matokeo pointi tatu katika mchezo huo, ingawa wanafahamu lolote linaweza kutokea.

"Kikosi chetu kimejiandaa kushinda, ingawa lolote linaweza kutokea, hususani katika kipindi hiki cha kuelekea kumaliza msimu, kila timu inataka kufanya vizuri hususani zile timu ambazo zipo katika mstari wa hatari wa kushuka daraja lakini na sisi tutapambana," alisema.

Mlandege ambayo imecheza mechi 17, ipo katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na pointi 35, wakati Selem View yenyewe ikiwa na pointi 17 baada ya kushuka uwanjani mara 16.

# MASHABIKI SIMBA, YANGA SC WAJITOKEZA KUCHANGIA DAMU

**Na Mary Geofrey**

MASHABIKI 203 wa Simba na Yanga walijitokeza kuchangia damu katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI) kwa ajili ya kuokoa maisha ya majeruhi wa ajali wanaotibiwa katika hospitali hiyo, imefahamika.

**Idadi hiyo, ilijitokeza kutokana na ahadi iliyotolewa na mfanyabiashara maarufu nchini, Azim Dewji ya kuwapatia mashabiki 300 tiketi za bure ili kwenda kushuhudia mchezo huo uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza jijini jana, Ofisa Habari wa MOI, Patrick Mvungi, alisema mashabiki wa timu hizo walijitokeza kuchangia damu na hivyo kufanikisha kukusanya chupa 187.

Mvungi alisema idadi ya chupa za damu walizokusanya zitawasaidia kuokoa maisha ya majeruhi wa ajali na wagonjwa wengine wanaohitaji huduma hiyo.

"Idadi hii ya mashabiki wa timu za watani wa jadi, Simba na Yanga iliyojitokeza, ilitokana na tangazo lilitoka siku ya Alhamisi, ambalo lilitaka mashabiki 300 kujitokeza kuchangia damu MOI Ijumaa na Jumamosi watapata tiketi bure," alisema Mvungi.

Mvungi alisema MOI inatoa shukrani za dhati kwa Dewji, ambaye alitoa tiketi hizo 300 pamoja na kuhamasisha watu kuchangia damu.

"Kwa namna ya pekee tunatoa shukrani za dhati kwa Dewji, tulimweleza changamoto tuliyonayo na alikua mstari wa mbele kushirikiana nasi na amekua akishirikiana nasi kwenye mambo mengi, na tunaendelea kumuomba aendelee kuwa na moyo huo huo wa kusaidia jamii," alisema Mvungi.

Alitoa wito kwa watu binafsi, mashirika, vikundi na asasi kufika MOI kuchangia damu kwa sababu hakuna kiwanda cha damu bali lazima damu itoke kwa binadamu iende kwa mgonjwa.

Katika mtanange huo wa watani wa jadi ambao ulishuhudiwa na Rais John Magufuli na Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Ahmad Ahmad, ulimalizika kwa Yanga kupata ushindi wa bao 1-0.



Mshambuliaji wa Simba, Luis Miquissone (kushoto) akijiandaa kumtoka kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Feitoto', katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam. Yanga ilishinda 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Swahili-Flix yambeba Mwakinyo*

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha Watanzania wanapata nafasi ya kumshuhudia bondia, Hassan Mwakinyo akipigana na Mjerumani Jack Culcay, kupitia mtandao wa Swahili Flix, imeelezwa.

Mwakinyo (pichani) atapigana na Culcay kuwania mkanda wa WBO Super Welter Weight katika pambano litakalofanyika Machi 21, mwaka huu.



Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Mwakinyo, Jay Msangi, alisema mchakato wa kuonyesha pambano hilo umelenga kuwapa burudani Watanzania na vile vile kumwombea dua bondia huyo apate ushindi.

Msangi alisema Mwakinyo ambaye ana umri wa miaka 24, na anashika nafasi ya kwanza kwenye uzito wa Super Welter, atakuwa ni bondia wa kwanza Mtanzania kugombea mkanda huo ambao ni wa pili kwa ukubwa duniani baada ya ule unaotambuliwa na WBO.

"Pambano hili litakuwa na ushindani kwa sababu mabondia wote ni wazuri, Culcay (34), amewahi kushinda medali za dhahabu katika mashindano ya ngumi za dunia, medali ya shaba katika Michezo ya Olimpiki na kujikuta akipatiwa jina la Golden Jack na Wajerumani," alisema Msangi.

Aliongeza Culcay ameweza kutetea mkanda huo anaoushikilia mara moja dhidi ya Mjerumani mwenzake, Jama Saidi na endapo akifanikiwa kuutetea kwa mara ya pili, atakuwa amejiweka kwenye nafasi ya kugombea mkanda wa dunia ambao umewahi kushikiliwa na Manny Paquiao.

Mwakinyo atapanda ulingoni akiwa na rekodi ya kushinda mapambano yake mawili ya mwisho nje ya nchi, moja dhidi ya Sam Eggington raia wa England na Raul Gonzalez wa Argentina, rekodi inayombeba dhidi ya Mjerumani huyo.

"Kwa uzalengo mkubwa kwa nchi yetu, Swahili Flix wameamua kuonyesha pambano hili kupitia mtandao wao ambao unaweza kushuhudia Mwakinyo akipigana kupitia simu ya mkononi, kompyuta kwa kuingia tovuti ya swahiliflix.tv," alisema kiongozi huyo.

# Michezo

Jumanne Machi 10, 2020

Nipashe





Malen akaribia kurejea Arsenal UKURASA 30



Rais John Magufuli (kulia), akifuatilia kwa makini mechi ya Ligi Kuu Bara kati ya Simba na Yanga iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe na Waziri wa Utamaduni, Michezo na Vijana wa Zanzibar, Balozi Ali Karume. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: IKULU**

## Mapato Simba, Yanga yaanikwa

**Na Mwandishi Wetu**

MECHI ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya watani wa jadi nchini, Simba na Yanga iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi imeingiza Sh. milioni 545.4 imeelezwa.

Taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ilisema mechi hiyo namba 270, ambayo iliyomalizika kwa wenyeji Yanga kupata ushindi wa bao 1-0, ilihudhuriwa na mashabiki 59,325.

Kiingilio cha chini katika mechi hiyo kilikuwa ni Sh. 7,000, huku cha juu kwa upande wa VIP A kilikuwa ni Sh. 30,000.

Hata hivyo baadhi ya mashabiki ambao walikuwa na tiketi walishindwa kuingia uwanjani kushuhudia mtanange huo kutokana na msongamano uliokuwapo katika mashine ya ukaguzi.

Rais John Pombe Magufuli alihudhuria mchezo huo ambao mgeni rasmi alikuwa ni wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), huku idadi kubwa ya mashabiki waliohudhuria walikuwa ni wa Wekundu wa Msimbazi.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Januari 4, mwaka huu, timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2.

# EYMAEL AFUNGUKA ALIPOIBANA SIMBA

### ●●● Lakini akata tamaa kutwaa ubingwa na kuweka wazi malengo yake ni kumaliza katika nafasi pili...

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya watani zao Simba, Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael amesema matokeo hayo mazuri waliyopata yalitokana na kufanyia kazi ubora wa kikosi cha vinara na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Bao pekee katika mchezo huo lilifungwa na Bernard Morrison, ambaye alimtungua kipa wa Simba, Aishi Manula kwa mpira wa adhabu uliozama wavuni baada ya kuchezewa rafu na Jonas Mkude nje kidogo ya eneo la 18.**

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Eymael alisema alikuwa akiwafuatilia wapinzani hao mara kadhaa walipokuwa wakicheza na kufanyia kazi ubora na mapungufu ya kikosi chao.

Eymael alisema kitu alichofanikiwa ni kudhibiti safu ya kiungo ambayo mechi zake tatu zilizopita, Simba ilicheza vizuri ikiongozwa na Mzambia Clatous Chama na Mkenya Francis Kahata.

"Vijana wangu wamecheza vizuri, wamefanyia kazi yale yale tuliyokuwa tukifanya mazoezini na kufanikiwa kupata pointi tatu muhimu katika mchezo wetu huu dhidi ya Simba, ila haikuwa mechi rahisi," alisema Eymael.

Mbelgiji huyo alisema baada ya matokeo hayo, wanaenda kujipanga kwa mara nyingine kwenda kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo wa ligi hiyo unaofuata dhidi ya Namungo FC.

"Nina furaha na kumshukuru Mungu kwa kupata ushindi dhidi ya mabingwa wajao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hatukucheza kama 'dabi', tulicheza kama fainali, ingawa tulipoteza nafasi kadhaa, kama ile ya Nchimbi 9 (Ditram), lakini malengo yangu ni kumaliza katika nafasi ya pili, naamini kila mmoja atakuwa na furaha," Eymael alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck amewaomba radhi mashabiki wa timu hiyo kutokana na matokeo mabaya waliyoyapata katika mchezo huo watani wa jadi ambao ulihudhuriwa na Rais John Magufuli na Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Ahmad Ahmad.

Sven alisema wachezaji wake walishindwa kutumia vema nafasi nyingi walizozitengeneza katika mchezo huo na wapinzani wao wametumia mapungufu waliyoyaonyesha na hatimaye kupata ushindi.

"Ni matokeo ya kuumiza, mashabiki wasikate tamaa, tumepata nafasi nyingi lakini hatujazitumia, mpira ni mchezo wa makosa, tunajipanga kwa ajili ya kufanya vizuri katika michezo ijayo," alisema kocha huyo.

Aliongeza wanajipanga upya kwa ajili ya kupata ushindi katika mechi zinazoendelea ili kuhakikisha wanashinda kufikia malengo yao ya kutwaa ubingwa.

Nahodha wa Simba, John Bocco alisema timu yao haikuwa katika kiwango kizuri katika kipindi cha kwanza, lakini malengo yao ya kutetea ubingwa bado hayajapotea.

"Wapinzani wetu walikuwa vizuri na walitumia nafasi moja waliyoipata tofauti na sisi tulishindwa kuwa makini kuzitumia nafasi tulizozipata, tunajua hali ya mashabiki, kwa upande wetu pia imetuumiza, hivyo tunawaomba radhi na waendelee kutupa sapoti kwani mechi bado zipo nyingi tutafanya vizuri," alisema Bocco.

Vigogo hao wa soka nchini wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya mechi zao zinazofuata ambapo Simba itawakaribisha Singida United hapo kesho huku KMC FC ambayo inapambana kujinusuru na janga la kushuka daraja ikiwaalika Yanga.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >